ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad Nafasi za Wanawake

42.Mhe. Farida Amour Mohammed Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Fatma Mbarouk Said Jimbo la Amani

44.Mhe. Hamad Masoud Hamad Jimbo la Ole

45.Mhe. Hamza Hassan Juma Jimbo la Kwamtipura

46.Mhe. Hassan Hamad Omar Jimbo la Kojani

47.Mhe. Hija Hassan Hija Jimbo la Kiwani

48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu Jimbo la Bububu

49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu Jimbo la Mji Mkongwe

50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub Jimbo la Muyuni

51.Mhe. Kazija Khamis Kona Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid Jimbo la Kiembesamaki

55.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

57.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 19 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuwasilisha Hati Mezani leo tunao wageni maalum wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wageni hawa jumla yake ni 20, ambao ni wageni wa Kamati za Skuli tatu za Pete, Muyuni na Kitogani. Naomba wageni hao 20 kutoka Kamati za Skuli hizo sasa wasimame, wale pale. *(Makofi)*

Karibuni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha hati mezani yenye mnasaba na Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2011/2012. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2011/2012. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mwaka 2011/2012. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Assaa Othman Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa mwaka 2012/2013. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 82

Malipo ya Elimu ya Juu Kutoka Bodi ya Mikopo

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa Bodi ya Mikopo ya Jamhuri ya Muungano ni ya pande zote mbili za Jamhuri. Kwa kuwa Zanzibar mara nyingi wanaopata mkopo huwa wachache kutokana na kuingizwa kwenye kapu la pamoja la maombi hayo, jambo ambalo hupelekea aidha kushindwa ama kwa sifa au tofauti ya vipaumbele baina ya Bara na Zanzibar.

Je, ni lini SMZ itawataka wenzetu wa Bara fedha za mkopo huo kwa upande wa Zanzibar zikatolewa katika fumula ya 4.5 kama vile Zanzibar inavyopata katika mambo mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru sana na kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82.

Mhe. Spika, kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania ni chombo cha Muungano kinachotoa mikopo kwa wanafunzi wa pande zote mbili za Muungano wa Jamhuri ya Tanzania na kuwawezesha kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu. Bajeti ya chombo hicho inajadiliwa na kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo matumizi yake yote yanapaswa kupelekwa katika vikao vya Bunge.

Vile vile mgao wa asilimia 4.5 unaotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Zanzibar unatokana na faida ya Benki Kuu na fedha za misaada ya wahisani zenye masharti nafuu. Kwa hivyo, asilimia hiyo haihusiani na mgao wa kasma ya mgao wa bajeti ya ndani inayoidhibishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, ni kweli kuwa vigezo vya utoaji wa mikopo wa chombo hicho vinazingatia sifa za muombaji, fani za kipaumbele na hali ya umasikini wa familia ya mwanafunzi.

Vigezo za fani za vipaumbele na sifa za juu ya muombaji zinatokana na Bodi ya Mikopo ya Zanzibar, kwa kutumia vigezo hivyo baadhi ya waombaji kwa upande wa Zanzibar wanapata mikopo inayotolewa na Bodi ya Muungano wa Tanzania na baadhi wanakosa, mikopo kupitia chombo hicho hupata mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Kwa hivi sasa serikali haina mpango wa kuomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuweka utaratibu wa mgao wa asilimia 4.5 kwa Zanzibar kwa fedha za Bodi ya Mikopo ya Jamhuri wa Tanzania. Kwa hivyo, ni vyema matumizi kama haya yakasubiri mapendekezo ya Kamati ya Pamoja ya Fedha, ambayo inaendelea kufanyiakazi masuala mbali mbali ya mgao wa fedha kwa serikali zetu mbili.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi tufanye subira mpaka Kamati ya Pamoja ya Fedha itakapotoa ripoti ya mapendekezo yake. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo sana kabisa la nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mfuko huu ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hupatikana kupitia kodi za wananchi kutoka pande zote mbili za Jamhuri. Je, itakuwa vyema au ni kuwatendea haki wazanzibari kuwanyima mikopo hii kwa kushindwa ku-*meet demands* za Mfuko huu ikiwemo *qualifications* pamoja na vipaumbele.

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar ni nchi na inategemea sana wataalamu katika kufanya mambo yake na kwa kuwa elimu ni ufunguo wa maisha. Je, kumnyima mzanzibari elimu kwa kumnyima mkopo huu si kuwarudisha nyuma wazanzibari, ili kuendelee hizo kero za Muungano.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika,

(a) Kumnyima mwanafunzi mkopo kwa kuzingatia vipaumbele si kwa Jamhuri ya Muungano tu, hiyo hata kwa sisi Zanzibar serikali yoyote Mhe. Spika, ili iende na mipango yake iwe imara basi ni lazima waweke vipaumbele. Kwa hivyo, mimi sione tatizo kama mwanafunzi wa Zanzibar atakosa huu mkopo kwa sababu amekosa kipaumbele ambacho kimewekwa.

Mhe. Spika, naomba arudie swali lake la (b) Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, swali la (b) lilikuwa ni kwamba elimu ni ufunguo wa maisha na ndio usukani ya maendeleo ya taifa lolote. Je, wenzetu wa Tanzania Bara kutunyima mfuko huu kwa kushindwa ku-*meet* hizo *demands* zao, si kuturudisha nyuma kielimu na kimaendeleo na hatimaye kuzidisha hizo kero za Muungano.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nataka nikiri kwamba sio kweli kama wenzetu Bara wananyima wanafunzi wetu wa Zanzibar mikopo. Kwa mfano, katika mwaka huu kwenye Bodi yetu ya Zanzibar tulibaini kama kuna wanafunzi karibu 237 ambao sisi tumewapa mkopo na kule wamepata mkopo. Sasa tutizame 237 ni wale tu ambao tuliwabaini wameomba pande mbili mbali wale ambao hawakuomba kupitia kwetu, isipokuwa wameomba moja kwa moja, hivyo ni dhahiri kwa mikopo hii hawanyimwi.

Lakini kama nilivyosema ni kwamba lazima serikali ambayo inataka iende, ilete maendeo katika nchi yake, basi lazima izingatie vipaumbele vya nchi yake na mahitaji kwa jumla.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante hivi Mhe. Naibu Waziri anaweza kutueleza mfumo gani hivi sasa uliopewa kipaumbele, ili wanafunzi wajue masomo gani ambayo yamepewa kipaumbele. Kwa kweli kuna taarifa kwamba wale wanaosoma masomo ya dini hawanufaiki na mkopo huo Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, takriban kwenye Bodi yetu ya Mikopo kwa hivi sasa basi ni fani tatu mpaka nne tu ambazo hatuwapi mikopo ni *Public Administration*, Dini na Kiarabu kwa wale wanafunzi wapya, kwa wale wanafunzi ambao ni walimu wako skuli basi tunawapa mikopo.

Mhe. Spika, tunafanya hivyo kwa sababu tunao wanafunzi wengi ambao wamesoma Dini na Kiarabu lakini bado hawajapata ajira. Kwa hivyo, hata ule uwezekano wa kupewa mikopo hii na kusoma na baadaye wakaajiriwa kwa hivi sasa ni mgumu na fedha hiyo hiyo ndio tunahitaji tuwape wanafunzi wengine.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika. *(Makofi)*
Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mnajua Mhe. Mwakilishi alikamata kichwa na nikasema sasa nitamuumiza na nikaona nifanye busara kidogo. Mhe. Mjumbe karibu. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa wakati tulionao mikopo ni lazima kwa wananchi wetu hasa kutokana na hali yao ya umasikini, ili waweze kuendelea na masomo.

Lakini katika uzoefu wangu na ushahidi ninao ni kuwa tunao baadhi ya vijana huwa wanaomba mkopo huu wa Zanzibar na kwa sababu ya vigezo huwa hawapati, lakini watu wale wanapohangaika Bara huwa wanapatiwa mikopo wanasoma na halafu wanakujafanya kazi huku. Kutokana na hali hiyo, hatuoni kuwa sisi wale wenzetu wanatuhurumia zaidi kuliko sisi wenyewe kama vile ilivyo Daftari la Kujiandikisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza nishukuru Mhe. Mwakilishi amehisi kwamba wenzetu wanatuonea huruma zaidi na huu ndio udugu unavyotakiwa. Lakini mimi niseme kama tunatoa mkopo Mhe. Spika kwa ajili ya uwezo ambao tunao, bajeti ambayo tunayo inapitishwa ndani ya Baraza hili na waombaji siku zote wanakuwa ni wengi kupita uwezo wa ile bajeti ambayo tunayo.

Kwa kweli tunajua kama mkopo ni muhimu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutoa mikopo kadri ya hali ya fedha tutakavyozipata kwenye bajeti. *(Makofi)*

Nam. 109

Kuwekwa Matuta Barabara inayopita Skuli za Muungoni, Kitogani, Muyuni, Bwejuu na Pete

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 109 ambalo limekuwa kero kwa wananchi wangu wa Jimbo la Muyuni hata na mimi wakati mwengine hutumia vidonge vya usingizi kulala kwa suala hili. *(Makofi)*

Kwa kweli jambo hili ni zito Mhe. Spika na hii leo wananchi wamekuja wenyewe kwa kukodi gari yao wenyewe kuja kusikiliza juu ya serikali yao sikivu, kwa mujibu wa Sheria na Katiba za nchi hii, wananchi hawa mimi wameniajiri na kwa bahati mbaya sikupata jimbo kutoka Ikulu Mhe. Spika, ni muajiriwa wa wananchi wa Jimbo la Muyuni wameniamini na tulikuwa karibu timu ya mpira watu 11 tukigombania kiti hichi na wakaniamini kunipa u-*captain*, ili nije niwakilishe katika chombo hichi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, sasa uliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, naomba swali langu Nam. 109 lipate jawabu, serikali sikivu kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Kumekuwa na kilio cha muda mrefu sasa kwa wananchi wa maeneo ya Muungoni, Kitogani, Muyuni na Bwejuu, kuomba barabara zinazopita maeneo yao ziwekwe matuta, kama zilivyowekwa barabara nyengine. Kwa mfano, Mwera ambayo ina matuta zaidi ya 20 na hata hii ya Mbweni – Chukwani ambapo hakuna skuli nyingi. Jambo la ajabu kuona uwekwaji wa matuta unafanywa kwa ubaguzi wa barabara fulani kinyume na misingi ya Katiba yetu ya Zanzibar ya 1984, ambayo inataka wananchi wote wapate fursa na haki sawa bila ubaguzi wowote.

(a) Je, ni kwa nini barabara za Muungoni, Kitogani, Muyuni na Bwejuu haziwekewi matuta kunusuru wapita njia na wanafunzi walioko jirani na barabara hizo.

(b) Je, inakuwaje barabara zipuuzwe kuwekewa matuta wakati barabara inayopita Msitu wa Jozani imewekwa matuta kuwanusuru Kima Punju wasipondwe na gari, hivi kweli kima ni bora kuliko binaadamu wa Kitogani, Muyuni, Bwejuu na Pete.

(c) Serikali inatoa ahadi gani ya kuweka matuta kwenye barabara hizo haraka sana kwa wananchi wa Muungoni, Muyuni, Bwejuu na Pete ambao hivi sasa wanasikiliza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali langu Nam. 109 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba nichukue nafasi hii kuwakaribisha jamaa zangu wanaotoka katika Jimbo la Muyuni na mimi nikiwa mdau katika Jimbo la Muyuni, kwa kutambua tu kwamba na mimi ni mtu wa Bwejuu. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Spika naomba nianze kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-
Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya juhudi za makusudi za kujenga barabara zenye ubora Unguja na Pemba, ili kuwawezesha wananchi wake kusafiri na kusafirisha bidhaa zao kutoka sehemu moja kwenye sehemu nyengine kwa wakati wowote kwa gharama nafuu na kwa haraka kwa kutumia usafiri wa magari, pikipiki ama baskeli.

Hata hivyo, baadhi ya madereva wamekuwa wakidhani kuwa barabara hizo wanastahiki kutumia wao peke yao, ambapo huendesha magari yao kwa mwendo wa kasi pasipokuzingatia alama za barabarani na usalama wa watumiaji wengine. Kutokana na mwenendo huo wa kasi ajali zimekuwa nyingi zikitokea kwenye maeneo mbali mbali ya nchi yetu na kusababisha majeruhi, ulemavu na hata vifo kwa baadhi ya watu waliopata ajali.

Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imekuwa ikichukua juhudi za makusudi za uwekaji wa alama za barabarani, lakini kuna baadhi ya watu huhujumu alama hizo kwa kuzingatia matumizi binafsi na hivyo kulazimika kuweka matuta kwa baadhi ya maeneo yenye msongomano mkubwa wa watu kama vile maskuli, misikitini, vyuoni na kadhalika au kuwalazimisha madereva kupunguza mwendo wafikapo maeneo hayo.

Mhe. Spika, kutokana na ongezeko la watu wanaojenga kando kando ya barabara sambamba na ujenzi wa maskuli na masoko kwenye maeneo hayo na madereva kutozingatia usalama wa barabarani ajali za barabarani zinazidi kuongezeka kila mwaka.

Hivyo, kuna baadhi ya maeneo wananchi wamekuwa wakijichukulia sheria mikononi mwao kwa kujenga matuta barabarani bila ya kupitia taratibu za Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, jambo ambalo ni uvunjaji wa sheria za nchi. Maeneo yaliyokithiri kwa kuweka matuta barabarani ni yale ya Mkoa wa Kaskazini na hasa katika Wilaya ya Kaskazini ‘A’.

Baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Serikali inafahamu umuhimu wa usalama barabarani kwa raia wake na imekuwa ikichukua juhudi za kupunguza ajali hizo kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya awali. Aidha Jeshi la Polisi nalo limekuwa likichukua jitihada ya jamii pamoja na maskuli juu ya usalama. Kutokana na elimu hiyo, wananchi hawana budi kuzingatia mafunzo hayo, ili kuepusha ajili ambazo zinaepukika.

Kuhusiana na suala la uwekaji wa matuta barabarani mara inapotokea tukio la ajali sio suluhisho la kupunguza ajali barabarani, isipokuwa suluhisho sahihi ni kufuata sheria za usalama barabarani kwa watu wote wanaotumia barabara.
Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi wake kupitia taasisi zake ikiwemo Idara ya Usalama na Leseni na tayari inaandaa mkakati wa kuwachukulia hatua za kisheria wale wote

wanaovunja sheria za usalama barabarani wakiwemo madereva wanaoendesha magari kwa mwendo wa kasi bila ya kuzingatia usalama huo. Aidha abiria wao na watu wengine wanaotumia barabara.

Hivyo, suala la uwekaji matuta kwenye barabara alizozitaja Mhe. Mjumbe haipo na badala yake zitawekwa alama husika kwenye maeneo ambayo alama hizo hazipo. Kutokana na hali hiyo, serikali hatutoi ahadi ya kuweka matuta, zaidi ni kuwaelimisha watumiaji na kuweka alama stahiki katika barabara hizo alizozisema Mhe. Mwakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru. Kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa, naomba niongezee kidogo kuhusiana na hali ya matuta kwa njia za Zanzibar na swali lililoletwa leo.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba maombi haya tunayo katika wizara, lakini tumetokezewa na changamoto ambapo watu wamechukua sheria mikononi wamejenga matuta kwa hiari zao bila ya kupitia Idara ya UUB au Wizara ya Mawasiliano, matuta yale yameharibu mtandao mzima wa njia.

Kwa hivyo, hivi sasa imezuiliwa kujenga matuta pahala mpaka hapo itakapokuwa na utendamano wa wapi pawekwe matuta na njia bado ibaki katika hali ya usalama na iwe barabara ya kweli na sio iwe barabara kama ambapo tunalima.

Mhe. Spika, maombi yote haya tunayo na wala wizara haijakataa kuweka matuta pahala ambapo panastahiki. Lakini tatizo liliopo ni kwamba zile ni barabara na zinahitaji kupita.

Jambo jengine ni kwamba uzuiaji wa magari kwenda kwa kasi kuna alama nyingi za barabara. Tatizo kubwa ni kwamba madereva wengi hawafuati alama za barabarani na wanaendesha mwendo wa kasi. Kwa hiyo, kuna mtandao mwengine ambao unaandaliwa, ili kuona kwamba sheria za barabara zinafuatwa. Mhe. Spika, wiki ijayo tarehe 22/04/2013 tunazindua Wiki ya Usalama Barabarani, ambayo itazinduliwa rasmi katika Hoteli ya Bwawani, kwa ajili ya kuweka wazi namna gani ya utumizi wa barabara.

Hivyo, tunamhakikishia Mhe. mwakilishi, kwamba wakati linaendelea hili basi awe na uvumilivu, ili kuona hasa idara kupitia wizara yake ni wapi hasa panastahiki kuwekwa matuta na sio kuweka matuta kiholela, ambapo sasa kumesababisha hata watu wa Kaskazini kuleta tena madai kwamba matuta yamezidi na gari haziwezi kwenda. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri pamoja Naibu Waziri kutokidhi swali la msingi tokea niingie Baraza hili Mhe. Spika, narudia tena kwamba ni muajiriwa wa wananchi wa Jimbo la Muyuni nimezungumza mara ya kwanza, pili na tatu na hata leo wananchi wangu wamefika wakati hawaniamini kama nasemea chombo hichi na hichi ni chombo cha wananchi.

Hivi leo kweli kuna sababu gani ya msingi mpaka Mhe. Rais anapiga kelele njia ya Mwera kuwekwa matuta zaidi ya 30 kweli ndio Katiba yetu hii kifungu cha 13 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 13(1)(2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinaeleza hivi:-

(1) “Kila mtu anayo haki ya kuwa na hifadhi ya maisha yake.

(2) Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa familia hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria”.

Mhe. Spika, leo Kima Punju wamekuwa bora kuliko wananchi wale mnatwambia nini, hivi serikali hii sikivu kweli hii na wale wananchi hawana umuhimu kuliko Kima Punju na huu sio uwajibikaji. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Naibu Waziri aniambie kuna sababu gani wengine kupewa haki hii na wengine wasipewe na huo si ubaguzi wa Katiba ya nchi hii na wananchi wamechoka wale. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba aulize swali, kwa sababu alikuwa akitoa maelezo na nilikuwa nasubiri aletwe swali kwani alikuwa akitoa maelezo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, katika Naibu Waziri anayezungumza humu kwa kujiamini bila ya kujali wananchi yeye ni mmoja na mimi hata nikamuuliza swali itakuwa sawa na kumpigia kengele paka na wala hawezi kunijibu Mhe. Naibu Waziri mimi. Kwa hivyo, tuendelee hivi mpaka baadaye tutajua jambo la kufanya.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, weka swali lako vizuri la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kifungu cha 13 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, naomba kunukuu kidogo.

Kifungu cha 13(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinaeleza hivi:-

“Kila mtu anayo haki ya kuwa na hifadhi ya maisha yake”.

Sasa ni sababu gani zilizopelekea wananchi wale wasipate hifadhi yao Skuli ya Pete, Kitogani na Muungoni na hizi Katiba tunatunga sisi wenyewe humu ndani ni sababu gani hebu tuwaeleze wananchi wapate kufahamu na Katiba ya Zanzibar iko wazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nadhani Mhe. Mwakilishi hasikilizi majibu yanayotoka upande wa serikali. Kwa kweli maelezo tumeyatoa marefu sababu zipi za msingi za kuweka matuta na Mhe. Waziri ameongezea majibu kwamba maombi yapo serikalini na hivi sasa kuna tatizo kwamba kuna uvamizi wa watu wanaoweka matuta kiholela na wala hatuwezi kukurupuka kama serikali tukasema kesho tukafanye jambo kwa sababu ya tempa ya watu. Serikali inaendeshwa kwa utaratibu, sheria, kanuni na kufuata haki na usawa kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, alichoahidiwa na serikali ni kwamba haya ni maombi yamekuja serikalini, yamepokelewa na utaratibu unaandaliwa na baadaye hiyo huduma itafika kwa wananchi. Kwa mfano, mimi mwenyewe Mhe. Spika nimekwenda Bwejuu tumefanya kikao na Shehia ya Bwejuu na uongozi wao tukakubaliana.

Kwa hivyo, utaratibu ni kwamba twende yaletwe wizarani na Bodi yetu ya Usalama Barabarani ikae na wao wanakwenda kujiridhisha na baadaye maombi yanakuja kwenda kuanza utaratibu wa kuweka matuta na huo ndio utaratibu wa kuendesha sheria na nchi ambayo inaheshimu Haki za Binadamu na Usawa mbele ya sheria. Kwa kweli usawa mbele ya sheria Mhe. Spika hauendeshwi kwa utashi wala mahitaji ya mtu binafsi, isipokuwa usawa mbele ya sheria unaendeshwa kwa taratibu na muongozo unaotoka serikalini.

Sasa muongozo wa serikali maombi yanakuja yanazingatiwa, vyombo husika vinakwenda kujiridhisha na baada ya kujiridhisha basi serikali inachukua hatua na ndicho ambacho serikali tumeahidi na ndivyo tutakavyofanya, hatutafanya kwa utashi wa mtu wala joto la mtu, isipokuwa tutakwenda kwa mujibu wa utaratibu serikali ambao tumeupanga. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante nikushukuru kunipa nafasi hii. Vile vile nimshukuru Mhe. Naibu Waziri pamoja na Mhe. Waziri kwa majibu na mimi swali langu ni dogo sana.

Kwa kuwa tatizo la kuweka matuta linatokana na baadhi ya madereva kutokutii sheria za nchi na wizara imeshajitahidi kuweka alama za barabarani na baadhi ya maeneo kuweka matuta. Lakini kwa kuwa nchi za wenzetu na hata Tanzania Bara wamejaribu kwenda na mfumo wa kisasa wa kuweka *camera* barabarani.

Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, je wizara yake haoini kwamba njia mbadala ya kuwadhibiti wale watu ambao hawafuati alama za barabarani katika ulimwengu huu wa kisasa ni kuweka *camera* barabarani, ili wale watakaobainika wanakwenda kinyume kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, wazo la Mhe. Mjumbe ni zuri lakini tunatambua kwamba wazo hilo linahitaji gharama na kwa muda huu tunachoweza kufanya ni kulipokea wazo na pale tutakapokuwa na uwezo wa kifedha linafanyiwa kazi. Lakini kwa hivi sasa hatuwezi kulifanyia kazi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hebu tumsikilize Mhe. Naibu Waziri na tusiwe na vikao vyengine. Mhe. Naibu Waziri endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, wazo alilokuja nalo Mhe. Mwakilishi ni wazo jema tena ni zuri. Lakini utekelezaji wake bila ya shaka unahitaji gharama na maendeleo ya kisayansi hatua ambayo kwa hivi sasa bado huatujaifikia. Tunachoweza kukisema kwamba tumelipokea na pale ambapo hali ya uwezo itaruhusu tutalifanyia kazi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa wizara hii ndio inayo dhamana ya kuweza kutujengea

matuta ambayo yapo katika kiwango, na hivi sasa kama alivyokiri Mhe. Naibu Waziri kwamba imejitokeza watu kwamba wanajenga matuta yale wenyewe kwa kuona labda wizara imechelewa kuwajengea na matuta hayo yako chini ya kiwango yani ni usumbufu kwa gari. Nimeshashuhudia mara nyingi machupa ya soda yakianguka katika matuta hayo, lakini pia gari kwa kweli zinapata msukosuko mkubwa kupita katika matuta hayo.

Je, ni lini Mhe. Waziri kwa kuwa yeyé ndiye mwenye dhamana hii ataweza kuturekebishia zile sehemu ambazo tayari matuta hayo yameshawekwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ili twende vizuri katika kuona kwamba jambo hili linapata pahali ambapo linasita, hatua ya kwanza ni serikali kuwatafuta waliohusika na uwekaji wa matuta haya kinyume na sheria ili kuona kwamba sheria inachukua mkondo wake.

Hatua ya pili kuhakikisha kwamba idara husika zinakwenda kuangalia maeneo hayo na kurekebisha ili kuweza kuona kwamba malengo yale ya matuta yanafikiwa lakini pasina kusababisha matatizo kwa watumiaji wengine wa barabara.

Nam. 97

Changamoto Zinazowakabili Walemavu Nchini

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

(a) Tarehe 3 Disemba kila mwaka huadhimishwa siku ya Walemavu Duniani, na miongoni mwa changamoto zinazowakabili ni kuwapatia elimu pamoja na ajira. Kwa niaba ya wananchi ningependa kujua ni ajira ngapi zimeshatolewa kwa ajili ya walemavu.

(b) Je, kuna mfuko maalum wa kuwasaidia watoto wenye ulemavu kuweza kusoma kwa kuwapatia mikopo na ruzuku ili waweze kufikia malengo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 97 lenye vifungu a na b naomba kutoa maelezo mafupi sana yafuatayo:

Mhe. Spika, naomba Mhe. Mwakilishi akubaliane na mimi kwamba suala la ajira linaambatana na sifa za kuajiriwa katika ngazi yoyote ile ya nafasi ya kazi, na ndio maana suala hili linaendelea kuwa ni kikwazo kulipatia ufumbuzi wa haraka. Aidha, suala hili linahitaji mipango ya muda mrefu ili kuwajengea uwezo watu wenye ulemavu kielimu na wao waweze kuingia katika soko la ajira bila ya matatizo.

Kwa idhini yako sasa Mhe. Spika, naomba kujibu swali nambari 97 la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Baraza la Watu wenye Ulemavu lilifanya vikao viwili ili kujadili suala hili la ajira kwa watu wenye ulemavu. Kimoja kilikuwa pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi Serikalini

na cha pili kilimhusisha pia Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Katibu wake wa Tume ya Utumishi Serikalini pia na Naibu Katibu Mkuu wa ofisi hiyo. Suala hili la ajira kwa watu wenye ulemavu lilionekana linakumbana na changamoto zifuatazo:

Kwanza ukosefu wa sifa za kuajiriwa katika kada mbali mbali za kazi kwa watu wenye ulemavu.

Pili watu wenye ulemavu wenyewe kutoomba nafasi za kazi zinapotangazwa ukizingatia kwamba sheria Nam. 2 ya Utumishi wa Umma inamlazimisha mtu kuomba kazi anayoitaka na sifa aliyonayo pale inapotangazwa.

Lakini pia ilionekana kwamba sheria ya Utumishi wa Umma inatoa fursa ya upendeleo kwa watu wenye ulemavu pale inapotokea watu wawili wenye sifa sawa kutaka kuajiriwa katika nafasi ya kazi basi kipaumbele hupewa mtu mwenye ulemavu.

Mhe. Spika, hakuna idadi kamili iliyorikodiwa na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusiana na watu wenye ulemavu ambao wameajiriwa. Na ni kwa sababu ofisi hii inapoajiri watu haibagui kwamba huyu anayeajiriwa ni mlemavu kwa sababu sheria inayotambua haki na fursa za watu wenye ulemavu inakataza kufanya hivyo. Watu wenye ulemavu wanapata *treatment* matibabu sawa sawa na watu wengine kwa sababu wana haki ya usawa. Kwa hivyo, hakuna takwimu katika Ofisi ya Utumishi wa Umma inayoelezea watu wenye utumishi wangapi wameajiriwa.

Hata hivyo, hivi karibuni tunaweza kupata takwimu hii kutokana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Watu wenjye Ulemavu kukusanya takwimu za watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya shehia hadi mkoa kwa mikoa yote mitano. Takwimu hii inahusisha aina ya ulemavu ambao mtu anao, wapi wanaishi na shughuli anayofanya katika kujipatia rizki yake ya kuishi siku hadi siku. Nina imani kukamilika kwa ukusanyo wa takwimu hii pamoja na uchambuzi wake kutaweza kutupatia uhalisia wa watu wangapi ambao wana ulemavu wameajiriwa katika ofisi na taasisi zetu mbali mbali za serikali, lakini pia katika taasisi binafsi.

Jibu (b) Mhe. Spika, suala la Mfuko Maalum kwa watoto wanaoishi na ulemavu peke yao halipo wala Mfuko huo haujaanzishwa. Mfuko uliopo ni Mfuko unaohusisha watu wote wenye ulemavu, ambao Mfuko huu umeanzishwa kutokana na matakwa ya kifungu cha 38(1) cha Sheria Nam. 9 ya Watu wenye Ulemavu, ambapo hivi karibuni nyote mmeshuhudia kwamba umeanzishwa na tumeuchangia na Mfuko huu ni endelevu utaendelea kuchangiwa.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inaendelea kutoa elimu bila ya malipo kwa jamii nzima ya Zanzibar na pia imeanzisha kitengo maalum cha Elimu Mjumuisho ili kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanapata haki yao ya msingi ya kupata elimu. Lakini vile vile Wizara ya elimu na Mafunzo ya Amali inao Mfuko kwa ajili ya kuwasomesha wanafunzi wote bila ya kubagua wale ambao wanataka kuendelea na elimu ya juu, Mfuko huu haubagui. Kwa hivyo, hakuna Mfuko maalum uliotengwa kwa ajili ya kuendeleza watoto wenye ulemavu kwa sababu nao hao ni sawa sawa na watoto wengine ambao wako kwenye jamii yetu.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kasema hawana takwimu maalum, awaoni kwamba sasa kuna haja ya kuandaa takwimu ya kuwajua ni wangapi walemavu ambao wanapata ajira na wangapi ambao wanastahiki kupatiwa mikopo au kuwezeshwa katika mambo mbali mbali yanayowahusu walemavu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, nimeeleza katika jibu langu mama kwamba takwimu hii tuna tamaa hivi karibuni tutakuwa nayo kwa sababu ofisi yangu kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu imekusanya na inaendelea sasa hivi iko katika hatua za mwisho kabisa kukusanya takwimu za watu wenye ulemavu kuanzia ngazi ya shehia hadi mkoa kwa mikoa yote mitano ya Zanzibar. Takwimu hizi zinahusisha aina ya ulemavu ambayo mlemavu huyo anayo, aina ya elimu ambayo anayo, kama mlemavu huyo ana ajira au hana iwe ya serikali au katika taasisi binafsi. Kwa hivyo, nimesema kwamba, suala hili ofisi yangu inalifanyia kazi na takwimu hii itapatikana.

Lakini naomba nimtoe mashaka tu Mhe. Fatma Mbarouk, kama kuna kikundi cha watu wenye ulemavu ambacho kimejikusanya kwa pamoja katika kufanya shughuli zao, basi Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika haibagui katika kuwapa watu hawa mikopo na kuwasaidia kufanya shughuli zao. Naomba sana tuwashajihishe wende kutafuta rasilimali hii katika kujiendeleza.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Waziri alisema kwamba watu wenye ulemavu wanapewa haki zao sawa na watu wengine. Je, nilitaka kufahamu haki hizo ni kama zipi.

Pili, ni walemavu wangapi wanaofanya kazi katika maofisi ya serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, watu wenye ulemavu wanastahiki kupata haki sawa kama ilivyoainishwa katika Katiba yetu ya Zanzibar ambayo tunayo na haki za Mwananchi wa Zanzibar zimeelezwa mule. Lakini pia wana haki za kupatiwa haki na fursa zote zinazoelezwa katika mikataba ya kimataifa kuanzia haki za binadamu, haki za kupata elimu na nyenginezo, mikataba ambayo Tanzania imeiridhia yote watu wenye ulemavu wana haki ya kupata haki hizo sawa na wengine.

Kuhusu swali lake la pili Mhe. Spika, nitaeleza sasa kwa mara ya tatu, kwamba ofisi inayohusika na uajiri ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa sasa haina takwimu maalum ambayo inaweza kutueleza imeajiri watu wangapi wenye ulemavu na ni kwa sababu sheria ya Watu wenye Ulemavu inakataza unapotaka kumuajiri mtu kutaka kujua kwamba wewe ni mlemavu au si mlemavu. Isipokuwa kama taarifa hiyo itaisaidia ofisi katika kutoa kipaumbele ikiwa wapo watu wanaoshindana ambapo mmoja ni mwenye ulemavu. Kwa hivyo, ofisi hii haina takwimu hiyo kwa sasa.

Nimeeleza ofisi yangu kwa njia ya kukusanya takwimu katika mikoa mitano baada ya muda mfupi takwimu hii tutakuwa nayo na Mhe. Spika, naahidi nitakapoipata tu itapokuwa tayari nitaiwasilisha katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. WAziri nimemsikia sana majibu yake mazuri aliyoyatoa, lakini kwa kuwa walemavu ni watu wa kusaidiwa kwa hali na mali, na kutowasaidia walemavu sikuwatendea haki. Sas akwa kuwa hivyo ndivyo ilivyo nauliza ikiwa sheria yetu inaweka sawa kwa mtu mlemavu na asiyekuwa mlemavu kuwa na maksi sawa katika kupata kazi.

Je, haoni kam akuna haja ya sheria hii kuifanyia marekebisho ili kuwawekea fungu maalum walemavu ili wapate ajira na wao waingie. Kwa sbabu kumuwekea sawa na mu ambaye hana ulemavu basi ni kumuonea kwa sababu wao ni watu wa kusaidiwa.

La pili, katika skuli zetu kuna elimu mjumuisho yaani watu wenye ulemavu na wasiokuwa na ulemavu wanachanganyika. Lakini wakati wa kufanya mitihani maksi zao zinakuwa sawa sawa mwenye ulemavu na asiekuwa na ulemavu. Sasa je, kwa kuwa mtu aliyekuwa hana ulemavu anaona, anasikia ana kila kituna mwenye ulemavu haoni vizuri, hasikii vizuri anataka kusaidiwa.

Je, kwa kuwa wizara yake ndio inayoshughulikia watu wenye ulemavu amejipanga vipi kuwasiliana na Waziri wa Elimu kuona kuwa wanatoa maksi za upendeleo kwa watu wenye ulemavu ili kuwatendea haki na wao wapate kujisaidia kama wenzao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, napenda nimhakikishie kwamba kama atarejea kuisoma sheria yetu mpya ambayo tumeipitisha hapa ya Utumishi ataona kwamba kipaumbele kipo kwa watu wenye ulemavu. Lakini naomba nimpe mfano halisi, ambao huo inaonekana kabisa kwamba Ofisi ya Utumishi wa Umma ilifanya upendeleo mkubwa watu wenye ulemavu.

Ofisi ilitangaza nafasi ya kazi na katika waliyoomba ilikuwa imetaka mtu mwenye shahada ya kwanza. Lakini katika maombi ambayo iliyapokea mtu mwenye ulemavu mmoja aliomba nafasi hiyo akiwa yeyé na stashahada (*diploma*), lakini baada ya *interview* na kutizama nafasi ya kazi yenyewe Tume ya Utumishi ilipokaa ikaona huyu mtu mwenye ulemavu anaweza kutekeleza wajibu wa kazi ile. Naomba nikuhakikishie kwamba hapa Tume ya Utumishi ilimuajiri mtu huyo mwenye ulemavu. Kwa hivyo, katika hili tunatoa kipaumbele kikubwa sana.

Lakini hili la pili ni gumu na ni karibu kwamba kitu hakiwezekani. Kwa sababu Mhe. Spika, nataka sasa iweko mitihani maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu na kuwapa upendeleo ili waweze kusonga mbele katika elimu yao.

Mhe. Spika, kufanya hivyo ni kwamba tutamaliza kuwapata wanaohitimu watu wenye ulemavu ambao hawatakuwa katika viwango vya kuweza kuajirika na kutusaidia ndani ya jamii yetu. Tunachofanya kama serikali ni kuweza kuhakikisha tunatoa huduma mfano kwa kupitia Wizara ya Elimu kuna suala zima la kuwasomesha watoto kupitia elimu mjumuisho. Chuo cha Ualimu cha Mazizini Mhe. Spika, kinasomesha walimu wa kufundisha katika kutoa mafunzo ya elimu mjumuisho. Ofisi yangu ya Wizara ya Elimu inashirikiana katika kutafuta na kuhakikisha vifaa vya kufundishia na kuwasaidia watu wenye ulemavu vinakuwepo katika skuli hizi ili kuwawezesha waweze na wao kusoma kama wenzao na waweze kufanya vizuri katika mitihani yao.

Mhe. Spika, kufanya jambo ambalo halitakuwa kwa madhumuni mema kabisa katika kuwafanya watu wenye ulemavu kama hawana uwezo wa kiakili, kwamba hawawezi kufanya sawa na wenzao, ni kuwabagua watu hao na sheria ya Watu wenye Ulemavu inakataza na ni dhambi kufanya hivyo.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi lakini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ni mashahidi kwamba tunao watu wenye ulemavu katika ngazi ya juu ya vyombo vya maamuzi vya nchi hii wakiwa wame-*compete* sawa sawa kielimu na wengine ambao hawana ulemavu. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 96

Usambazaji wa Vizima Moto Katika Idara za Serikali

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

(a) Kutokana na muongozo wa Kimataifa juu ya usalama kazini ni kwa kiasi gani serikali imesambaza vizima moto (*portable fire extinguishers*) katika Wizara, Idara na katika Afisi za Umma.

(b) Na kwa kuwa ajali zinaweza kutokea popote, kuna juhudi zipi zimeanza kuchukuliwa kuwafundisha wafanyakazi na wananchi juu ya matumizi ya vifaa hivyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Fatma Mbarouk Said swali lake nambari 96 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kabla ya kujibu moja kwa moja naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Muongozo wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) nambari 174 wa mwaka 1993 kuhusu kinga ya ajali na madhara makubwa katika sehemu za kazi una lengo la kuzitaka nchi wanachama kuhakikisha kuwa zinachukua hatua madhubuti za kukinga ajali, kupunguza uwezekano wa kutokea ajali na kupunguza madhara ya jali na pia kuzingatia chanzo cha ajali.

Serikali kupitia Wizara yangu inafahamu kwamba moto ni chanzo kikubwa cha ajali zinazopelekea madhara makubwa ya hali na mali na hata kusababisha vifo kwa wafanyakazi na jamii kwa jumla. Kwa hivyo, serikali imetunga Sheria na Sera mbali mbali ili kukabiliana na hali hiyo. Kwa mfano:-

1. Sheria ya Usalama na Afya Kazini Namba 8 ya mwaka 2005

Inamtaka muajiri au mmiliki wa sehemu ya kazi kuhakikisha kuwa sehemu yake ya kazi inakuwa salama na si hatari kwa muajiri, mfanyakazi na jamii inayozunguka sehemu ya kazi. Kifungu cha 43 kinaeleza kuwa, kila muajiri anatakiwa ahakikishe kuwa kuna njia rahisi za kukimbia kutoka kwenye sehemu ya kazi pale inapotokea dharura hiyo. Kifungu

cha 83 kinamtaka kila muajiri kuhakikisha kuwa kuna njia za kuzimia moto zinazoweza kutumika kwa urahisi.

2. Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011

Kifungu cha 77 (1) kinaeleza kuwa, "Katibu Mkuu Kiongozi, kila Katibu Mkuu na kila Mkuu wa Idara au Taasisi anatakiwa achukue hatua za kuhakikisha kuwa mazingira ya sehemu ya kazi yanakuwa salama na si hatari kwa usalama na afya za watumishi wa umma kulingana na Sheria Namba 8 ya mwaka 2005, ya Usalama na Afya Kazini.

3. Sheria ya Zimamoto na Uokozi mwaka 1999

Kifungu cha 10(1) cha Sheria hii kinaeleza kuwa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kinaweza kuweka au kutoa maelekezo ya kuweka *"fire hydrants"* na mipango mengine ya maji kwa ajili ya kuzimia moto kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

(a) Jukumu la kuweka na kusambaza vifaa vya kuzimia moto *(portable fire Extinguishers)* kwenye Taasisi za Umma ni la kila Katibu Mkuu na Mkuu wa Taasisi husika kama ilivyoeleza Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya mwaka 2011.
Idara ya Usalama Kazini inapofanya ukaguzi inatakiwa kuhakikisha kuwa vifaa hivyo vipo, viko kwenye hali nzuri na vinaweza kutumika wakati wowote vikihitajika. Juu ya vipi viwekwe, vya aina na ukubwa gani, na pahala gani, taasisi husika inaweza kuwasiliana na Idara ya Usalama na Afya Kazini, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi au Idara ya Kukabiliana na Maafa.

Mpaka hivi sasa zipo baadhi ya Wizara na Taasisi za Umma ambazo tayari zimeweka vifaa hivi. Idara ya Usalama na Afya Kazini inaendelea kuwasiliana na Kamisheni ya Utumishi wa Umma juu ya utaratibu wa ukaguzi wa kina wa taasisi za umma kuhusu usalama na afya kazini, kama kinavyoelekeza kifungu cha 77 (2) cha Sheria ya Utumishi na Umma Nambari 2 ya mwaka 2011.

(b) Ni kweli ajali zinaweza kutokea popote na wakati wowote. Juhudi iliyoanza kuchukuliwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kupitia Idara ya Usalama na Afya Kazini ni kuteua Wawakilishi wa Usalama na Afya Kazini (*focal person)*, kwenye kila Wizara na Mashirika ya Serikali kwa Unguja na Pemba. Wawakilishi hawa wameteuliwa na Wizara zenyewe, kwa maelekezo ya Idara, kulingana na maelekezo ya vifungu vya 18 na 19 vya Sheria Namba 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini. Kazi yao ni kuwa waratibu wa masuala yote ya usalama na afya katika sehemu zao za kazi. Tayari wamepatiwa mafunzo ya awali juu ya kazi yao hiyo.

Kwa ujumla kila mfanyakazi anatakiwa afahamu juu ya kuwepo kwa vifaa vya kuzimia moto kwenye sehemu yake ya kazi na jinsi ya kuvitumia kwa usahihi.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mhe. Waziri je, iwapo itatokea ajali ya moto na ikawa labda taasisi haikuweka vifaa hivyo, ni adhabu gani ambayo itachukuliwa kwa taasisi hizo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu mama, kuna sheria tatu ambazo zinalazimisha masuala hayo ya kuweka vifaa ambavyo vinaweza vikakinga ajali au vikasaidia kupunguza ajali. Sheria hizo zote tatu zimeweka bayana kwamba kwa yeyote yule ambaye hatokidhi mahitaji ya kuweka vifaa vya usalama kazini basi hatua kali za kisheria zitachukuliwa pamoja na kupelekwa kwenye vyombo vya kisheria.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kuna baadhi ya taasisi vifaa hivyo vipi. Je, Mhe. Waziri ni taasisi zipi hizo ambazo vifaa hivyo vipo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, nitampatia kwa maandishi kwa sababu ni nyingi sana nikizitaha hapa sasa hivi tutafika mpaka Sala ya Ijumaa.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Wizara ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya mwaka 2011/202

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru *Allah* nichukue fursa hii vile vile kukushukuru wewe mwenye binafsi kunipa fursa hii ili kutoa tarifa ya utekelezaji kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Lakini vile vile nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa hekima n abusara kubwa ambayo wanaitumia katika usimamizi wa sekta hizi na kuona kwamba mambo yote yanakwenda kwa ufanisi, kwa kutoa nasaha, maelekezo, kukosoa na pale ambapo tumefanya vizuri vile vile kutoa sifa kama ilivyo.

Baada ya nasaha fupi hizo Mhe. Spika, sasa naomba nitoe tarifa hii ya utekeleza wa maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Katika taarifa hii Mhe. Spika, kuna maagizo ambayo yalitolewa lakini vile vile kuna na utekelezaji ambao ilitakiwa wizara itekeleze. Kwa kuanza agizo nambari moja ilikuwa kwamba, wizara itafute soko la kuuza *liquid nitrogen gas* ya ziada.

Katika hatua ya utekelezaji wizara imeanza kuwasiliana na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Zanzibar na inadhamiria kujadili suala hili kwa undani wakati Wizara ya Mifugo itapokutana na Wizara ya mifugo ya Tanzania Bara ili nayo itusaidie kutafuta soko kwa kule Tanzania Bara.

Lakini agizo na pili ilikuwa wizara itoe taaluma ya ufugaji kwa wazalishaji wa mazao ya baharini ili wazalishaji nao wapate faida. Katika hatua ya utekelezaji vikundi vya uzalishaji wa mazao ya baharini vimepatiwa taaluma ya uzalishaji bora na baadhi ya wazalishaji kutoka katika vikundi vya mazao ya baharini wamepatiwa fursa ya kwenda China ili kupata mafunzo zaidi ya uzalishaji kwa ufanisi.

Agizo la tatu ilikuwa wizara iwasiliane na uongozi wa Kiwanda cha Sukari Mahonda ili kisimwage sumu ambayo hatimaye itaathiri mazao ya samaki kama vile ilivyotokea Bumbwini Makoba. Katika hatua ya utekelezaji wizara inatoa taaluma hiyo kwa wazalishaji katika mabwawa ya samaki ili kuhakikisha kwamba wanatumia maji yaliyo safi ili wasipate hasara.

Aidha wizara imewasiliana na Idara ya Mazingira kuitaka kuelekeza wazalishaji wa viwanda wasimwage mabaki ya viwanda vyao bila ya mpango unaostahili.

Agizo la nne Mhe. Spika, ni kwamba wizara ifanye juhudi ya kuhakikisha inapatiwa kibali cha kuajiri vijana 20 zaidi kufanya kazi za kudumu katika kituo cha Kisakasaka. Katika hatua ya utekelezaji wizara imeshaomba nafasi za ajira kutoka Ofisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na tumepatiwa nafasi 40 tulizotakiwa kuzijaza.

Maombi ya nafasi hiyoy 40 yameshatumwa. Kwa nafasi 119 zilizobaki tumeahidiwa kupewa nafasi pale serikali itakapopata uwezo wa kifedha.

Agizo la tano wizara ilitakiwa itafute hati halali ya kumiliki eneo la Kisakasaka pamoja na jengo lililokuwemo ndani ya eneo hilo. Katika hatua ya utekelezaji wizara eneo la Kisakasaka limeshapimwa na ombi la kupatiwa hati miliki limeshawasilishwa katika wizara husika.

Wizara imewasiliana na Shirika la Uchapaji la Gazeti la Serikali kutaka kufahamu kwamba kama lipo toleo la kuitafishwa nyumba hiyo, lakini ilibidi kwamba archives kufuatilia suala hili na kuahidiwa kuleta taarifa lakini hadi leo hatujazipata.

Agizo la sita Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitakiwa iangalie mikataba na makubaliano ya uvuvi wa bahari kuu yaliyofikiwa kwa mtazamo wa mbele ili kuepusha Zanzibar na maafa yanayoweza kuepukika. Katika hatua yake ya utekelezaji wizara mikataba ya uvuvi wa bahari kuu ipo katika mamlaka ya bahari kuu, serikali imechunguza mikataba hiyo na kuona yapo mapungufu na sheria, na hivi sasa yanafanyiwa marekebisho.

Agizo la saba Mhe. Spika, wizara ilitakiwa iunde tume ya wataalamu wa kufanya tathmini ikiwa miradi inayoendeshwa na wananchi itakuwa na manufaa kabla ya mradi kuanza. Wizara katika hatua yake ya utekelezaji inacho kitengo maalum ambacho hufanya uchambuzi yakinifu ili kuhakikisha kwamba mradi wa kutekelezwa utakuwa na manufaa kwa wananchi ambacho kinaundwa na wataalamu wa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti wakishirikiana na wataalamu wa fani husika.

Agizo la nane kilichokuwa kiwanda cha kusindikia samaki ambacho amepewa mwekezaji ambaye hivi sasa hakifanya kazi kiwanda hicho kipewe mwekezaji atakayekitumia kwa manufaa ya wananchi. Katika hatua ya utekelezaji jengo lililokuwa la Kampuni ya *ZAFICO* lipo chini ya uangalizi ya Ofisi ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Wizara imewasilisha maombi ya soko, gati la wavuvi na kiwanda cha samaki Japan kwa kupitia *JICA* na tunasubiri majibu ya maombi hayo.

Agizo la tisa wizara kwa kushirikiana na Serikali Kuu kuwapatia au kutekeleza ombi la wana kamati wa soko la Matemwe na Pwanimchangani kupatiwa boti za uokozi. Hatua ya utekelezaji kwa hivi sasa eneo le hifadhi ya *MICA* inazo boti za doria ambazo pia zinatumika kwa matokeo ya dharura ya uokozi kwa wavuvi wa maeneo hayo.

Agizo la kumi wizara iwashirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuandaa mpango wa kuwalinda wazalishaji wadogo wadogo wa nchini kuwaepusha na wavamizi wa wafanyabiashara kutoka nje kupelekea kuanguka wazalendo kibiashara.

Wizara imefanya juhudi hizo ya kuwapatia uwezo wa ushindani wa kibiashara wazalishaji wazalendo, wizara imetayarisha mswada wa kuiomba serikali kupunguza kodi kwa mahitaji ya wazalishaji nchini bidhaa za uvuvi na mifugo. Mswada huo ukipita tunategemea gharama za uzalishaji nchini zitapungua na hivyo kuwafanya wazalishaji wetu kuwa na nguvu zaidi kwa kushindana na wazalishaji wa nchi za nje.

Agizo la kumi na moja wizara ishirikiane na makampuni ya mwani na kufanya upembuzi yakinifu na hatimaye kuweka bei ya mwani yenye maslahi kwa wananchi na kampuni. Katika hatua ya utekelezaji wizara tumekutana na makampuni ya mwani nayo yamekutana na wakulima wa mwani na hawakufikia muafaka wa kupandisha bei.

Vile vile wenye makampuni wanazungumzia juu ya kupunguza bei ya mwani kwa sasa kutokana na kuanguka kwa soko la dunia. Wizara inaendeleza mazungumzo hayo juu ya suala hili, wizara imeanda waraka unaohusu bei ya mwani kwa lengo la kupandisha bei ya wakulima kutokana na kushuka kwa soko la Ulaya.

Agizo la kumi na mbili wizara iwaongoze wakulima wa mwani katika wilaya ili kuwajengea ari na uwezo wa kuzalisha kwa kiwango kikubwa. Katika hatua ya utekelezaji wizara kupitia Idara ya Mazao Baharini imepitia katika Shehia za Unguja na Pemba kuwahamasisha wazalishaji wa mwani juu ya uzalishaji wa mwani wenye ubora, vile vile imeshahamasisha kujiunga na *SACCOS* kuhakikisha matumizi katika soko la ndani na kama kutengeneza sabuni na kadhalika.

Agizo la kumi na tatu wizara ifuwatafutia misaada ya vyombo vya kisasa kwa ajili ya uvuvi wa baharini yenye kina kirefu. Wizara itatoa taaluma na imeshatangaza zabuni kwa ununuzi wa vyombo vya uvuvi wa bahari kuu.

Agizo la kumi na nne kamati imeshauri wizara kutoa misaada kwa wavuvi inayostahiki na wasiruhusu kuingiliwa na wanasiasa na viongozi wa jamii. Wizara inashirikiana na viongozi na

wana jamii kuhakikisha kwamba misaada inayotolewa wanapewa wazalishaji wanaostahiki. Pia wizara imetengeneza miongozo kwa viongozi kushajihisha wananchi kuepukana na uvuvi haramu.

Agizo la kumi na tano wizara ijenge jengo lao wenyewe na isitegemee jengo liliopo Dunga kwa ajili ya huduma ya utabibu wa mifugo ambalo sio miliki yao. Hatua ya utekelezaji jengo la Dunga ni la Wizara ya Mifugo na Uvuvi na limeshakwisha kupimwa na kuombewa hati miliki na hivi sasa linaendelea kufanyiwa matengenezo.

Agizo la kumi na sita wizara inakabiliwa na tatizo la upungufu mkubwa wa watendaji hasa Idara ya Utibibu wa mifugo huko Pemba. Hatua ya utekelezaji wizara inawaendeleza wataalamu wake na inawashajihisha wanafunzi waliomaliza masomo kujiunga na Chuo cha Kilimo na Mifugo Kizimbani na imeshawaombea wahitimu hao kuajiriwa.

Agizo la kumi na saba wizara itoe taaluma ya kuchagua miradi yenye tija kwa mwanajamii. Hatua ya utekelezaji wizara inawashajihisha wananchi kuibua miradi yenye manufaa kwao na wizara inayafanyia uchambuzi yakinifu miradi hiyo.

Agizo la kumi na nane wizara iibue miradi ya muda mrefu. Hatua ya utekelezaji miradi ya muda mrefu imeandaliwa nayo ni chinjio, uvuvi wa kina kirefu na maendeleo ya miundombinu ya mifugo ambayo kila mmoja utachukua muda usiopungua miaka mitano.

Agizo la kumi na tisa wizara ijipange kuandaa vijana wa Kizanzibari kuwa na taaluma ya uzalishaji bora wa mazao ya baharini badala ya kutegemea wageni ambao hulipwa pesa nyingi. Hatua za utekelezaji wizara imewapatia mafunzo vijana 59 wa Kizanzibari katika elimu ya mazao ya kibaharini, pia kila mwaka wizara inategemea kutoa fedha na mafunzo zaidi.

Agizo la ishirini wafugaji wa kuku wa kienyeji juu ya kuwalinda mifugo yao dhidi ya maradhi. Hatua ya utekelezaji wizara imeshatoa taaluma kuhusu kuwakinga kuku dhidi ya maradhi imetolewa kupitai vyombo vya redio na magazeti. Aidha wafugaji wa kuku wameshajihishwa kuchanja kuku kuwakinga na maradhi kama vile mahepe magwa.

Vikundi vya wafugaji kuku vimepatiwa taaluma kupitia mradi wa ajira kwa vijana ambao unaendelezwa katika Wilaya ya Kaskazini ‘A’ ambapo vijana 40 wanashirikishwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. Hiyo ni taarifa fupi kuhusiana na maagizo ya Baraza lako tukufu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na pia sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye rehma karimu wa kutujaalia kuwepo tukiwa na afya njema.

Aidha sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha utekelezaji wa maagizo mbali mbali yaliyotolewa na Kamati ya Mifugo, Habari, Utalii na Uwezeshaji ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, pia sina budi na naomba uniruhusu kutoa shukurani za pekee kwa wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Habari, Utalii na Uwezeshaji iliyo chini ya mwenyekiti wake Mhe. Asha Bakari Makame mwakilishi wa vitu maalum na makamo wake Mhe. Ali Mzee Ali ambaye imekuwa ikitusaidia sana katika kutushauri, kutuelekeza na kutukosoa kwa lengo la kuleta ufanisi wa majukumu tuliyopewa na serikali.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa wote wa Baraza lako tukufu kwa kuweza kuchangia hotuba zetu na hoja ambazo tumekuwa tunawasilisha hapa Barazani na kutoa miongozo iliyokuwa na usahihi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya maagizo 33 yenye mchanganuo wa maagizo 44 yalitolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa kamati hiyo. Maagizo yote yamefanyiwa kazi na wizara yangu. Aidha michango na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wajumbe imekuwa ni chachu kupitia ofisi yangu katika kutekeleza mipango ya serikali na kwa wakati na kuleta ufanisi.

Utekelezaji wa Maagizo:

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kwa ruhusa yako niwasilishe kwa ufupi na kwa muhtasari utekelezaji wa maagizo yote 44 yaliyotolewa na Baraza lako tukufu. Aidha jadweli iliyoambatanishwa na taarifa hii inaelezea kwa kina utekelezaji wa kila agizo.

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ina wajibu wa kupigania kwa nguvu zote kuyaondoa matatizo yanayorudisha nyuma maendeleo nchini ambayo kamati imeyasikia moja kwa moja kutoka wana michezo wenyewe yakiwemo kwa kukosekana kwa ushirikiano baina ya taasisi na vile vyama vya michezo Tanzania Bara na hapa Zanzibar hususan kwenye michezo ya kimataifa.

Kukosekana kwa ruzuku wakati inapohitajika, uvamizi wa viwanja vya michezo na kuwakosesha vijana nafasi ya kufanya mazoezi. Aidha kukosekana kwa taratibu nzuri ya wizara kuendeleza sekta ya michezo kwa kutekeleza vyema raslimali watu ambapo mafunzo ya michezo hupewa watendaji wasiohusika na michezo, kutopatikana kwa motisha za kimichezo, kutopewa kipa vipa umbele na serikali kuu kwa kuondolewa utaratibu wa Mhe. Rais kuonana na wanamichezo kila baada ya muda maalum.

Pia kukosekana kwa jengo maalum la ofisi za wanamichezo kwa vyama vyote vilivyosajiliwa, kutokuwa na umoja na ubunifu baina ya viongozi wa vyama vya michezo na uongozi wa michezoni kububikwa na rushwa na hatimaye wale wasiokuwa na uwezo wa kuongoza kuchaguliwa kuwa ndio viongozi.

Mhe. Spika, hayo ndio matatizo yaliyobainika katika sekta ya michezo na kamati yako ya Baraza lako tukufu na tumeyatafutia dawa kwani tunaamini kuanguka kwa soka na michezo mbali mbali hapa Zanzibar kwa jumla na kurejea kama ilivyokuwa hapo zamani na kuendelea zaidi ni jambo linalowezekana na ndio maana tumedhamiria na kukusudia kuyashughulikia matatizo haya, kwani michezo katika ulimwengu wetu ni ajira.

Miongoni mwa hayo ambayo tumeanza kuyachukulia hatua ni kwanza kuteuwa Mrajis wa Vyama vya Michezo. Aidha hivi karibuni mimi mwenyewe nimeshakutana na viongozi wa Baraza la Michezo, Chama cha Mpira wa Miguu na vyama mbali mbali na wadau wa michezo ikiwa ni sehemu ya mikakati hiyo yenye lengo la kuandaa mbinu zitakazosaidia kupata ufumbuzi wa kudumu wa matatizo hayo na hatimaye kuendeleza michezo nchini.

Mhe. Spika, kuhusu uvamizi wa viwanja vya michezo wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo limekuwa likikutana na taasisi zinazohusika na utawala wa ardhi na tawala za mitaa na pia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuvilinda viwanja vya michezo.

Aidha katika kuendeleza raslimali watu Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo imekutana na kufanya mazungumzo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na hapa naomba nimshukuru sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kufanya jitihada kubwa kwenye suala hili na pia tumeunda kamati ya michezo ya wizara mbili itakayoshirikiana kuibua vipaji vya michezo na pia mazingatio ya kuanzisha tena mtaalama wa somo la michezo skulini.

Mhe. Spika, kuhusu motisha za kimichezo suala hili tumeanza kulifanyia kazi kwa kuwazadiwa wanamichezo wanaofanya vizuri katika mashindano mbali mbali. Hivi majuzi vijana waliofanya vizuri katika mashindano ya Judo ya Afrika ya Mashariki tulifanya mazungumzo nao na kuwazawadia.

Kuhudu pendekezo la Mhe. Rais wa Zanzibar kuonana na wana michezo kila baada ya muda limefanyiwa kazi ambapo mwaka huu Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya mazungumzo na wadau wa michezo kwa mara tau Ikulu mjini Zanzibar.

Katika vikao hivyo vya Mhe. Rais alishauriana na wadau hao wa michezo juu za kuendeleza na kufufua ari ya michezo.

Mhe. Spika, katika jengo la Kamisheni ya Michezo hapo Mwanakwerekwe ipo Ofisi ya Baraza la Michezo ambalo ndilo linaloratibu shughuli za vyama vya michezo 33 vilivyosajiliwa. Kuhusu agizo la kamati ya kuwa na jengo maalum litakalokusanya vyama vyote 33 vilivyosajiliwa. Agizo hilo tumelipokea lakini agizo linahitaji mashauriano na mashirikano zaidi na kamati na wadau wengine wa michezo ili kurahisisha utekelezaji wake.

Mhe. Spika, kuhusiana na uongozi wa vyama vya michezo agizo limetekelezwa kwa waziri mwenyewe kwa kukutana na viongozi wote wa vyama vya michezo na kuwataka wabadilishe ratiba zao na waitishe mikutano ya uchaguzi na kuchagua viongozi imara wa vyama vyao.

Mhe. Spika, kuhusu agizo la kamati linaloitaka wizara kuwa wazi katika kulizungumzia suala la uanachama wa Zanzibar katika Shirikisho la Soka Ulimwenguni. Wizara ipo wazi katika kuzungumzia suala la Zanzibar la kujinga na *FIFA* na mwenye mamlaka ya kulitolea tamko jambo hilo ni Chama cha Soka *ZFA* ambacho kwa mujibu wa taratibu ndicho chenye mamlaka na madaraka ya kuomba uanachama huo.

FIFA imeshatoa jibu rasmi kwamba kwa hadhi ya Zanzibar iliyonayo katika medali ya kimataifa hivi sasa, Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar hakiwezi kupata uanachama kwa *FIFA*.

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia Tume ya Utangazaji inaendelea kulifanyia kazi agizo la kamati la kuzitaka redio binafsi za *FM* kupeleka matangazo yao kisiwani Pemba kulingana na uwezo wa kifedha za redio hizo. Na kuhusiana na agizo la kamati kwa Wizara ya Habari, Utamzaduni, Utalii na Michezo kuwasimamia wamiliki wa redio binafsi nchini hususan wenye tabia ya kuwarekodi waheshimiwa na wananchi mbali mbali bila ya ridhaa zao, Tume inajiandaa kutoa mafunzo mbali mbali kwa watendaji wa redio hizo binafsi ili kuhakikisha maadili ya utangazaji yanazingatiwa ipasavyo.

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia Kamisheni ya Utalii na kwa kushirikiana na Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Uwanja wa Ndege imeunda kamati maalum ya wataalamu kuchunguza namna ya kupata takwimu sahihi za wageni wanaoingia nchini. Kuundwa kwa kamati hii kumetokana na uhalisia wa ushirikiano kati ya Kamisheni ya Utalii na Idara ya Uhamiaji pekee hakuwezi kufanikisha upatikanaji wa takwimu hizo.

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inaendelea kupokea ushauri na maelekezo kutoka kwa kamati yako na wajumbe wa Baraza lako tukufu, hatua hii itaiwezesha ofisi yangu na wizara yangu kwa jumla kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi na kusaidia changamoto zinazotukabili. Ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wataendelea kushirikiana na sisi katika jukumu letu la kuwahudumia wananchi.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali maelezo ya kina ya maagizo haya 44 ya utekelezaji wa maagizo yameorodheshwa katika kiambatanisho hiki isipokuwa kwenye majibu ya kifungu 1(b) ukurasa wa 1 baada ya neno “shilingi” yaingizwe maneno “Shilingi thalathini milioni kati ya shilingi mia moja na ishirini na nne milioni sawa na asilimia 24.

Mhe. Spika, baada ya masahihisho hayo sasa naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwa heshima sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2011/2012.

Lakini kabla ya hapo naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi ya leo kuamka kwa salama na afya na kuniwezesha kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Pili naomba kuishukuru sana kamati hiyo kwa mashirikiano makubwa waliyotupa kwa kipindi chote cha uongozi wao. Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ina jukumu la kusimamia na kuratibu programu zinazolenga katika kukuza ajira na kunyanyua kipato cha wananchi hususan wale wenye kipato cha chini ili waweze kumudu maisha yao ya kila, na hivyo kuwapunguzia makali ya umaskini masuala ya kukuza ajira ni miongoni mwa mambo ambayo yamepewa kipa umbele katika mpango mkuu wa kitaifa kwenye dira ya 2020 na mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Zanzibar.

Mhe. Spika, dira ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ni kuona jamii ya Zanzibar yenye fursa za kutosha za ajira, kipato endelevu. Dhamira ya wizara ni kuwezesha upatikanaji ajira wenye heshima na utekelezaji wa programu zenye uwezeshaji ili kuhakikisha maisha bora kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi imefanya kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kupitia idara zilizo chini ya wizara hii. Baada ya kamati kufanya kazi ilishauri na kufanya maagizo kwa ajili ya kufanyiwa kazi na wizara.

Mhe. Spika, taarifa hii inazungumzia utekelezaji wa maagizo mbali mbali yaliyotolewa na wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza lako tukufu kwa wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2011/2012.

Aidha maelezo ya utekelezaji yanayotolewa katika taarifa hii yanahusu kipindi cha mwaka wa bajeti hadi mwezi wa Machi 2013.

Mhe. Spika, ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Baraza lako tukufu la Wawakilishi la mwaka 2011/2012 inaonesha ya kuwa kuna jumla ya maagizo 15 yanayohusu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kutekeleza maagizo hayo yanaoneshwa katika jadweli iliyoambatanishwa.
Kwa heshima sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa maagizo hayo yote.

Agizo la kwanza Mhe. Spika, wizara iwapatia mafunzo maalum wajasiriamali wa Zanzibar juu ya umalizaji wa kazi zao ili ziweze kuwa na mvuto na kupata soko la ndani na nje ya Zanzibar. Utekelezaji Mhe. Spika, imekuwa ikiendelea na mafunzo ya uhamasishaji wa bidhaa za wajasiriamali, ufungashaji na soko ili kusaidia kupata soko.

Mafunzo hayo yamefanyika kwa wajasiriamali 80 Unguja na Pemba na kweli yameanza kuonesha mafanikio. Aidha ushauri umekuwa ukitolewa wakati wa kutembelea kazi za wajasiriamali katika maeneo yao ya uzalishaji.

Agizo la pili Mhe. Spika, ilikuwa ili kufanya mfuko wa JK na AK ni tegemeo la wananchi wanyonge na bila ya kupunguza kiwango cha utendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar, kamati inashauri mfuko huu kurejesha kwenye wizara inayohusika na kusimamia mambo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na ushirika ili usimamiwe vizuri zaidi.

Tayari utekelezaji wake mazungumzo yameshafanyika na suala hili Mhe. Spika, limeshajadiliwa na pande zinazohusika, tayari benki kupitia bodi yao wameridhia na sasa tunasubiri kukamilisha makubaliano kati ya wizara inayohusika na masuala ya fedha na Benki ya Watu wa Zanzibar.

Agizo la tatu kamati imeitaka wizara kuvipa kipa umbele maalum vikundi vya watu wenye ulemavu, kuwapatia mafunzo na mikopo ili waweze kujikwamua kwenye jangwa la utegemezi.

Mhe. Spika, hatua tumeanza kuzichukua na za kutoa mafunzo. Watu wawili wanaume wenye ulemavu; mmoja mwenye ulemavu wa mkono kutoka Wilaya ya Mjini yeye bado hajapatiwa

mkopo na mwengine kutoka Mkoa wa Kusini Unguja mwenye ulemavu wa mguu tayari amepatiwa mafunzo na mkopo katika mfuko wa kujitegemea.

Aidha mafunzo ya mikopo kwa wenzetu hawa yanategemea sana kutokana na maombi yao.

Mhe. Spika, vikundi 12 vya watu wenye ulemavu na hapa naomba kusaidia lile suala ambalo asubuhi lilijitokeza kuhusu suala la kuwasaidia walemavu. Tayari vikundi 12 vya ulemavu vimepata mkopo kupitia mfuko wa Zakka. Kati ya hivyo 8 vinatoka Unguja na 4 vinatoka Pemba. Jumla ya shilingi milioni kumi na nane na laki tano zimetolewa kwa walemavu hao.

Mhe. Spika, agizo la nne katika jitihada za kupunguza unyanyasaji wa waajiriwa hasa katika sekta binafsi, kamati imeshauri wizara kuwapa taarifa ya moja kwa moja wafanyakazi kupitia wilaya zao kila wanapofanya marekebisho ya mshahara. Hatua ya kutoa taarifa kwa wafanyakazi juu ya marekebisho ya mishahara kwenye sekta binafis zimefanyika.

Mhe. Spika, agizo la tano wizara ifanye kila njia kumuendeleza mjasiriamali Bwana Said pamoja na wale wote waliojitokeza katika ubunifu kama wake wa kuvumbua vitu vipya ambavyo ni chachu ya ujenzi wa njia mpya za uzalishaji na ukuaji wa sekta ya viwanda hapa nchini. Ni wajibu wetu wizara kupanga mipango ya muda mrefu kwa kushirikiana na serikali kuu ili kuwa na mwendelezo mzuri wa vijana wetu wazalendo wenye mwelekeo kama huu.

Aidha ni vyema wizara ikanunua gari hiyo ya Bwana Said na kuiweka makumbusho. Halikadhalika wizara isimamie suala zima la usajili la Karakana ya sugu ili nayo itambulikane kitaifa.

Mhe. Spika, hapa huyu ni mvumbuzi ambaye ameunda gari maalum. Bahati nzuri nilipata bahati ya kuipanda gari hiyo na hii gari inaitwa sugu 11, maana yaka alianza na moja akaiita sugu 1 na hii ya pili ikaiita sugu 11 na tayari kwa upande wa wizara utekelezaji wa suala hilo la agizo la kamati tumechukua hatua za kuwasiliana na Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania ili kumuendeleza mjasiriamali huyo.

Mhe. Spika, maelezo nasema tumemuwezesha kushiriki maonesho ya wiki ya Sayansi na Teknolojia ambapo amepatiwa zawadi akiwa ni miongoni wa wavumbuzi wa kusajiliwa ili kutambuliwa uvumbuzi wake. Tayari mimi binafsi naomba nikiwa ni Waziri wa masuala haya ya uwezeshaji nimempa zawadi ya shilingi milioni moja mvumbuzi huyu ili iwe ni motisha kwa kuendelea kufanya shughuli zake.

Agizo la sita Mhe. Spika, katika suala zima la utoaji na ufuatiliaji wa mikopo nchini, ni vyema wizara ikawa na kitengo imara cha kuelimisha watendaji wa serikali na wananchi wengine ili waelewe jinsi ya kupata mikopo na njia sahihi za matumizi ya mikopo hiyo kwa nia ya kujikwamua kutokana na janga la umaskini wa kipato.

Utekelezaji wake Mhe. Spika, wizara inatoa mafunzo kwa wakopaji kabla ya kupatiwa mikopo hiyo.

Agizo la saba wafanyakazi wengi wa kada ya mahoteli hukosa haki zao za msingi kutoka kwa waajiri wao hasa mara baada ya kufukuzwa kazi, zoezi ambalo huwakumba mara kwa mara kutoka hoteli moja hadi nyengine. Tunatoa wito kwa wizara kuwachukulia hatua waajiri wote wenye tabia ya unyanyasaji kwa waajiriwa.

Hatua za utekelezaji, maelekezo ya kamati yamefanyiwa kazi na wafanyakazi wanaopatwa na matatizo ikiwemo lile la kufukuzwa kazi wameelekezwa kutoa taarifa wizarani ili hatua zichukuliwe. Mhe. Spika, kuna kitengo maalum cha utatuzi wa migogoro. Kitengo hiki kutokana na matatizo kama hayo ambayo yameelezwa na kamati imeshachukua hatua na tayari malalamiko 68 yaliwasilishwa na kuchukuliwa hatua mbali mbali za kutatua.

Agizo la nane Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Serikali Kuu haina budi kujenga ofisi maalum kwa ajili ya Idara ya Mikopo ili kuokoa fedha nyingi zinazotumika kwa kukodi majengo ambayo zaidi shilingi milioni tatu nukta sita zinatumika kwa kulipia kodi kila mwaka kwa ofisi za Unguja na Pemba.

Kufanya hivyo kutawasaidia kupata fedha zaidi kwa ajili ya matumizi mengine ya uendeshaji, kama vile usafiri na kulipa stahiki za wafanyakazi wa idara hii ili kuwajengea ari zaidi ya kuwajibika.
Mhe. Spika, tayari suala hili tumeshalifikisha serikalini na tayari tumeshapata agizo kwamba katika bajeti ijayo tutenge fedha maalum kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya ofisi.

Mhe. Spika, agizo la tisa kutokana na ukweli kwamba wadaiwa walio wengi hawalipi madeni yao, wakati umefika kwa wizara kuandaa sheria ya kuwatia hatiani na kuwaadhibu wale wote watakaobainika kutolipa mikopo hiyo au kuichelewesha kwa makusudi.

Mhe. Spika, utekelezaji wake tunafuatilia kwa karibu zaidi kwa kushirikikana na kamati za wilaya pamoja na Masheha katika kuwafuata wadaiwa sugu, ili warejeshe mikopo walioichukua.

Mhe. Spika, maelezo ya ziada sera ya mikopo karibuni itamalizika ambapo inaandaliwa na Wizara ya Fedha na washirika wengine wa mikopo. Aidha wanatarajia kuandaa miongozo mipya itakayowasimamia uendeshaji wa shughuli za mikopo kwa kuwa taratibu ziliopo sasa hazitoi nafasi kwa kumshtaki mtu.

Mhe. Spika, agizo la tisa kutokana na ukweli kwamba wadaiwa walio wengi hawalipi madeni yao, wakati umefika kwa wizara kuandaa sheria ya kuwatia hatiani na kuwaadhibu wale wote watakaobainika kutolipa mikopo hiyo au kuichelewesha kwa makusudi.

Mhe. Spika, utekelezaji wake tunafuatilia kwa karibu zaidi kwa kushirikikana na kamati za wilaya pamoja na Masheha katika kuwafuata wadaiwa sugu ili warejeshe mikopo walioichukua.
Mhe. Spika, maelezo ya ziada sera ya mikopo karibuni itamalizika ambapo inaandaliwa na Wizara ya Fedha na washirika wengine wa mikopo. Aidha wanatarajia kuandaa miongozo mipya itakayowasimamia uendeshaji wa shughuli za mikopo kwa kuwa taratibu ziliopo sasa hazitoi nafasi kwa kumshtaki mkopaji.

Mhe. Spika, agizo la kumi kamati inashauri idara hii ya mikopo iendeshwe kwa utaratibu wa kuwa na bodi ambayo itafanya maamuzi yake, kwa utendaji bora zaidi.

Utekelezaji wake, Mhe. Spika, tumeanza na kamati maalum ya kuidhinisha mikopo, ambayo inajumuisha idara nyengine za Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Lakini maelezo ya ziada kuhusu uundwaji wa bodi. Suala hili linasubiri kukamilika kwa sera ya mikopo, sera ya uendeshaji wananchi kiuchumi na ushirika na miongozo ya utoaji mikopo inayoandaliwa.

Mhe. Spika, agizo la kumi na moja katika kusimamia vyema fedha za umma, ni jukumu la wizara kuanzisha *database* ya wakopaji ambayo itawaunganisha wakopaji wote kupitia taasisi mbali mbali za watoaji mikopo ya serikali na binafsi, ili kuwaepusha na mikopo mingi kwa wakati mmoja ambayo hatimaye huwashinda kulipa.

Utekelezaji wake, Mhe. Spika, utekelezaji umeanza kwa kuudwa kwa mtandao wa wakopeshaji wadogo wadogo Zanzibar. Maelezo ya ziada, kamati maalum imeandaliwa ya watu 10 kutoka taasisi mbali mbali za wakopeshaji. Kwa mara ya mwisho kamati ilikutana tarehe 09/04/2013.

Agizo la kumi na mbili kutokana na idadi kubwa ya mifuko ya mikopo kwa wananchi, kamati inakubaliana na wazo la kuunganisha mifuko yote yenye lengo la kuwainua wananchi, kwa kuwa na mfuko mmoja tu ili kupata urahisi wa kufuatilia hasa tukitilia maanani kwamba tuna upungufu wa wafanyakazi wa kufuatilia mikopo hiyo.

Utekelezaji wake, Mhe. Spika, agizo hili tunalifanyia kazi kwa nguvu zetu zote. Tayari Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alitangaza rasmi katika ukumbi wa Salama Hall, alipozindua mfuko wa ZAKA na ameahidi kuichanganya mifuko yote na kuwa mfuko mmoja wa Uwezeshaji.

Mhe. Spika, agizo la kumi na tatu kamati inatoa agizo kwa wizara kufuatilia hadi kujua taarifa sahihi kuhusu gari iliyotolewa na SMZ kwa ajili ya idara ya mikopo, na ambayo hadi sasa inatumiwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.
Mhe. Spika, wizara imelifuatilia suala hili, barua iliopo ni ya kukabidhiwa gari Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kutoka Baraza la Mapinduzi na hakuna barua rasmi iliyoandikwa au iliyoandikiwa au iliyotuagiza kukabidhiwa gari hiyo idara ya mikopo.

Agizo la kumi na nne Wizara ifanye jitihada za makusudi za kuongeza idadi ya wafanyakazi katika Idara ya Mikopo, ili kuongeza ufanisi katika ufuatiliaji wa mikopo hiyo. Mhe. Spika, wizara tayari imeshachukua hatau hiyo na maelezo ya nyongeza, inaeleza hapo pembeni kwamba tayari imeshaajiri wafanyakazi 6, watatu Unguja na watatu Pemba yamewasilishwa mapendekezo hayo.

Mhe. Spika, agizo la kumi na tano kamati kwa kushirikiana na wizara, inaomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iwajibike ipasavyo kwa kukusanya mapendekezo yote, yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi kupitia kwenye hotuba zao za Baraza kuyapeleka

serikalini, ili yafanyiwe kazi kwa nia ya kuimarisha nchi yetu na watu wake. Suala hili nimelenga Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Tayari hatua tumezichukua kwa kuwasiliana nayo.

Mwisho kwa niaba ya viongozi na watendaji wa wizara yangu. Mhe. Spika, natoa shukrani zangu kwa kamati, kutokana na ushauri, maelekezo na muongozo wanaotupatia vinavyotuwezesha kuimarisha utendaji wa kazi zetu na kuleta ufanisi katika kufanikisha malengo tuliyokusudia. Wizara inafarijika sana na utendaji wa Kamati hii.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Asaa Othman Hamad: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema nyingi alizotuneemesha, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu ripoti ya kamati hiyo.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo hii, kwa madhumuni ya kujadili mambo mbali mbali yenye maslahi mema na ustawi mzuri kwa nchi yetu na watu wake.

Mhe. Spika, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 106(i) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi - Zanzibar, toleo la mwaka 2012. Majukumu na kazi za Kamati hii yameainishwa katika kanuni ya 115 ya Kanuni za kudumu za Baraza la Wawakilishi ambapo, pamoja na mambo mengine, Kamati ina majukumu ya msingi yafuatayo:

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.
c) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika.
d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.
e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.
f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.
g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.
h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Mhe. Spika, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imepewa majukumu ya kusimamia Wizara tatu zifuatazo:

- Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
- Wizara ya Mifugo na Uvuvi
- Wizara ya Kazi, Uwezeshaji wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Spika, kamati yetu ina Wajumbe wanane na makatibu wawili na imekuwa ikifanya kazi kwa mashirikiano makubwa baina ya Wajumbe pamoja na makatibu wake. Nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari pamoja na makatibu wake kwa kazi nzuri waliyoifanya na kupelekea kumaliza misimu mitatu ya kazi za Kamati kwa umahiri na ufanisi mkubwa. Naomba niwatambulishe kwa majina Wajumbe na makatibu hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Asha Bakari Makame - Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Mzee Ali - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Asaa Othman Hamad - Mjumbe
4. Mhe. Salim Abdalla Hamad - Mjumbe
5. Mhe. Abdi Mossi Kombo - Mjumbe
6. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
7. Mhe. Kazija Khamis Kona - Mjumbe
8. Mhe Mansoor Yussuf Himidi - Mjumbe
9. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
10. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita baina ya Unguja, Pemba na Dar es Salam. Kamati ilianza kutekeleza shughuli zake kwa Unguja, kuanzia tarehe 12/09/2012 hadi tarehe14/09/2012.

Aidha, Kamati iliweza kwenda Dar es Salaam na kufanya shughuli zake huko kuanzia tarehe 17/9/2012 hadi tarehe 21/9/2012. Katika mzunguko wa pili Kamati ilifanya kazi zake kisiwani Pemba kuanzia tarehe 10/12/2012 hadi tarehe 21/12/2012. Kamati katika awamu ya tatu ilifanya kazi zake kwa upande wa Unguja kuanzia tarehe 4/3/2012 hadi tarehe 15/3/2012

Mhe Spika, Kamati yetu kimsingi imeridhika na utendaji wa wizara zote tatu ilizozitembelea. Kamati inawapongeza kwa dhati watendaji wa Wizara zote kwa juhudi kubwa wanayoichukua kutekeleza majukumu yao, licha ya mazingira magumu wanayokabiliana nayo.

Mhe. Spika, naomba sasa niwasilishe mbele ya Baraza lako tukufu, muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 kwa kuchambua Wizara moja moja kama ifuatavyo:-,

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO:

Mhe. Spika, natumai sote tunaelewa na kufahamu kwa kina umuhimu uliopo kwa wizara hii na vitengo vyake. Wizara hii inabeba majukumu mazito ya Kitaifa yakiwemo ya Utalii ambao ndio mhimili mkuu wa uchumi wetu na Habari ambayo ni nyenzo muhimu kwa mawasiliano katika jamii.

CHUO CHA MAENDELEO YA UTALII:

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii ni sekta inayoongoza katika kuingiza fedha nyingi za kigeni hapa nchini. Kwa kuuona umuhimu huo, Kamati katika kazi zake mwezi wa Septemba, 2012 ilipanga kutembelea Bodi ya Utalii pamoja na Chuo cha Utalii, Dar es Salaam ili kuweza kubadilishana ujuzi na uzoefu na wenzetu kwa lengo la kuweza kujadili na kuishauri Serikali juu ya mbinu na mikakati bora zaidi ya kuimarisha Sekta hii muhimu.

Hata hivyo kutokana na sababu zisizoweza kuepukika, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea taasisi moja tu ambayo ni Chuo cha Taifa cha Utalii ambacho ni kipya na chenye miundombinu ya kisasa kabisa ya kufundishia mafunzo mbali mbali ya utalii. Katika ziara hiyo, Kamati ilifuatana na baadhi ya watendaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar. Kama hiyo haitoshi, katika mzunguko wa tatu wa kazi zake za kawaida, tarehe 6 Machi, 2013, Kamati ilitembelea Chuo cha Mandeleo ya Utalii, Zanzibar ili kuona utekelezaji wa shughuli zake pamoja na kuona namna chuo hicho kilivyojipanga katika kuyafanyia kazi mafunzo yaliyopatikana katika ziara ya Kamati huko Dar es Salaam ambayo Mkuu wa Chuo hicho alishiriki kikamilifu.

Mhe. Spika, Kamati imeridhishwa na imefurahishwa sana na maendeleo makubwa yaliyofikiwa katika Chuo hicho ikiwa ni pamoja na mafanikio mbali mbali ya kitaaluma. Chuo kimefanikiwa kupata mradi wa ujenzi wa jengo la ghorofa moja lenye ofisi, madarasa na maktaba linalogharamiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa gharama ya Tsh milioni 800 ambalo hadi mwezi wa Machi 2013 lilikuwa katika hatua ya kuezekwa.

Aidha, kwa kupitia Mradi wa *ADB* litajengwa jengo jengine la ghorofa nne(4) na kituo cha ujasiriamali litalogharimu Dola za Marekani 1,862,680 litalokuwa na miundombinu ya kisasa ya kusomeshea masuala ya Utalii. Ni jambo la furaha na faraja kuona kuwa miudombinu ya jengo hilo la ghorofa nne italingana na ile iliyopo katika Chuo cha Taifa cha Utalii, Dar es Salaam ambayo Mkuu wa Chuo hicho aliiona na kuweza kujifunza, kuiga na hatimae kuingiza ramani zake katika mradi huo mpya wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii, Zanzibar.

Kwa mnasaba huu basi, kamati inapenda kutoa pongezi nyingi na za dhati kwa Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kwa jitihada, ujasiri na umahiri wake mkubwa wa kukiletea mabadiliko na mafanikio makubwa Chuo hicho tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo. Kamati inatoa wito kwa wanawake wanaoshika nyadhifa mbali mbali za uongozi hapa nchini kuiga mfano bora wa mwanamama mwenzao huyo shupavu, mchapakazi, mwenye moyo wa kizalendo na mpenda maendeleo.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii, bado Chuo hicho kinaonekana kuendelea kukabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo hatari ya

mmong'onyoko wa ardhi katika ufukwe ulio karibu kabisa na Chuo hicho na upungufu mkubwa wa usafiri ulioko katika Chuo hicho. Kutokana na changamoto hizo, Kamati imeishauri Wizara kutoa msukumo maalum katika kulitatua tatizo la mmong'onyoko wa ardhi chuoni hapo kwa kutafuta wataalamu na wafadhili wa kusaidia kulitatua tatizo hilo sugu.

Aidha, Kamati imeishauri Wizara ikae na Uongozi wa Chuo hicho ili kuona namna ya kuweza kukipatia Chuo hicho gari nyengine ili kiweze kuendesha shughuli zake vizuri. Ni aibu na inasikitisha sana kuona kuwa Chuo hicho kina gari moja tu ambayo imeshachakaa na huharibika mara kwa mara kutokana na matumizi makubwa.

HOTELI ZA KITALII:

Mhe. Spika, ni jambo la faraja sana kuona kuwa baadhi ya wamiliki wa hoteli za kitalii kuweza kujishirikisha moja kwa moja kwenye masuala yanayohusu jamii na Taifa kwa ujumla. Hoteli ya kitalii ya Melia iliyopo Kiwengwa mwaka huu iliandaa maadhimisho ya siku ya Wanawake duniani yaliyofanyika hotelini hapo tarehe 8 Machi, 2013 ambapo Mwenyekiti wa Kamati hii alikuwa Mgeni Rasmi.

Napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa Uongozi wa hoteli hii kwa kuthamini juhudi za Mwenyekiti na Kamati kwa ujumla katika kupinga unyanyasaji wa wafanyakazi katika sehemu za kazi hasa katika hoteli za kitalii. Hivyo, Kamati inatoa wito kwa viongozi wa hoteli nyengine za kitalii kuiga mfano huu mzuri uliooneshwa na hoteli ya Melia ili kuitekeleza kwa vitendo dhana ya Utalii kwa wote.

HOTELI YA BWAWANI:

Mhe. Spika, wakati kamati ilipotembelea Hoteli ya Bwawani, ilishuhudia uvamizi wa eneo la hoteli hiyo kwa ujenzi wa majengo ya biashara yaliyofanywa na mtu binafsi. Kamati imeshangazwa sana na kitendo cha kutolewa kibali cha ujenzi mnamo mwezi wa Septemba, 2012 wakati ambapo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikwishatoa agizo la kutojengwa kwa eneo hilo mnamo mwezi wa Febuari, 2012. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaiomba Wizara na taasisi nyengine za Serikali kuyasimamia ipasavyo maagizo ya viongozi wakuu wa Kitai

SHIRIKA LA UTANGAZAJI (*ZBC*):

Mhe. Spika, kama ilivyo katika nchi yoyote duniani, sekta ya utangazaji ina wajibu mkubwa katika kuhamasisha jamii katika harakati za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha**,** katika kikao chake mwezi wa Januari, mwaka huu wa 2013, Baraza lako tukufu lilipitisha sheria ya Kuanzisha Shirika la Utangazaji, Zanzibar ikiwa na lengo la kuliongezea Shirika hilo uwezo wa kisheria, kiutendaji na kiutawala ili kulifanya Shirika hilo kubadilika na kutekeleza wajibu wake kwa wananchi kwa ufanisi zaidi likizingatia kasi ya maendeleo ya teknolojia katika sekta hiyo.

Mhe. Spika, mnamo tareha 17 Septemba 2012, Kamati ilitembelea kituo cha utangazaji cha Shirika hilo huko Dar es Salaam na kuzungumza na watendaji wa kituo hicho pamoja na uongozi

wa wizara. Katika mazungumzo hayo Kamati iliarifiwa kuwepo kwa changamoto kadhaa ikiwemo uhaba wa nafasi katika kituo hicho kwa ajili ya watendaji.

Aidha, maslahi ya watendaji hao ni madogo mno ukilinganisha na hali halisi ya maisha katika jiji la Dar es Salaam. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kushirikiana kikamilifu na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuona namna ya kuwaongeza ari ya kiutendaji wafanyakazi hao kwa kuwapandishia maslahi yao ili yalingane na hali ya maisha ya Jiji la Dar es Salaam. Vile vile Wizara inapaswa kuinua uwezo wa kituo hiki ili kiweze kutoa vipindi bora vitakavyowavutia wananchi na hivyo kumudu ushindani wa vyombo mbali mbali vya habari huko Tanzania Bara.

Mhe. Spika, kamati ilipata fursa pia ya kulitembelea Shirika hilo hapa Zanzibar tarehe 7 Machi, 2013 ili kuona utekelezaji wa shughuli zake pamoja na kuona maandalizi ya kulibadilisha Shirika hilo kiutendaji pamoja na safari yake ya kuelekea digitali. Kamati imebaini changamoto kadhaa zinazowakabili watendaji wa Shirika hilo ikiwemo uhaba wa vifaa vya kisasa na vya kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya Shirika hilo kwa sasa. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaona ipo haja kubwa kwa Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuliimarisha na kuliendesha Shirika hilo ili kupata ufanisi zaidi.

MICHEZO:

Mhe. Spika, katika sekta ya michezo, kamati inaipongeza Wizara pamoja na timu ya Taifa ya Zanzibar ya mchezo wa Judo kwa mafanikio makubwa yanayoonekana katika timu hiyo na hasa kwa kushika nafasi ya pili katika mashindano ya mchezo wa Judo kwa nchi za Afrika ya Mashariki yaliyofanyika hapa Zanzibar hivi karibuni. Ni wazi kuwa matokeo hayo yameipa sifa kubwa nchi yetu na kuonekana kuwa vijana wetu wanaumudu mchezo huo vilivyo.

Mhe. Spika, Pamoja na mafanikio hayo bado sekta ya Michezo inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo mikakati imara ya kuibua vipaji vilivyopo pamoja na matatizo mbali mbali inayovikumba vyama vya michezo ikiwemo migogoro ndani ya vyama na ufinyu wa bajeti katika shughuli za michezo. Katika ziara yake ya Tanzania Bara ya tarehe 18 Septemba 2012, Kamati ilipata nafasi ya kuonana na kubadilishana mawazo na Katibu wa Baraza la Taifa la Michezo Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na viongozi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhusu vyama vya michezo ambapo changamoto kadhaa za vyama vya michezo zilijadiliwa zikiwemo hizo nilizozitaja. Kutokana na hali hiyo, Kamati inasisitiza haja ya Katibu wa Baraza la Michezo Zanzibar na Tanzania Bara kuwa wabunifu katika kazi zao na kuzishauri Serikali njia bora za kushirikiana katika kunyanyua michezo nchini.

Mhe. Spika, katika suala zima la kuibua vipaji vya michezo hapa nchini, Kamati katika kazi zake za mwezi wa Machi 2013 ilipata nafasi ya kukitembelea kituo cha Akademia ya Michezo kilichopo Dole ambacho kimejengwa kwa ajili ya kulea vipaji vya watoto katika michezo ikiwemo ya judo, mpira wa miguu, riadha, mpira wa kikapu na mengineyo. Kamati imegundua kuwa watendaji wa kituo hicho hawapati stahiki zozote kutokana na kazi ya kulea vipaji vya watoto hao.

Aidha, Kamati imesikitishwa sana kuona kuwa kituo hicho kinakosa huduma muhimu ya maji, vyoo na umeme jambo ambalo ni hatari kwa afya za watoto wanaokwenda kituoni hapo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaitaka Wizara iwe karibu zaidi katika kukiendeleza kituo hicho ikiwa ni pamoja na kukipatia kituo hicho maji, umeme, vyoo, uzio, barabara nzuri ya kukifikia na kukitafutia hati miliki.

MAGOFU:

Mhe Spika, kila nchi hapa duniani ina historia yake na mipango yake katika kuienzi na kuitunza historia hiyo. Zanzibar kama nchi moja wapo, nayo ina historia yake na vielelezo vyake vinavyoijenga historia hiyo. Magofu ni moja kati ya vielelezo muhimu vya historia ya nchi yetu. Hata hivyo magofu mengi hapa nchini yanaonekana kukosa kutunzwa vizuri na hivyo haiba ya magofu hayo imeondoka.

Aidha, taarifa sahihi zinazohusu maeneo mbali mbali ya kihistoria zimekosa kutunzwa vizuri jambo ambalo linaweza kupelekea kupotoshwa kwa taarifa sahihi za maeneo ya kihistoria. Kamati ilipotembelea magofu ya Mkama Ndume kisiwani Pemba katika mwezi wa Disemba, 2012 ilibaini kutoweka kwa sehemu mbali mbali muhimu za ngome hiyo zikiwemo ngazi za chini kwa chini na nguzo za msikiti wa eneo hilo.Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiagiza Wizara kuzijenga tena nguzo hizo za msikiti wa eneo la Mkama Ndume na kufanya jitihada za kuyafukua maeneo yaliyojifukia ya Ngome hiyo.

Aidha, wizara itoe kipaumbele maalum katika kuyaenzi, kuyatunza na kuyadumisha magofu yaliyopo hapa nchini pamoja na kuhakikisha kuwa maelezo sahihi ya maeneo ya kihistoria yanaandikwa na kutunzwa vizuri ili kuepusha upotoshwaji wa taarifa za kihistoria katika maeneo hayo.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

Mhe. Spika, Sekta ya mifugo na ile ya uvuvi ni tegemeo la idadi kubwa ya watu, hususan wale wanaoishi katika ukanda wa pwani, vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa msingi huo basi, Serikali imeamua kuunda Wizara maalumu itakayoshughulikia maendeleo ya mifugo na uvuvi kwa maslahi ya Taifa hili.

MIFUGO:

Mhe. Spika, ni jukumu la Wizara ya mifugo kuratibu na kupanga maendeleo ya mifugo kwa kutoa taaluma juu ya mbinu bora za uzalishaji kwa lengo la kufanya ufugaji uwe wa kibiashara na wenye tija zaidi. Kuhakikisha kuwa mifugo yote nchini iko salama kutokana na maradhi mbali mbali ya mifugo na kuhakikisha mifugo haienezi maradhi kwa binadamu.

Mhe. Spika, pamoja na jukumu hilo muhimu, bado wafugaji wengi hapa nchini wanakabiliwa na changamoto kadhaa zinazokwamisha shughuli zao. Miongoni mwa changamoto hizo ni kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya mbinu bora za ufugaji, upatikanaji wa chanjo za uhakika za

mifugo (hususan za ng'ombe) pamoja na elimu inyohusiana na umuhimu wa chanjo kwa mifugo yao.

Kutokana na hali hiyo, Kamati inaona ipo haja kwa Wizara kufanya juhudi maalum za kuimarisha utoaji wa elimu kwa wafugaji juu ya mbinu za kisasa za ufugaji pamoja na kuwaandalia ziara za kimafunzo wafugaji wetu ili kuwaongezea uzoefu na maarifa ya ufugaji unaokwenda na wakati na wenye tija zaidi. Aidha, Wizara haina budi kusaidia katika kupata utaratibu utaohakikisha upatikanaji wa chanjo za mifugo zinazokidhi viwango vinavyokubalika kitaalamu ili kuwaepusha wafugaji kutumia chanjo zisizofaa ambazo huleta madhara kwa mifugo yao.

UVUVI:

Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na uvuvi ina jukumu la kuwahudumia wavuvi, wakulima wa mwani pamoja na wale wanaojishughulisha na ufugaji wa samaki na mazao ya baharini kwa lengo la kuinua hali zao za maisha na Taifa kwa ujumla. Aidha, sekta ya Uvuvi ina jukumu la kuhakikisha kuwa rasilimali za baharini zinahifadhiwa kwa kuzingatia matumizi mazuri ya rasilimali hizo. Sekta hii pia ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa sera na sheria zinazohusiana na maendeleo ya uvuvi.

Mhe. Spika, taarifa ya utekelezaji wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imeeleza kuwa utekelezaji wa sheria na taratibu za uvuvi ni changamoto kubwa inayoikabili Idara hiyo kwa hivi sasa. Kamati imebaini kuwa mwamko mdogo baina ya wananchi katika utekelezaji wa Sheria za uvuvi unaochangiwa pia na hali duni za maisha walizonazo wavuvi wetu unazidi kuwachochea wavuvi hao kuendelea kutumia njia za uvuvi ambazo hazikubaliki kisheria.

Hivyo, ni jukumu la Wizara kuendelea kuwaelimisha wananchi juu ya njia sahihi za uvuvi ambazo zinakwenda sambamba na sheria ya uvuvi nchini. Aidha, Kamati inatoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kuhimizana na kushajiisha jamii tunayoiongoza juu ya umuhimu wa kufuata taratibu zinazokubalika katika kutekeleza kikamilifu sheria ya uvuvi, ili kujipatia maendeleo endelevu ya sekta ya uvuvi.

ZAO LA MWANI:

Mhe. Spika, wakati kamati ikijadili taarifa ya utekelezaji wa wizara hii kwa upande wa Pemba mnamo mwezi wa Disemba 2012, iliarifiwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea (Korea ya Kusini) kupitia Shirika lake la Maendeleo (*KOICA*) imeonesha nia kubwa ya kutaka kujenga kiwanda cha kusagia mwani katika eneo la Tumbe.

Kamati inaipongeza sana wizara kwa hatua hii yenye mwelekeo wa kuwapatia soko la uhakika wakulma wa mwani pamoja na matarajio ya kupatikana kwa fursa za ajira kutokana kuanzishwa kwa kiwanda hicho. Hata hivyo, kamati inasisitiza kuwa wizara ihakikishe kuwa wananchi walio katika eneo litalojengwa kiwanda hicho wawe wa kwanza katika kufaidika kwa kujengewa kiwanda hicho katika eneo lao.

UTUNZAJI WA MALI ZA SERIKALI:

Mhe. Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kama zilivyo wizara nyengine za serikali, ina dhima kubwa ya kutunza mali za serikali zinazomilikiwa na wizara hiyo. Kamati imebaini kutotunzwa vyema kwa mali za wizara hii ikiwemo majengo na maeneo mbali mbali. Kamati imeshuhudia nyumba ya wizara iliyopo Mkoroshoni, Pemba kwa miaka mingi imeachwa bila ya mlinzi wala usimamizi mzuri, jambo ambalo limeifanya nyumba hiyo kuharibika. Kutokana na hali hiyo, kamati inashauri kuwa nyumba hiyo ivunjwe, matofali na mabati ya nyumba hiyo yahifadhiwe na baadaye wizara itafute fedha kwa ajili ya kuijenga upya nyumba hiyo.

Mhe. Spika, kamati yetu ilipata fursa ya kutembelea nyumba na maeneo ya wizara hapo Mazizini na Mtoni na kubaini kuwa baadhi ya nyumba hizo zinakaliwa na watu wasiostahiki licha ya watu hao kuandikiwa barua na wizara kuwataka wazirejeshe nyumba hizo kwa Wizara. Hivyo, kwa vile wizara bado inazihitaji nyumba hizo na kwa vile tayari imeshaanza kuchukua hatua ya kutaka kurejeshwa kwa nyumba hizo, ni vyema ikalifuatila zaidi suala hilo.

Mhe. Spika, kamati imegundua kumegwa kwa eneo la Mtoni kwa kujengwa nyumba katika eneo la Wizara. Kutokana na hali hiyo, kamati inaitaka wizara kufuatilia kwa makini vielelezo vyote vinavyohusu eneo la Mtoni na kuweka mikakati itayozuia uvamizi zaidi katika eneo hilo. Kamati pia imeitaka wizara ifanye uhakiki wa kuyatambua maeneo yake yote, ili kuepusha uvamizi na kupotea kwa maeneo ya wizara.

Mhe. Spika, kamati imegundua kuwa maeneo kadhaa ya wizara kukosa hati miliki hususan eneo la Nziwengi, Pemba ambalo limetengwa kwa ajili ya karantini ya mifugo. Ni jambo la kustaajabisha kwamba eneo hilo limeshapimwa na malipo kwa ajili ya hati miliki yameshatolewa kwa Wizara husika.

Hivyo, kamati inaitaka wizara kukumbusha na kufuatilia zaidi kwa wizara husika kuhusu hati miliki ya eneo hilo. Aidha, kamati kupitia taarifa hii inaiomba wizara inayohusika na utoaji wa hati miliki za maeneo, kuuona umuhimu wa kuipatia Wizara ya Mifugo na Uvuvi hati miliki ya eneo hilo muhimu la karantini ya mifugo.

WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA USHIRIKA:

Mhe. Spika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ina jukumu kubwa la kusimamia shughuli zote za kuongeza ajira zenye staha kwa vijana na kuinua hali zao na Taifa kwa ujumla. Kutokana na dhima hii nzito inayobebwa na wizara hii, iko haja kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwakabidhi rasmi jengo la wizara wanalolitumia hivi sasa.

UJENZI WA JENGO LA WIZARA:

Mhe. Spika, kamati inaishauri Serikali Kuu kuiweka ajenda ya uendelezaji wa ujenzi wa jengo la wizara hii kwenye vipaumbele vyake kwani mazingira ya baadhi ya Idara zake ikiwemo Idara ya Ushirika hayaridhishi na hayaendi sambamba na matakwa ya usalama na afya kazini ambayo Wizara hii inayasimamia kwa taasisi nyengine. Aidha, ni wazi kuwa gharama za uendelezaji wa ujenzi wa jengo la wizara hii zitakuwa ni ndogo ikilinganishwa na ujenzi wa majengo mengine ya serikali ambayo ujenzi wake unaanza upya.

HALI YA VTENGO VYA WIZARA – PEMBA:

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba, Kamati imejionea hali ngumu ya watendaji waliomo kwenye jengo la Wizara liliopo Chake chake ambalo linatumiwa na Idara tatu (Idara ya Ajira, Idara ya Afya na Usalama Kazini na Kamisheni ya Kazi). Jengo hilo ni dogo mno ikilinganishwa na idadi ya watumiaji pamoja na zana walizonazo. Aidha, tatizo la usafiri limeonekana kuwa ni sugu kwa idara hizo ambazo zimekuwa na kazi za ufuatiliaji wa vikundi, *SACCOS* na miradi mbali mbali mjini na vijini. Hivyo, kamati inaitaka wizara kuvitupia jicho la huruma vitengo vyake vya Pemba, ili viweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

AJIRA MBAYA ZA WATOTO:

Mhe. Spika, kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa kutekeleza Mradi wa kutokomeza Ajira mbaya za Watoto ambao unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Wizara hii kupitia Kamisheni ya Kazi na Shirika la '*Save the Children'* chini ya ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya ambapo jumla ya watoto 377 wamerejeshwa skuli katika shehia 16 Unguja na Pemba. Shehia hizo ni Ndagoni, Wesha, Vitongoji, Uwandani, Micheweni, Mjini Kiuyu, Majenzi na Kangani kwa upande wa Pemba na Kijini, Nungwi, Mchangani, Mkokotoni, Marumbi, Uzini, Charawe na Chwaka kwa upande wa Unguja.

Ni wazi kuwa wizara hii imefanya juhudi hizo kwa kutambua kuwa elimu ndiyo msingi wa maendeleo ya taifa hili, hususan ikitolewa kwa watoto ambao ndio tegemeo kubwa la taifa hapo baadae. Ni matumaini ya Kamati hii kuwa wizara itaendelea na jitihada zake hizo, ili kuhakikisha kuwa watoto wengine zaidi walio katika shehia mbalimbali nao wanafaidika na mradi huu.

PROGRAMU YA KAZI NJE NJE:

Mhe. Spika, kamati pia ilipata nafasi ya kupokea taarifa ya Programu ya Kazi Nje Nje na kuonana na vijana walio katika progaramu hiyo pamoja na kutembelea vikundi pamoja na vijana waliofaidika na mafunzo yanayotolewa kupitia programu hiyo ambayo ni ya ujasiriamali na biashara. Miongoni mwa vijana waliofaidika na mafunzo hayo ambao Kamati ilipata fursa ya kuwatembelea, ni vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya walio katika vituo vya kurekebisha tabia (*Sober Houses*).

Kwa masikitiko makubwa, kamati imepokea taarifa ya kuwa hadi sasa vijana wanaoishi kwenye nyumba za kujirekebisha kutokana na matumizi ya dawa za kulevya hawana uhakika wa hatima yao mara baada ya kutoka katika majumba hayo, kwani tayari wameshatengwa na familia zao na jamii kwa ujumla. Hivyo, Kamati inaishauri wizara na taasisi zote zinazohusika katika mapambano haya kubuni mipango madhubuti ya kuwapatia miradi endelevu vijana hawa, ili kuwajengea mustakbali mwema wa baadaye na kuwanusuru wasirejee kwenye matumizi ya dawa hizo hatari kwao na taifa kwa ujumla.

IDARA YA MAENDELEO YA USHIRIKA:

Mhe. Spika, baada ya Kamati yetu kupata fursa ya kutembelea Idara ya Ushirika ya Dar-es-Salaam na kujifunza jinsi vyama vya ushirika vinavyoendeshwa, kamati inatoa wito kwa Idara ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar kujipanga vizuri katika upande wa rasilimali watu hususan kwenye fani ya uongozi, wakaguzi na maofisa ushirika, ili kuiepusha nchi yetu na mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa Sera na Sheria ya Ushirika huko Tanzania Bara. Aidha, kamati inaona kuwa ipo haja ya kukuza ushirikiano uliopo baina ya Idara hizi mbili za Tanzania Bara na Zanzibar kwa kuandaa progarmu za pamoja na kutembeleana.

Mwisho kabisa Mhe Spika, kamati yetu inatoa shukurani za dhati kwa wizara hizo tatu inazozisimamia kwa ushirikiano wao waliouonesha kwa kamati hii kwa kipindi chote ambacho kamati hii imekuwa ikifanya kazi. Napenda pia kutoa shukurani za dhati kwa usikilizaji mzuri wa Waheshimiwa Wajumbe wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii na tunatoa wito kwa serikali kuyatekeleza kwa vitendo yale yote yaliyoagizwa na kushauriwa na kamati, ili kuongeza ufanisi wa Wizara hizo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kamati imepokea kwa masikitiko kwa jambo ambalo limetokezea kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Spika, kuna Mhariri Mkuu wa Habari *ZBC* kuna maelezo kwamba mwenzetu huyu alifanya kosa la utovu wa nidhamu, na jambo la pili alitumia fedha shilingi milioni 6 bila ya kufuata taratibu na Katibu Mkuu wa Wizara alichukua hatua ya mwanzo kwa kumpa uhamisho wa kiidara. Kwa kweli lililotokea Waziri wa wizara husika amemrejesha jambo linaloleta utata na ambalo halitoi picha nzuri kwenye utendaji ndani ya wizara.

Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri atakapokuja namuomba kupitia kwao Mhe. Spika, kutoa majumuisho ya wizara yake, basi airidhishe kamati hii ambayo imefanya kazi kwa muda wote huo pamoja na Baraza hili, ili jambo hili liweze kuwekwa vyema na kuelezwa pale wananchi wanapolihoji.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Spika kwa ruhusa yako pamoja na Wajumbe wa Baraza hili naomba kuwasilisha na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana kwa ripoti hiyo ya Kamati. Kwa hiyo, naomba sasa twende kwenye kuchangia na nianze kumkaribisha Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadaye Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kuweza kuchangia wizara tatu.

Naomba niende moja kwa moja kwenye Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, tunayo mambo mengi huko nyuma hasa katika masuala ya bajeti wakati ule tulijaribu kuyaeleza, ili wizara husika iweze kutekeleza na tulitarajia katika uwasilishwaji wa ripoti ya Kamati hii mpya ya hivi sasa tulitegemea kupata majibu ambayo tayari yameshatekelezwa.

Pia naomba nianze na sehemu ambazo niliwahi kuzichangia na bado katika buku nimejaribu kuangalia sijapata kuziona humu. Lakini tuseme binadamu ndio sisi mapungufu yamo na mambo mengine tunakuwa nayo.

Sehemu ya kwanza ni kwenye Mahakama ya Kazi, niliwahi kueleza mimi kwamba hii bado inajidhorotesha katika utendaji wake hasa katika masuala ya maposho na kupitia kwa wale wazee wetu *assessors* wale hawapati yale maposho yao, kwa mujibu wa sheria imo katika vifungu ambavyo kwa mujibu wa sheria zetu 98 hayo mafungu mpaka leo hawayapati na hata wakiyapata wanakuwa wanayapata kidogo kidogo.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana kesi zinachelewa kutolewa uamuzi na watu wanazidi kuharibikiwa katika masuala yao, kwa sababu kuna wengine wanakuwa wanasimamishwa kazi au mtu ameamka vibaya bosi anamfukuza mtu kinyume na utaratibu. Kwa hivyo, suala hili ningeomba sana wizara husika hebu tulione hili suala tunakoelekea huko kusiwe kugumu na tuwe na urahisi wa kuweza kulitatua suala hili na kulimaliza.

Mhe. Spika, Idara ya Kazi niseme mmoja katika mihimili mikuu na hasa katika kuwaondoshea wananchi wa Zanzibar unyonge na umasikini. Kwa kweli idara hii Mhe. Spika mara nyingi sana huifanyia kazi mimi na ninakuwa karibu sana, lakini kuna baadhi ya mambo huwa yananisikitisha na hasa nikisikia dhana ya jambo kwa kunyoshea mtu kidogo nakuwa nasikitika sana.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huleta mambo kwa manufaa ya sehemu mbili, ya kwanza ni kuwanufaisha wananchi wenyewe, pili serikali kupata kodi zake. Lakini kwa upande mwengine huwa inakuja kwa tafsiri nyengine ambayo si nzuri kuisema. Mhe. Spika, tumesema kuwa Zanzibar sasa tumeleta sera ya utalii, watu wenye Makampuni yao ya *tours* waje na kila kitu wafungue, ili neema ile wazanzibari tuweze kupata tunufaike na tuondokane na umasikini.

Mhe. Spika, matatizo yanakuwa ni mengi sana na haya Mhe. Waziri akubali tu, kwamba tunayasababisha sisi idara au *management* yenyewe inayohusika kule kutoambizana ukweli. Mhe. Spika, wazee wamesema ‘ukificha sana mke ndugu hutozaa’ na hii ndio sababu iliyotufikia kwamba tujidhoroteshe na sheria zetu tulizokuwa tunazitunga.

Mhe. Spika, *Wallahi* niseme ninakuheshimu sana mzee wangu Mhe. Spika, *experience* yangu imetokana na wewe *otherwise* kama si wewe mimi nisingekuwa na *experience*, na kwa nini naijali na ninaifanyia kazi, kutokana na kwamba umeniwezesha pamoja na kunifundisha kupitia *UNDP* ndipo ninapofika pahala kuwa naona uchungu tunasema hapa na hatimaye yale tuliyokusudia hayafanyiwi kazi. Mhe. Spika, naomba ulinde kiti chako.

Mhe. Spika, Idara ya Kazi kuna *Zan Tour* madereva wanapata tabu sana wanasumbuliwa na mhusika pale ambaye ni Muhindi ametoka India na kuja Zanzibar anawaambia kwamba serikali yako yote nimeiweka kwenye kiganja hapa; anajisifu hivyo na ukitizama si uongo. Kwa mfano, Mkurugenzi amekwenda anamwambia *this is a chair* anakaa hapa Mkurugenzi na ninampa fedha na hiyo ni dhana potofu, *I don’t know*, lakini hivyo ndivyo inavyozungumzwa na kama ni kweli au uongo *correction* ataijua yeye kwa sababu yeye ndiye anayekwenda.

Sasa akiondoka yeye inakuwa basi anawaambia mnaona nyinyi yule tayari nimeshaonesha ile, yaani kila mkienda kule nyinyi hamtofanikiwa jambo la aina yoyote na kweli. Mhe. Spika, kesi hiyo kila siku *Zan Tour* wanabughudhiwa haishi.

Kwa hivyo, kama ni kwenye Mkurugenzi wangu kitendo hicho anacho basi akiache mara moja kabisa na hivi sasa si wakati wa kuoneana muhali, isipokuwa ni kuambizana ukweli tu, na ikiwa hawezi basi ajiondoe na Mhe. Rais atangaze mwengine tumechoka na kudhalilishwa wananchi wetu katika maeneo yao.

Kwa kweli watu wa *Zan Tour* kila siku wanapeleka malalamiko yao kuhusu maposho yao masikini ya Mungu wanatoka makwao wanakwenda mashamba na wala hakuna *allowance* ya aina yoyote, wanadhalilishwa na halafu kuna wengine mule mule sisi tunawasaidia, yaani wale wazanzibari wenyewe tunawaumiza wazanzibari wenzetu, mimi mtu kama huyo humuona mtu wa maajabu makubwa sana, na wala sijui mtu wa aina gani kumuumiza ndugu yako. Mhe. Spika, naomba sana suala hili lifikiriwe.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye mahoteli. Mhe. Spika, mimi niliomba *special* ziara na nikasema kama hawana mafuta basi tutachangia. Mhe. Spika, kuna matatizo kwenye mahoteli namna moja au mbili.

Kwanza wazanzibari tuko kidogo kwenye ajira; na hili tusikatae tukubaliane nalo ndugu zetu wa Kenya hivi sasa wameshakuwa wengi na hilo hamtaki kuliona mnalifumbia macho siku zote tukikwambieni hamtaki kuliona. Kwa kweli leo tunashindwa kuwapa watoto wetu ajira na tunawasomesha katika Chuo kile pale cha Maruhubi ambacho kinasomesha vizuri kabisa, lakini nacho pia hakithaminiwi na wala hakishirikishwi.

Kutokana na hali hiyo, hatari inatokezea kwa sababu tunaeleza kwa kusema na tunajua. Kwa mfano, leo mtu Mkenya anayo miaka 6 na *still* anaendelea pale ukimuuliza kamuelimisha nani hana aliyemuelimisha na sheria iko wazi na tunashindwa kuwaondoa sijui kwa sababu gani, labda tunapewa fedha na hilo kweli na rushwa hii itakwisha lini? Mhe. Spika, sasa tutawatia pingu, na Kamati ya *PAC* kamata tia pingu na tutafanya hivyo Mhe. Spika na wala hakuna mzaha tena na Kanuni tutaweka kando tutamtia mtu pingu.

Mhe. Spika, naomba sana kuhusu ziara ifanyike na wizara yetu ifanye, wenzenu Kamisheni ya Utalii, Uhamiaji wamekubali na bado nyinyi tu na sijui kitu gani na Mhe. Waziri nimeshamwambia kaka au mzee wangu, kwamba ziara hii ni muhimu itatusaidia, ili tuone yale mapungufu kwa sababu tunakimbia na kuyakwepa tu, lakini mimi nitakwenda nayo sambamba na wala sitokubalina naye. Kwa hivyo, nitahakikisha Mhe. Spika kwamba kabla ya bajeti ziara tumeshafanya na tunaleta majumuisho hapa Barazani. *(Makofi)*

Nikiondoka hapo sasa naomba niende katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Kwa kweli wizara hii kuna matatizo mengi ya hawa wawekezaji wetu na sijui wizara inachukua hatua au sheria inawalinda vipi au inawabana wapi. Mhe. Spika, wawekezaji wetu wanadhalilishwa kwa kunyang'anywa ardhi zao na sijui wizara inalijua hilo na kama inalijua sijui kama inafuatilia hilo nasema hivyo Mhe. Waziri sijui sababu gani zinazofanya hivyo.

Vile vile pale katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuna Katibu ambaye siye na kama ingewezekana Mhe. Waziri amuondoe, kwa sababu ni moja miongoni mwa kuwadhalilisha hawa wawekezaji. Mhe. Spika, kijana yule hafai na tumedungua kwamba miongoni mwa

matatizo ni hilo na wala tusimuonee haya mtu, kwa sababu anafanya mambo nafikiri Mhe. Waziri hayaoni, lakini si vizuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunaomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba amuone huyo mtu atamuweka pabaya na ushahidi upo, na akitaka mimi nitamwambia na wala hakuna kifichana hivi sasa Mhe. Spika isipokuwa tuambizane ukweli tu.

Katika wizara hii Mhe. Spika na ninamuomba sana Mhe. Waziri awe na *special day* ya kuwatembelea hawa, kwa ajili ya kuwakagua na kuwasikiliza matatizo yao nini na akutane na wizara husika, ili aweze kuwasaidia na kuondosha tatizo.

Pia suala la *security* bado hatujaandaa vizuri ya kuwalinda wawekezaji katika mahoteli yao; wanavamiwa ovyo tutawakosa jamani hawa tangu hapo tunasema uchumi wetu mdogo basi tutazidi kuwa na uchumi mdogo na kuwa chini kabisa na wananchi wetu wabakie kuhunika na halafu tupige kelele watoto wetu wezi, wizi gani tumeusababisha sisi wizi, hili tukubaliane.

Sasa twende katika habari yenyewe tunao waandishi wetu humu ndani ambao hawa wanatuzunguka, *Alhamdulillah* wanatuelewesha vizuri, lakini hatuoni haya shilingi 5,000/= tunawalipa kwa siku, tunawasimamisha pale wakati mimi mzima wa afya na kila kitu siwezi kusimama masaa yote na wao wanasimama wale pale tunawatizama vipi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lazima tuwahurumie na wao angalau tungeweka kwenye 50,000/= na hata 100,000/= si vibaya, kwa kweli wanatufanyia mambo mazuri na hilo naomba sana Mhe. Spika. Kwa mfano, tunao waandishi wetu wanaandika ripoti vizuri, basi ni shilingi 5,000/= Mhe. Spika. Jambo la kusikitisha zaidi na uchungu hiyo shilingi 5,000/= yenyewe wanaipata sio kwa *time* yenyewe na wanapewa chiri chiri sijui kama za mwaka jana wameshapata au kikao kilichopita, tunawaonea, hatuwathamini.

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba yeye jemedari ajitahidi kuwarekebishia mambo yao. Vile vile Mhe. Waziri bado anaendelea na sifa nzuri kwenye wizara yake, lakini asijekujiharibia kwa watu fulani na wala asiwaonee haya, kwa sababu hawa ndio wale watu Wakurugenzi au Makatibu wanakwenda kufanya vibaya na wanawadhalilisha hawa, ili wasitoe ripoti vizuri pamoja na kutofanya kazi vizuri. Kwa hiyo, Mhe. Waziri afanye kazi yake, kwa ajili ya kufanikisha vizuri.

Mhe. Spika, nikiendele kuna hichi kitu ambacho ni *transmitter*. Kwa kweli hapa naomba kuuliza *transmitter* hii ya *ZBC* au *AGAPE*. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi aje kunielezea ni nani hasa mmiliki wa hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa haraka haraka nasikia ah! Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ilitoa fedha shilingi milioni 8 kwa ajili ya masuala ya *digital*. Sasa sijui *digital* hiyo kwa lengo la kurahisishia kabisa hii Kampuni ya *AGAPE* au kuweka sawa hii *ZBC*, pia na hili namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atakapokuja na suala hili anifahamishe.

Tukija katika michezo na ninakumbuka kwamba Mhe. Waziri nilimwambia kuhusu suala la uchaguzi. Kwa kweli suala hili najua Mhe. Waziri linamkera na nitaendelea kumkera, ili akamilishe kwa ujasiri wake watu wa riadha waweze kufanya uchaguzi, kwa sababu kuna watu wanafanya *sabotage* kwa makusudi. Mhe. Spika, kwamba Katibu ambaye yupo sasa hafai anafanya mambo kinyume na utaratibu, sasa ndio maana kila siku uchaguzi gani huo uliokuwa miaka 20 usiofanyika na kila siku kesho kesho tu. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ajitahidi, ili aweze kufanikisha.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la Hoteli ya Bwawani na katika wizara hii ndio ya mwisho, lakini sio mwisho kumaliza isipokuwa kwa wizara hii. Mhe. Spika, Hoteli ya Bwawani pale kuhusu hati miliki tumeambiwa mpaka hivi sasa haijulikani iko vipi. Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, afuatilie hati miliki na tuone kwa uangalifu kabisa na iweze kupatikana na tujue nani mmiliki hivi sasa.

Vile vile niseme kuwa suala la Hoteli ya Bwawani wafanyakazi wamesimamishwa ambao niliwazungumza wakati uliopita wako 15 na wengine wana ubadhirifu wa fedha. Nadhani jambo la msingi ni kukaa nao pamoja na kuwauliza hivi ni kweli na kama ni kweli watiwe hatiani na kama si kweli basi warejeshwe kazini waendelee kufanya kazi zao.

Mhe. Spika, hili ndilo tatizo na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora juzi ameeleza vizuri sana na Mwenyezi Mungu ambariki, ampe hekima na aeleze vile vile siku zote anavyoeleza, kwa kweli ameonesha nia jinsi gani watu wanavyofukuzwa kazi kiholela na ameonesha utaratibu *stage by stage*.

Kwa hiyo, namuombea sana na hivyo ndivyo anavyotakiwa waziri a-*clear* katika mambo ambayo yenye matatizo kwenye wizara zao, kwa kweli ametusafishia na Mwenyezi Mungu atamjaalia kumuendeleza kumpa vyeo mpaka kufa kwake kwa baraka na mimi sharifu *Inshallah* na Ijumaa ya leo Mwenyezi Mungu aibariki. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namalizia Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tatu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, sawa ndio namalizia Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Kwa kweli wizara hii niseme kwamba wamejitahidi sana katika utendaji wao wa kupandisha mbegu za kisasa na hilo tumeliona na walikuwa wakipiga kelele mitambo na ninafikiri hivi sasa mitambo imekamilishwa na wameipata.

Pia naomba kusema kwamba masuala ya mradi uliopita naomba tena wautafute, kwa ajili ya kuweza kuwasaidia wananchi kwa kupata maboti ya kisasa ambayo yanakwenda na wakati na wala hatuvitaki tena viboti vya mbao, bora wakawie lakini wakituletea basi watuletee *fiber* ambayo ni *strong* inavyokwenda katika bahari, yaani *deep sea*. Mhe. Spika, tumeshachoka na vibao vile vya kupigwa kofi na kuondoka pale na wala visitusaidie chochote na itakuwa ni haraka kwa serikali pamoja na wafadhili wetu.

Mhe. Spika, kuna mfadhili hapa ambaye anataka kuleta neema. Mfadhili huyo anataka kuleta mifugo ya kisasa kwa kupitia ng'ombe wa kisasa na sijui tuna tatizo gani? Mhe. Waziri namuomba kupitia kwako Mhe. Spika, labda wakati atakapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho aje anieleze amefikia wapi huyo na tuone nani mwenye matatizo ambaye anazuia, kwa sababu alitaka sehemu ambazo ni za upandaji wa majani kwa ajili ya ulishaji wa ng'ombe.

Kwa kweli mpaka leo tunaona kimya na tunamuweka kwenye *dilemma* tu na wala hajui afanye nini na kiwanda tayari ameshajenga, lakini wale ng'ombe wenyewe husika kwa ajili ya kutoa maziwa hajaleta kwa sababu ameshindwa kupata maeneo. Mhe. Spika, tunaomba sana suala hilo kwa ajili ya kuweza kupata.

Mhe. Spika, naheshimu sana wakati wako kama nilivyokwambia mwanzo mzee wangu nakustahi na hapa naunga mkono ripoti ya Kamati kwa asilimia mia moja na ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Ripoti hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Mhe. Spika, kabla sijaanza na mchango wangu jana Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alitoa masikitiko yake hapa makubwa ya kuona kwamba tunajadili taarifa hizi ambazo ni muhimu lakini jambo la kusikitisha ni kwamba Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, yaani wale ambao ni wahusika hawapo katika Baraza hili, na hili ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Spika na leo ndivyo ilivyo katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, hili ni tatizo kubwa kwa sababu haya tunayoyazungumza ni muhimu yanahitaji kufuatiliwa na Mhe. Waziri peke yake haiwezekani akakaa hapa akaandika kila taarifa ambayo inatoka na kuna nyengine zinampita, lakini kama wapo wale basi wanaweza kuchangia na kuweza kusawazisha yale ambayo tunayazungumza.

Lakini hapa wizara zote tatu ikiwemo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Wizara Kazi na Wizara ya Mifugo na Uvuvi watendaji wao hawapo, isipokuwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na Mhe. Waziri hongera sana. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, nianze kwa kusema…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, watendaji wapo lakini viti vya mbele wanavikataa kuvitumia, sasa wengine hawaonekani kule. Kwa hivyo, nadhani hasa Makatibu Wakuu wanaheshimu kukaa viti vya mbele. Mhe. Mjumbe, endelea. *(Makofi)*

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, baada ya maelekezo yako nakushukuru sana. Lakini niwaombe kama ulivyotoa muongozo wao basi wakae mbele tuwaone na sio wajificheni, kwa sababu wakijificha sisi tunatoa malalamiko yetu. *(Makofi)*

Sasa naomba nianze Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kuendeleza na kuthamini juhudi za wasanii wetu ameweza kufanya ukarabati mkubwa wa ukumbi ule ambao wanatumia wasanii wetu katika

kufanya shughuli zao za kurikodi pale Rahaleo. Na Mhe. Rais ameyafanya haya kutokana na juhudi ambazo wasanii wetu wamekuwa wakiitangaza nchi yetu ya Tanzania na Zanzibar kwa ujumla katika ulimwengu huu hususan msanii ambaye jana ametutoka mama yetu, kipenzi chetu Bi Kidude Binti Baraka. Nichukuwe fursa hii kutoa pole kwa wafiwa na wasanii wote wa Tanzania na Zanzibar kwa ujumla kwa msiba huu ambao umetokea.

Lakini Mhe. Spika, mbali na juhudi ambazo zimechukuliwa na Rais wetu na serikali kwa ujumla kuufanyia ukarabati ambao ulifunguliwa hivi juzi na Mhe. Rais. Lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, ukumbi ule umekuwa ukitumiwa kwa shughuli ambazo sizo zilizokusudiwa. Hivi sasa ukumbi ule unafanyiwa shughuli za harusi na kukodishwa katika masuala mengine. Hili Mhe. Spika, nadhani eneo lile ni eneo nyeti na ni eneo ambalo Rais aliona kwamba ipo haja na ni muhimu hasa kuwafanyia wasanii wetu ili wasipate tabu katika kurikodi shughuli zao. Lakini tunaporuhusu masuala ya kwenda kufanya harusi pale tutaondoa haiba na uzuri wa eneo lile. Kwa hivyo Mhe. Spika, Waziri atueleze sababu gani ambazo ameruhusu kufanyika shughuli zile za harusi.

Mhe. Spika, baada ya hapo nije suala zima ambalo linazungumza masuala yetu ya michezo ambao kamati hii imetoa maelekezo mbali mbali. Mheshimiwa kamati ilitoa maelekezo kutokana na kukosekana kwa ushirikiano kwa vyama vyetu hivi vya michezo vya Tanzania Bara na Zanzibar hususan *TFF* na *ZFA*.

Mhe. Spika, *TFF* ni chombo ambacho kinaongoza mpira wa miguu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa sote ni watanzania, timu ya taifa ni timu ya Tanzania yaani Tanganyika na Zanzibar. Mhe. Spika, timu hii ya taifa ya Tanzania yaani Taifa Star wewe ni yako, mimi ni yangu na Mheshimiwa wa Mpendae Mhe. Dimwa ni yake, Mhe. Said ni yake, Mwakalebela ni yake, Kayuni ni yake ni ya watanzania wote.

Sasa Mhe. Spika, imenibidi nizungumze haya kutokana na dharau ambazo *TFF* imekuwa ikitufanyia wazanzibari. Hivi juzi *ZFA* iliiomba timu ya taifa ya Tanzania ije Zanzibar ili kucheza mchezo maalum na timu ya *Zanzibar Haroes* kwa ajili ya kusherehekea sherehe zetu za muungano tarehe 26. Kwa sababu timu yetu ya Taifa ya Tanzania ambayo inashirikisha wachezaji wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar inaundwa na wachezaji wote pande zote mbili ili waje hapa Wazanzibari na wapenzi wa mpira wa miguu Zanzibar waione timu yao. Mbali na kufanya vizuri katika mashindano haya ya mchakato mzima kushiriki katika kombe la dunia, kwa hivyo wazanzibari timu yao waliitaka ije hapa waione na washerehekee sherehe za muungano katika mchezo huu wa mpira wa miguu.

Lakini cha kusikitisha Mhe. Spika, *TFF* wamekataa ombi lile na majibu walioleta wataleta timu ya taifa ya vijana ya *under* 20 hii ni dharau. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri kukaa katika kutatua migogoro namisuguano ambayo ipo kati ya *TFF* na *ZFA* na kukosa ushirikiano kwa sababu hivi ndio kukosa ushirikiano. Lakini haya hayatoshi Mhe. Spika, migogoro ambayo tumekuwa tukiipigia kelele kila siku ndani ya *ZFA* kuanzia ngazi ya taifa, ngazi ya Wilaya na hii ndio inayosababisha kuzorota na kudumiza mchezo wetu wa mpira wa miguu Zanzibar.

Mheshimiwa hivi pundi *ZFA* ilifanya uchaguzi na tukatarajia kwamba mafanikio mategemeo makubwa ya Zanzibar kuona kwamba tunatokana katika migogoro na kuelekea katika kuinua

soka letu la Zanzibar. Lakini mimi nadhani Mheshimiwa haya yote yanatokana na kupita kwa wakati wa katiba ya *ZFA* ipo haja ya kuisimamia, kuirekebisha Katiba hii na hata viongozi wetu wakuu wamekuwa wakipiga kelele suala hili.

Sasa katika haya maelekezo ambayo kamati yameyatoa yamo haya ili kuinua na kuufufua mchezo wetu wa miguu, Wizara inahitajika kufanya kazi ya ziada, serikali inahitajika kufanya kazi ya ziada kwa kushirikiana na Wizara, Baraza la Michezo na *ZFA* na vyama vyengine vya michezo.

Mheshimiwa mbali haya hayatoshi lakini kwamba vyama hivi pia vimekosa ofisi ya kufanyia kazi zao hii ripoti imeeleza. *ZFA* haina Ofisi, vyama vyengine vyote havina ofisi vinakodi vichochoroni, *ZFA* imekodi hapo keshokutwa unaambiwa kwamba wamemaliza kodi. Sasa Wizara ifanye kazi ya ziada kuwasaidia vyama vyetu vya michezo waondokane na haya matatizo waliyonayo.

Mhe. Spika, mtoto akilia baba inahitajika kumnyamazisha na kumsaidia mtoto wake, wapo wadau mbali mbali ambao wana uwezo, wapo viongozi humu ndani ya Baraza ambao wanaweza kusaidia. Waziri ikiwa hawezi ameshindwa na suala amwambie Waziri mwenzake. Yupo Maalim Haroun yule pale ana uwezo wa kusaidia wa kutafuta nyenzo mbali mbali zakuendeleza michezo, naye mwana michezo maarufu Mhe. Machano yupo. Mhe. Waziri usione tabu kuwashirikisha mawaziri wenzako, kuwashirikisha viongozi wenzako katika kuendeleza na kufufua mchezo wetu wa mpira wa miguu. Kwa sababu ni mchezo ambao unapendwa na wazanzibari wote, watanzania wote ulimwengu mzima.

Mhe. Spika, serikali imesaidia katika kuendeleza kituo cha michezo kule Dole lakini Mheshimiwa kituo kile hakina mbele hakina nyuma kile nikichaka tu sio kituo cha michezo. Unapokwenda kuangalia vituo vya wenzetu *Football Academy* unahakika hapa kweli hapa wamekuja kufundishwa watoto *football*, kile bado hakijakuwa *Football Academy*. Ipo haja kufanya kazi ya ziada. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika ahadi zake katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, ameahidi kuendeleza vijana, kufufua michezo, kujenga viwanja vya kisasa. Haya yote anayoyasema sio afanye yeye, ameweka wasaidizi wake Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, na wao watafute na njia na mbinu ya kuyatekeleza haya basi serikali haiwezi kufanya yote watyafutwe wahisani na wafadhili mbali mbali.

Mhe. Spika, nije *ZBC*. *ZBC* hivi sasa tuko katika *digital*, Mheshimiwa Zanzibar na ina vituo mbali mbali ikiwemo kama vile coconut, wapo Zanzibar Cable na wazanzibari wameungana na vituo hivi kutokana na ubora wa *channel* ambazo wanaonesha hususan masuala haya ya michezo ikiwemo *football, league* za ulaya, *champion* league.

Sasa nadhani *ZBC* ipo haja sasa ya kukaa na kutafakari kuonesha michezo hii ya *Champions league*, ligi kuu ya Uingereza na mengineyo na michezo mbali mbali ili wazanzibari wapenda michezo wavutike kununua ving'amuzi hivi bila ya hayo itakuwa pale inakaa *AGAPE* tu. Hii *AGAPE* mwisho itahamia Gando na Rahaleo kwa sababu ndipo ilipo, Mpendae haitafika wala Makunduchi haitafika. Lakini kama watafanya ukarabati wa kuboresha vipindi vyao ninakuhakikishia hivyo vyengine vyote vitakuwa havifai wote wataelekea kwa *ZBC television*.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo ninaheshimiu muda wako, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja na ninamuomba sana Waziri afanye kazi kama alivyosema Mhe. Mshimba anafanya kazi vizuri aendelee hivyo hivyo ili kwa faida ya Wazanzibari na Watanzania kwa jumla.

Baada ya kwisha kusema hayo ninakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa hii asubuhi hii pengine kuwa ni msemaji wa mwisho. Pia nikupongeze wewe kwa busara, hekima, ulizonazo katika kukiongoza chombo hiki. Kwa sababu kama si hekima, busara na maelekezo yako kwa kweli leo tusingemaliza kazi. Kwa sababu ulitupiga panga sana lakini kwa kukuheshimu na kwa busara zako tumekubali na tunategemea kwamba kazi itamalizika leo. Hii ni busara na hekima zako, vyenginevyo tungefika jumatano ijayo kwa kazi ambazo tulijiandaa kuhusu hizi ripoti za kamati.

Mhe. Spika, baada ya kukupongeza wewe kwa busara zako na hekima zako pia niwapongeze mawaziri waliohusiana na ripoti hii ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Utamaduni na Habari kwa vile walivyowasilisha taarifa zao kwa umahiri, kwa umakini hnii inaoneshea kuwa wanao ushirikiano mkubwa na watendaji wao ndio wakaweza kufikia hapo, niwaambie ahsanteni sana.

Mhe. Spika, serikali mara nyingi tuna makusanyo mazuri ya fedha ya kila mwezi lakini kwa mwananchi wa kawaida haoni kuwa kuna maendeleo yoyote katika serikali. Kwa sababu yeye kila siku maisha yanambana na kumkamua. Kwa hivyo yale maendeleo na makusanyo ya fedha ambayo serikali inatangaza kila siku yanapanda juu, lakini maisha ya mwananchi wa kawaida yanarudi chini. Sasa serikali kupitia wizara zake mbali mbali zinajitahidi kuandaa taratibu za kuweza kujaribu kuwakamua wananchi katika hali hiyo ngumu ya maisha.

Mhe. Spika, nianze na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu kwenye chakula kiteweo ni muhimu sana na viteweo vyote vimo ndani ya Wizara hii, samaki na mazao yote ya baharini ambayo yanaliwa yapo kwenye wizara yake na huko nchi kavu ng'ombe, mbuzi, kuku na wengineo wote ni Wizara hii. Kwa hivyo Wizara hii imekusanya jambo moja muhimu sana kwenye chakula kiteweo, ili viteweo vipatikane vizuri lazima wafugaji na wavuvi waandaliwe vyema ili waweze kuzalisha hivyo viteweo ambavyo vitaweza kukidhi haja ya matumizi yetu na ikiwezekana waweze kuuza nje kujipatia fedha.

Mhe. Spika, Wizara hii inayo vikundi vingi vya ufugaji wa ngo'mbe, mbuzi, kuku ambavyo mara nyengine huwa vinafadhiliwa na wahisani mbali mbali kama *PADEP*, *TASAF*, na vyenginevyo. Lakini Mhe. Spika, kwa vikundi vingi mara tu baada ya ule ufadhili kumalizika navyo huanza kuyayuka kama uyoga. Kwa hivyo ningeiomba wizara hii kabla mradi haujaanzishwa kama ni ufugaji wafugaji wapewe taaluma za kufuga hasa pale ambapo tumeamua kuchukua hawa ng'ombe tunaowaita ng'ombe wa kisasa.

Mhe. Spika, katika shehia yangu uliletwa mradi ya *PADEP* ufugaji ng'ombe wa kisasa na wafugaji walinunua ng'ombe 25 wamekufa mmoja mmoja kwa hesabu yangu katika shehia ile sasa hivi wapo ng'ombe watano tu. Nadhani itakuwa sio shehia hii tu hiyo inatokana na kuwa

wale wafugaji waliopewa kazi hii hawakupatiwa taaluma ya ufugaji wa ng'ombe wa kisasa. Na pia pengine haikuangaliwa hali ya hewa ya kule ng'ombe wanakotoka na ile sehemu wanayopelekwa, kutoka sehemu ya baridi kidogo na unampeleka sehemu ya joto kidogo.

Sasa haya mabadiliko ya hali ya hewa yanayowakumba hawa wanyama ni mojawapo pengine ya sababu zinazopelekea ama waumwe na hatimae kufa na hata wale waliozalisha katika maeneo mengi hawazalishi kulingana na ile sifa waliopewa kwa ng'ombe hawa wanaweza kuzalisha mpaka lita kumi, kumi na tano wengine wanazalisha kasoro ya hapo pamoja na kuwa wameitwa kuwa ni ng'ombe bora wa maziwa. Sasa ningeiomba Wizara hii kwa kupitia wataalam wake wa mambo ya mifugo kabla ya mradi haujaletwa walengwa wapatiwe taaluma ya kutosha ili baada ya kupata kazi tu jambo wanalopata ni kazi ya kuchunga lakini tija huwa ni ndogo kwa sehemu kubwa sana. Ni wachache wanaofaidika na kazi wanayoifanya.

Mhe. Spika, kadhalika katika mazao ya baharini kuna hili zao la mwani, zao ambalo wakulima wake wakubwa ni wanawake na zao hili bei yake ni ndogo mno lakini kazi yake mpaka ukapatikana huo mwani ni kazi kubwa mno. Sasa huu mwani unanunuliwa na makampuni binafsi, serikali bado haijakuwa na mpango ya kununua huu mwani hasa kwa kuwa lengo la kuwapa wananchi wetu kufanya hizi kazi ni kuwa wapate tija waweze kujitegemea kimaisha sasa Wizara haioni kuwa ni vyema kama lilivyo vile Shirika la Taifa la *ZSTC* wanavyonunua karafuu na hatimae wao wakasafirisha nje na huu mwani Wizara hii ikaununua badala ya haya mashirika hatimae wao ndio wakatafuta soko ili kuwawezesha hawa wakulima wetu na hii bei ndogo wanaopata kulingana na kazi kubwa wanayoifanya.

Kadhalika Mhe. Spika, bado wavuvi wetu walio wengi wanatumia zana na vyombo vya kiasili katika uvuvi. Ni vyema Wizara hii ikawaandaa wavuvi wetu hata katika kuwaweka katika hali ya ushirika wakawapatia vyombo na zana za kisasa za uvuvi ili waweze kuvua kwa wingi hawa samaki ambao bado inasemekana mna samaki wengi baharini ambao hawajavuliwa.

Mhe. Spika, wavuvi walio wengi bado hali zao za kimaisha ni duni pamoja na kuwa kazi hii wameifanya kwa muda mrefu. Sasa ili kuwanyanya hali zao ni vyema serikali ikawasaidia kuwapatia zana za kisasa za uvuvi.

Mhe. Spika, nije kidogo katika Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kwanza niipongeze sana Wizara hii kwa kila mara tunapoanza kikao chetu cha kawaida kama sikosei huwa wanawaleta wajasirimali wao hapa na bidhaa zao mbali mbali. Na wanakuja watu kwenye vibanda vyao tofauti vikiwa na kazi tofauti za ushonaji, ususi, nyengine zinazotoa taaluma tu ya udhibiti wa mazingira na wengine wanaleta bidhaa ambazo ni za kutumia na nyengine wanaziita kuwa ni dawa.

Mhe. Spika, lakini hizi zinazofanywa kuwa ni dawa kichupa kitasifiwa kinatibu presha, sukari na kutakuwa na maelezo mengi na conclution yake ya kila kichupa cha dawa kinamalizia kinatibu na nguvu za kiume. Kila kichupa cha dawa nilichokipitia na kukisoma wataeleza kinatibu hiki hiki hiki na mwisho wake kinamalizia kutibu nguvu za kiume.

Nimuulize Mhe. Waziri kuna utafiti wowote uliofanywa ili wanaume wasije kuvamia au ni biashara tu, kwa sababu pengine wameona kuwa wazanzibari wana matatizo hayo lakini hatuna

matatizo ya nguvu hizo sasa hizo dawa zinazoonesha hivyo je upo utafiti wa kitaalam uliofanywa au nembo tu ya biashara kutafuta masoko.

Mhe. Spika, mwisho nije kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na nije kwenye sekta moja tu ya hii habari. Mhe. Spika, radio kwa Zanzibari iko zamani mno hata kabla ya uhuru na hii miaka ya karibuni serikali imeruhusu mashirika na watu binafsi kuanzisha taasisi hizi za utangazaji. Kwa hivyo zipo radio nyingi sana za *FM*. Ombi langu kwa Wizara hii iwaandae watangazaji wetu, waandishi wetu kuweza kukabiliana na ushindani wa hizi radio binafsi, wawape mafunzo ya mara kwa mara ya ndani na nje inservice training ili waweze kuendana na kukabiliana na upinzani na radio hizi.

Kwa kuwa katika biashara hii serikali haijajitoa na chombo hiki ni cha zamani sana si vyema nafasi yake kuchukuliwa na hivi vyombo vilivyoibuka tu leo na jana. Ni vyema habari zinazotoka kwenye chombo hiki cha serikali ziwe za kitaalam zaidi, zifanyiwe utafiti na ziwe na ukweli ndani yake. Na hatutafika lengo hilo kama waandishi, watangazaji na wengine hawatoandaliwa vizuri lazima wapewe fursa za masomo ya nje na ndani ili waweze kwenda na wakati kama ilivyo.

Mhe. Spika, ili waweze kutoa taarifa sahihi kuna kipindi fulani sisi tulipokuwa shule kulikuwa kuna kitu kwenye michezo yetu tunaita wrong telephone. Mtu mmoja anamnong'oneza mwenzake jambo mara moja tu lakini harudii, sasa inakwenda mpaka wa mwisho ndio anaetoa sauti kwa lile tamko linalotoka huku akija akiulizwa mtu wa mwanzo alivyosema inakuwa ni tofauti na mtu wa mwisho alivyopokea.

Kwa hivyo tusiwafanye waandishi wetu wajitahidi, msemaji anaposema wao wasije wrong telephone waandike na watangaze kama vile ambavyo msemaji amesema. Waandike na watangaze kama vile tamko lilivyotoka asipambe lugha yake kama mwandishi wa gazeti ili gazeti lake aweze kuuza tu lakini msemaji akawa hajasema vile ambavyo yeye ameandika.

Mhe. Spika, Wizara hii pia inashughuli za huu utalii lakini kwa kuwa serikali na chain ina muungano baina ya Wizara na Wizara mara nyingi hawa watalii wetu wanapokuja wanatembezwa katika sehemu mbali mbali. Mimi ambalo sijapenda hata kidogo wanatembezwa katika lile soko la Darajani ambalo ni chafu halisafishwi na wanapitishwa mule wanachukua picha zetu, samaki walivyoekwa ovyo wanatangaza hivi ndivyo wazanzibari walivyo. Hili si lake la soko lakini mle wanapitishwa kuna watu hata hawa sio wageni kama watakwenda katika masoko yale akimkuta samaki alivyowekwa anaweza akamkataa asimle. Kwa sababu kawekwa katika mazingira ambayo ni mabovu kweli kweli.

Mhe. Spika, ningeomba wizara hii iyazingatie haya yote.

Naunga mkono hotuba ya kamati. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe leo ni Ijumaa kwa hivyo tukatekeleze ibada kwa maana hiyo basi niakhirishe kikao hiki hadi saa kumi na moja jioni leo.

(Saa 6.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mawazo yangu kuhusiana na hii Kamati iliyopo mbele yetu. Mhe. Spika, kwanza niwapongeze hawa mawaziri jinsi walivyoweza kuleta zile taarifa zao za utekelezaji kwa umakini mkubwa. Kwa kweli nimefurahishwa sana nawapongeza sana.

Aidha, nichukue fursa hii vile vile kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii jinsi alivyokwenda pale kuwasilisha taarifa yake. Kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa hili jimbo langu la Wawi nawapongeza sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nianze na hapa kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mhe. Spika, katika wizara hii nianze na suala zima la uvuvi, kwa kiasi kikubwa Wazanzibari wamewekeza maisha yao katika uvuvi na hii ni kutokana na kutekeleza ile azma ya serikali yetu ya kupunguza umasikini na kujiongezea kipato. Katika hili inasikitisha sana kwamba wavuvi mara nyingi wanapata tabu katika uzalishaji wa haya mazao ya bahari, kwani uzalishaji wao ni mkubwa wakati mwengine lakini soko ni tatizo.

Kwa mfano Mhe. Spika, kipindi cha mwezi ukienda giza hapa wavuvi huwa wanavua mazao mengi ya bahari yakiwemo madagaa, lakini matokeo yake soko la dagaa linakuwa halipatikani. Sasa watu hawa ambao wamewekeza maisha yao katika suala la uvuvi sijui waende wapi katika kipindi hichi. Kwa mfano, gharama hata zile za kurudisha mafuta inakuwa shida. Sasa nadhani serikali ingekuja ikatueleza hapa katika kutekeleza ule mpango wake wa kupunguza umasikini na kujiongezea kipato watafanya vipi kuwasaidia wavuvi hawa ambao hulazimika kuuza mazao yao kwa bei ya kutupa hasa katika kipindi kile cha mwezi wa giza.

Mhe. Spika, tumeambiwa hapa katika agizo lile la 13 la wizara hii wamesema wana mpango wa kile kiwanda kukibinafsisha na kuwekeza katika suala zima la kusindika mazap ya habari. Lakini sasa Mhe. Spika, katika hili ningeomba kwamba na zana za uvuvi nazo wawe makini sana, kwa mfano hivi sasa wakati sisi wavuvi wetu wanashughulikia sana mambo ya mashua, ngalawa, sasa wenzetu wanavua kitaalamu sana vifaa. Kuna boti Mhe. Spika, ambazo zina-*detect* mpaka aina ya samaki na idadi yake walioko chini, sisi bado mpaka leo wavuvi wetu wanaendelea kutumia vidai hivi vya kujaribu na kubahatisha, hivi vigalawa vidogo vidogo. Sasa ni lini serikali itawawezesha hawa kuweza kupata zana za kisasa ambazo zikawasaidia katika kuongeza kipato chao.

Mhe. Spika, sasa niende katika suala zima la mifugo, Mhe, Spika kwa sasa vijana wengi wameamua kuwekeza vile vile katika mambo ya mifugo. Nashukuru kwamba Mhe. Waziri katika agizo nambari 16 la utekelezaji amelizungumzia hili, lakini amezungumzia ku-*train* vijana katika Chuo cha Kilimo hapa Kizimbani. Nataka akumbuke tu Mhe. Waziri, kwamba katika Kisiwa cha Pemba hakuna daktari bingwa katika masuala haya ya *animal husbandry*, mtu wa *veterinary specialist* hayuko tunategemea zaidi madaktari wetu wale walio-*qualify* katika kiwango cha *diploma*, ambapo wengi wao sasa hivi ni wazee na wanaelekea kustaafu.

Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa kufanya majumuisho nadhani angetueleza kwamba ni mkakati gani ameuandaa ili kuweza kupata *specialist* pale Pemba katika masuala haya ya Tiba za Mifugo.

Halikadhalika Mhe. Spika, kuna hawa madaktari tulionao wa stashahada wanafanya kazi katika mazingira magumu mno, kuna uwezekano wa hawa kuambukizwa na maradhi ya wanyama pale wanapotibu kutokana na ukosefu wa vifaa vya uhakika katika kufanya kazi zao. Sasa nadhani Mhe. Waziri atueleze mkakati wa wizara yake ili la kuweza kuwapatia wataalamu wale vifaa vya uhakika. Ng'ombe unaweza kumfanyia *artificial examination* unaingia hata yale ma-*gloves* huna unalazimika kuingiza mikono peku peku jambo ambalo ni tatizo. Sasa mimi nadhani angetusaidia hapa waziri, ana mkakati gani wa kuweza kuwasaidia wale jamaa pale kusudi waweze kufanya kazi katika mazingira ya uhakika sio katika kujaribu na kubahatisha afya zao.

Aidha, Mhe. Waziri atueleze je, hawa madaktari wetu wanaofanya kazi katika mazingira magumu kwenda kutibu *smallpox* kwenye kuku, maradhi ya uti wa mgongo kwenye ng'ombe, mafua ya ng'ombe na kitu gani, hawa wanapata *risk allowance*? Kwa sababu uwezekano wa kusambaziwa maradhi hawa madaktari wetu wa mifugo ni kubwa.

Sasa yeye atueleze hapa Mhe. Waziri kweli anawapa *risk allowance*, kama hawapi basi ni tatizo na ajitahidi wafanye mkakati wa kuweza kuwapa kitu kama hiki. Kwa sababu wenzao katika tiba za binadamu wale wanaofanya katika mionzi wanapewa *radiation allowance* na kadhalika na kadhalika. Sasa na huku nadhani haitakuwa dhambi hata kidogo kama na hawa wanaotibu wanyama kwamba watawapa na wao hizi *risk allowance.*

Mhe. Spika, jambo jengine ni katika suala zima la ufugaji. Wengi wetu na mimi binafsi ni mdau katika masuala haya, lakini inasikitisha sana kwamba dawa tunazopewa hizi za kuzuia maradhi hasa yale ya mahepe katika kuku kwa Uswahilini tunayaita 'Magwa' unakuwa na kuku 1000, 1500, 2000 wanapukutika kama uyoga na huku ushapewa dawa za kuzuia mahepe. Sasa dawa hizi jamani waziri tunataka utwambie hazina nguvu tena au sijui vipi. Tunaomba utueleze kama zimeshapitwa na wakati au maradhi sasa hayasikii dawa tujue upande mwengine wa kuelekea tuache kwenye mifugo. Kwa sababu tunateketea vibaya kwa mahepe yanapotushika, kuku wanapukutika sana.

Katika hili Mhe. Spika, kule katika vijiji tungepata ile huduma ya *outreach service, mobile clinic* wanatoa kule kwenye afya ya binadamu. Sasa na kule kwetu kungekuwa na madaktari kama wale wakawa wanakuja vijijini kuangalia mifugo yetu. Hivi ninavyokwambia Mhe. Spika, kuna matatizo katika jimbo langu la Wawi mara nyingi sisi wafugaji ng'ombe tunapata tatizo, ng'ombe anapata ugonjwa ule wa kuvimba kiwele, ukienda ukimkama badala ya kupata maziwa unapata damu.

Sasa sijui ni lini Mhe. Waziri katika hili atatuletea wataalamu ili waweze kuja kukagua mifugo yetu na hatimaye ile dhana ya serikali ya kupunguza umasikini iondoke. Kwa sababu serikali haiwezi kutuajiri sote lazima wengine tujiajiri wenyewe, leo tushafuga ng'ombe mpaka tunategemea kuvuna maziwa ng'ombe unakwenda amevimba kiwele unakwenda kukamua kumbe ni damu. Sasa mimi nadhani hili ni tatizo na umasikini hauwezi kutuondoka hapo na

tunaiomba wizara yako itueleze itatusaidia nini katika hili kusudi na sisi tuweze kujikwamua na kujiondosha katika umasikini na hatimaye kuongeza kipato

Nashukuru kwamba huu mchango wangu Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri pale anaufuatilia kwa kina sana hii ni dalili ya kutatuliwa tatizo hili.

Mhe. Spika, niende katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, hii wizara kwa kweli imesibu waziri anajitahidi katika hili la kutumikia wananchi katika misingi ya umakini wa hali ya juu na ndio anatuonesha utumishi uliotukuka mno. Kwa hivyo, kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi nampongeza sana Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora anatupatia utumishi tunaouhitaji, yaani ulio makini, mahiri, adilifu na wenye kutukuka mno.

Sasa niende katika mchango wangu Mhe. Spika. Katika hili kwanza mimi nataka nizungumzie Mfuko wa JK na AK, huu Mfuko kwa kiasi fulani unanipa wasi wasi, kwanza upatikanaji wake. Nashukuru wakati anawasilisha pale Mhe. Waziri wanataka kuuhamisha katika kujibu huku vile vile wanataka kuuhamisha kutoka *PBZ* na kuupeleka katika kitengo fulani kwenye ofisi yake. Hili kwanza napongeza kutoka pale *PBZ*. Tatizo la Mfuko huu nadhani hakuna vigezo katika kutoa kwake watu wanapewa tu na wala katika kupewa hawaangalii kwamba kiasi fulani tutatoa katika Mkoa wa Kusini na kiasi fulani tutatoa Mkoa wa Kaskazini, unamiminwa tu kiasi ambacho maeneo mengine yanakosa.

Mhe. Spika, nataka tuelewe kwamba Mfuko huu wa AK na JK ni Mfuko uliotolewa na marais wetu, lakini umepatikana kupitia kodi za walipa kodi wa nchi hii bila ya kujali eneo analotoka au mkoa. Kwa hivyo kila mtu anatakiwa anufaike na huu Mfuko.

Mhe. Spika, kuna maeneo hatupati Mfuko huu. Mimi pale Wilaya yangu ya Chake Chake pale na katika Jimbo langu la Wawi kuna watu wana kikundi chao kinachozalisha sana masuala ya uvuvi, viwanda vya mbao wameomba Mfuko huo wakiongozwa na kijana mmoja anaitwa Suleiman Mwachawa, wameomba mfuko huu karibu mwaka wa pili barua yao iko *PBZ* hawajapata jibu lolote, wenzao wanachukua na kuchukua wao hawapewi, ni kwa sababu gani ya msingi ambapo wale vijana wanazalisha sana. Sasa mimi naomba lile kundi la kina Mwachawa pale na wao ndio Wazanzibari wapewe na wanazalisha tunawaona mimi najua zile biashara zao pale wanajitahidi.

Halafu katika Jimbo langu la Wawi kuna vijana waliomba Mfuko huu wakaambiwa kuna asilimia 10 ya *interest* waengeze, watu wa *PBZ* wakamwambia aa, ni asilimia 25 *interest* yake. Sasa mimi jana tu wamenilalamikia na document wanazo hao vijana, wamenifuata hapa niko kwenye Baraza wamekatwa 25% wakati mwanzo waliambiwa ni 10% nataka leo waziri utwambie hapa, *interest* ya Mfuko huu ni kiasi gani tusiwanyanyase, wale walichukua mkopo wakaona watalipa *interest* asilimia 10, PBZ wakaambiwa walipe 25%. Sasa leo tueleze kusudi kama PBZ wamewalipisha 25% wale watu wangu wa pale Mji wa chini pale Wawi basi hizi 15% niende nikawasaidie kudai PBZ. Hilojengine.

Mhe. Spika, twende katika suala zima la mambo ya michezo na burudani. Kwanza nataka serikali ifahamu kwamba Timu ya Taita ya Jamhuri ya Muungano ni timu ya Tanzania nzima.

Inasikitisha sana pamoja na kwamba tuna kocha kutoka nje ya nchi lakini ile *bench* ya ufundi pale ilikuwa wawepo Wazanzibari na sisi tuna watu makini sana katika mambo ya mipira. Hapa tuna watu makini kama vile kina Salihina, Ali Bushiri, wana utaalamu mkubwa sana, Mhe. Waziri anieleze kwa nini katika *bench* ya ufundi ya *TFF* ni Wazanzibari wangapi waliopo pale. Hilo moja.

Jengine Mhe. Spika, hata ile Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatakiwa ienee. Mimi najua watasema kwamba wanachagua kwa mujibu wa kiwango, lakini kama kuna watu wanajua kulisakata soka vijana wetu wanajua kulisakata soka sawa sawa hapa.

Juzi juzi hapa walipata nafasi ya tatu katika Kombe la Kagame je, nyinyi mliwazawadia nini wale vijana. Hilo alijibu hapo kwanza. Halafu jengine anambie kwamba ni kiwango gani kinachoatumia kupata Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano, ikiwa ni kigezo cha wachejaji hapa tunao wazuri tu, Nadil Haroub Canavaro, Nassor (Cholo), wanaweza kucheza kabumbu kweli kweli.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana nakushukuru kunipatia nafasi hii na naomba nikae. Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii leo kwa kuweza kuchangia hasa hii Kamati yangu ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu katujaalia Kisiwa chetu cha Unguja kina utajiri mkubwa sana wa bahati na ndio nishati yetu aliyotujaalia Mwenyezi Mungu tunayoitumia kwa sote.

Mhe. Spika, naanza katika Huduma ya Uvuvi. Serikali yetu imeweka Wizara nzima ya Mifugo na Uvuvi, nampa hongera Mhe. Rais kwa kutchagulia mawaziri ambao wana juhudi kubwa sana na mahiri kwa kufanya kazi. Huduma ya uvuvi ndio huduma iliyotawala kwetu, lakini bado hatujitumia kutokana na ile hali ya kuweka uchumi wetu katika huduma za uvuvi. Kwa sababu wananchi wetu wengi ni masikini kutokana na huu uvuvi wa kizamani. Ningeliiomba serikali iwape wavuvi wetu huduma za zana za kileo ili tuvue samaki tuepukane na umasikini, kwa sababu nchi yetu ni nchi iliyozungukwa na bahari, lakini ajabu leo hata samaki wa kibati hatuna.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iwape wananchi wavuvi ambao wanatumia bahari ya Zanzibar zana za kileo ili tupate samaki kwa wingi. Samaki tunao lakini hatuna zana za kuvulia Mhe. Spika. Sasa naiomba wizara ifanye juhudi iwame zana wananchi wapate huduma na watafutiwe soko la kuuza samaki, vijengwe viwanda vya kusindikia samaki, samaki tunao kwa wingi, vijana wetu wanakosa ajira kwa sababu hakuna viwanda vya kuhudumia samaki.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika imeweka *Sunday Market*, lakini *Sunday market* huwezi kuona samaki wa kibati na bahari tunayo, tumezungukwa na mkono wa bahari vipi leo *Sunday market* haina samaki wa kibati. Naiomba serikali itoe zana iwape wananchi, iwape vijana wafanye kazi waitumie bahari, bahari ya Zanzibar ina samaki wengi sana leo ajabu wanatoka watu wa nje wanakuja kuvua samaki hapa kwetu na sisi ndio petu, sisi ndio bahari yetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naiomba serikali itoe zana.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye huduma ya mwani. Mwani ni zao la pili baada ya karafuu na mwani ni huduma inayofanywa na akinamama, leo akinamama wanafanya kazi kubwa lakini kipato chao kidogo. Kwa hivyo, naiomba wizara iwafikirie kinamama wanaofunga mwani hasa kule katika jimbo langu la Matemwe sasa hivi kina mama wengi sana wanafunga mwani na ndio kazi yao na ndiko kunakotoka mwani mwingi kuliko kokote kwa Unguja hii. Kwa hivyo, wizara iwafikirie wafunga mwani bei wanayopewa ni ndogo Mhe. Spika, kulingana na kazi kubwa ya bahari.

Mhe. Spika, nakwenda katika mifugo. Mifugo tunayo lakini mifugo tuliokuwanayo inadhoofika haina huduma za madawa, mifugo wanayopewa wananchi ni kidogo, mwananchi anapewa ng'ombe watatu, ng'ombe watatu wanapewa watu 20 wanaambiwa kikundi cha ushirika. Hivyo naiomba wizara iwafikirie wafugaji kuwapa ng'ombe wa uhakika na wapewe huduma za madawa ili wapate kufanya kazi. Madawa yanakuwa hayatoshelezi kwa kuwafugia wanyama hao, wanyama wanakufa ovyo, wale wafugaji kuku ukienda katika vikundi vya ushirika wanakwambia sasa hivi sisi madawa hatuna kuku wetu wamekufa. Sasa niiombe wizara ifanye kila jitihada iwapelekee madawa wafugaji.

Mhe. Spika, nije katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo katika sehemu ya magofu. Magofu ni katika sehemu moja inayovutia utalii, lakini bado serikali haijaweza kuhifadhi magofu Unguja na Pemba. Kuna sehemu moja tumetembelea Pemba kuinaitwa kwa Mkamandume, ni mahala ambako kuna historia kubwa na kunaweza kutia fedha nyingi, lakini bado kumetupwa hata kuhifadhiwa hakujahifadhiwa, hakujajengwa hasa kukawekwa vizuri kuwa hapa ni pahala pa kuvutia watalii wakenda pale wakahakikisha hapa kweli pana historia ya zamani. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia wizara yake kwamba iwape uwezo wa kujenga magofu ya kuvutia.

Mhe. Spika, sasa nakwenda katika Wizara yangu mahiri ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Mhe. Spika, kwanza nampa pongezi Mhe. Waziri wa wizara hii kwa uwezeshaji, lakini bado namuomba Mhe. Waziri awaangalie vijana wangu hasa kule kwenye Jimbo la Matemwe bado hawajawezeshwa kiajira, bado hawajawezeshwa kivikundi. Lakini pia nampa pongezi kwamba kiko kikundi changu kimoja kimepata ruzuku ile inayoitwa Zakka kule Kijini, Matemwe. Hapo natoa pongezi. Kwa hivyo, naiomba wizara izidi kuwawezesha vijana.

Mhe. Spika, ili nisipoteze wakati wako mimi pamoja na wananchi wangu wa Jiombo la Matemwe naunga mkono maagizo yangu ya kamati hii ahsante sana nashukuru.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kupata nafasi hii fupi ya kutoa mchango wangu unaohusiana na Ripoti ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari inayofanyia kazi katika wizara tatu ikiwa ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Kwanza kabla ya yote nitoe pongezi zangu za dhati kwa hotuba nzuri iliyoandikwa na kamati hii na ikapata msomaji ambaye ndiye.

La pili Mhe. Spika, kwa kuanza moja kwa moja nianze na Wizara ya Habari na kwanza nianze kwa Hoteli ya Bwawani. Mhe. Spika, katika taarifa kutokana na agizo la kamati na utekelezaji wake ukurasa wa tano kifungu nambari nane kwa ruhusa yako naomba nisome unaeleza kama ifuatavyo:

Kifungu cha 8 kinaeleza hivi:-

> "Kwa vile Hoteli ya Bwawani ndio jicho la serikali yetu, kamati inaishauri wizara ifanye hima kurekebisha eneo lililomong'onyoka la ukingo wa Hoteli ya Bwawani, kwani kila wakichelewa nguvu za maji zinazidi kuteka eneo kubwa zaidi la ardhi".

Utekelezaji ni kuwa, eneo lililomong'onyoka ukingoni mwa Hoteli ya Bwawani tayari limeshashughulikiwa kwa kurejesha ukuta uliokuwepo unaozuwia maji ya bahari.

Mhe. Spika, mimi nilikwenda kuliona eneo hili na ni kweli ukuta umejengwa, lakini kuangalia ile sehemu yenyewe ilivyo na ukuta ule uliojengwa ambao zimetumika fedha nyingi sana na namna ulivyojengwa, kuna hatari ya hapo baadae ukaanguka kama ukuta uliokuwepo.

Kwa hivyo, ushauri wangu, zaidi ya kazi kubwa iliyofanywa kwa makusudi kuzuia mmong'onyoko huu, ningelishauri kazi nyengine ya ziada ya kusaidia zaidi itekelezwe, ikiwa ni pamoja na kutafuta wataalamu waliokuwa wanahusika na mambo ya ardhi kuangalia pale ni aina gani ya mikoko ipandwe na ipandwe kwa wingi ili izuwie mmong'onyoko. Vile vile ikiwezekana ni pamoja na kuweka mawe ya kutosha pembezoni mwa ukuta huo ili kuzuwia usibomoke kwa urahisi.

Mhe. Spika, jengine katika Hoteli ya Bwawani ni kuwa hoteli hii ndio hoteli ambayo sisi wenyewe tunaringia ni hoteli yetu ya historia, ni kubwa na yenye hadhi.

Lakini kwa taarifa tulizonazo ambazo sizakuaminika tunasikia tu kuna mpango ama hoteli ile kuuzwa au kuvunjwa kabisa na kujengwa hoteli nyengine ambayo kutokana na hali ilivyo ile hoteli hivi sasa pamoja na kuwa ina matatizo ya ufanisi katika kushughulikia, ningeliomba Mhe. Waziri aliyehusika atupe taarifa rasmi kuhusu hatma ya hoteli hii. Ni kweli itavunjwa, itauzwa, itakodishwa au itafanywa nini lakini ninasikia kwenda katika hali ile ilivyo haitokwenda tena.

Mhe. Spika, nikizungumza kuhusu wizara hii, eneo la hoteli kuna bwawa limeekwa kwa makusudi na kwa muda mrefu na limejaa maji ambalo halifanyi kazi isipokuwa labda kwa uono wangu mwenyewe ni kuzidi kuharibi mazingira. Mimi ninataka nielewe hatma ya bwawa lile lisilotumika kwa vyovyote ni ipi.

Mhe. Spika, wizara inahusiana na Chuo cha Maendeleo ya Utalii ambacho kipo Maruhubi. Kwanza nimpongeze mkuu wa chuo hiki kwa juhudi yake na tumekuwa pamoja katika safari nyingi na tumeona tuliporudi namna alivyogeuka na kukigeuza chuo kuwa ni chuo cha kisasa kabisa na *inshaa Allah* Mwenyezi Mungu ampe nguvu ya hivyo, lakini chuo kimo katika hatari kubwa sana ya kuliwa na mmomonyoko wa ardhi kwenye upande wake wa baharini.

Skuli imechukua hatua kubwa sana au imejitahidi sana kupambana na hali hii lakini hali ni mbaya zaidi na haipo katika uwezo wa skuli ile. Kutokana na hali ya mmomonyoko inavyokwenda kunatakiwa kufanywa utafiti wa kina na kazi kubwa ifanywe ili chuo kile kiweze kusalimika. Kwa hivyo ninaishauri serikali kwa kupitia wizara kuwa ione umuhimu wa chuo kile ambacho ni kimoja tu katika Zanzibar kutokana mmomonyoko ule wa ardhi na kisaidiwe ili kibakie katika hali iliyokusudiwa na kutoa huduma zake ipasavyo.

Jengine Mhe. Spika, kwa kumalizia kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwanza nitoe shukurani kwa hii wizara ina watu wasikivu sana kutokana na kazi kubwa waliyofanya kamati kwa kushirikiana na watendaji wa wizara, tumetoka kwenye analogue na hivi sasa tunaingia katika digital na tunaona mabadiliko yanayotokea, tokea kwenye kivazi mpaka kwenye matangazo.

Sasa Mhe. Spika, ninachotaka kujua kwa kuwa huko tunakotaka kwenda taarifa tuliyona ni kuwa vifaa vingi sana ambavyo ni vichakavu na uzoefu nilionao ni kuwa bajeti iliyopita ya wizara hii ilikuwa ni ndogo sana kupita kiasi, mbali ya zile pesa zilizokatwa kwa ununuzi wa meli. Halafu matangazo wamejipangia hawa kuendelea kwa masaa 24 ni gharama kubwa sana.

Sasa ili tuweze kuingia kwenye mtandao vilivyo ningeliomba kwa Mhe. Waziri akanipa maelekezo ya kina ni namna gani kajirekebisha kuweza kupata vifaa mbadala kwa kuondoa vile vichafu au vilivyochakaa na vipi matangazo yataweza kwenda kwa masaa 24 katika hali ambayo ni muafaka sio kutia vipindi kaseti za kutizama lakini ni pamoja na matangazo yale ya mazingira ili tuweze kufaidika vilivyo.

Lakini Mhe. Spika, kuna la mwisho kuhusu wizara hii, naomba nisikilizwe kwa makini na tena kwa makini sana. Mhe. Spika, sisi tunaipenda sana ZBC televisheni yetu na tunaiangalia sana na tunaifuatilia sana hotuba za viongozi wetu wakuu. Tunafarijika kwa namna watu wetu wanaochukua habari za mchanganyiko kwa kuweza kutoa maelekezo kama wanavyotoa.

Lakini Mhe. Spika, tukiangalia katika nchi nyengine hata hii nchi tuliyoungana nayo ya Tanzania Bara, Mhe. Rais anapozungumza huwa yupo peke pamoja na kuwa ana walinzi, ukenda nchi nyengine ndio kabisa utakuta Rais anakwenda peke yake anazungumza unamuona anavyotulia anavyotamba na kadhalika na kutoa maelezo ya kuvutia. Lakini siku zote kwetu sisi huku nyuma lazima kuna watu ambao wanazunguka.

Mimi nasema Mhe. Spika, tena ninasema kwa nia safi kwa maana ya kuboresha, hakuna utaalamu wa kupiga picha ikawa walinzi wale wapo lakini Mhe. Rais au kiongozi yeyote anapotoa hutoba kama zile shughuli muhimu akaonekana kama tunavyoona katika nchi nyengine. Naomba kumalizia hapo kwa wizara hiyo.

La pili Mhe. Spika, kwa ufupi ni Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kwanza nampongeza Waziri na watendaji wake kwa kupata wizara hii ngumu na kwa muda mfupi na kuonesha mabadiliko makubwa na nia ya kuwasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi.

Mhe. Spika, mimi kwanza hapa ninazungumzia kuhusu mfuko wa AK na JK. Ninavyojua kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa shilingi milioni mia sita na Rais Mstaafu wa Zanzibar alitoa shilingi milioni mia sita ikawa ni bilioni moja nukta mbili kwa kuanzisha mfuko huu wa AK na JK na zikapelekwa benki.

Benki wao ndio waliokuwa wakiangalia wanaotaka kusaidiwa wanaomba halafu wao wakatoa fedha hizi na kadhalika. Lakini kwa bahati mbaya fedha hazikurejeshwa ipasavyo na ilikuwa zirejeshwe ili waweze kusaidiwa na vikundi vyengine waweze kujiendeleza.

Sasa kutokana na maelezo tuliyopata ni kuwa katika ufunguzi wa mfuko huu uliotolewa juzi wa Zakka, Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kule Hoteli ya Bwawani alisema kuwa au alielekeza kuwa mifuko yote iwekwe katika sehemu moja ili itumike ipasavyo na kuweza kuweka kumbukumbu sahihi.

Lakini katika utekelezaji wa suala hili kwa sababu kamati nayo imetoa maelekezo kama hayo, wizara imesema kuwa suala hili limeshajadiliwa na pande zote zinazohusika *PBZ* kupitia bodi yao wameridhia na sasa tunasubiri kukamilisha makubaliano kati ya wizara inayohusika na masuala ya fedha na Benki Kuu ya Tanzania.

Hapa ningetaka nielezwe kwa nini ikawa lazima kuingizwa katika Benki Kuu ya Tanzania wakati tunajua mfuko huu ulikuwa katika Benki ya Watu wa Zanzibar, na hiyo wizara inayohusika ni wizara ipi; Wizara ya Fedha ya Muungano au ni hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika: Unazo dakika 5 Mhe. Mjumbe.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kama ni dakika 5 moja kwa moja naingia kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Spika, wizara hii ambayo ndio wizara inayoleta vitoweo ina kazi kubwa sana na ni muhimu kwetu sisi. Kazi wanayofanya ni ya kitaalamu. Wanafanya kazi ya kuzalisha, ya kubadilisha mbegu, wanafanya kazi ya kulea na kadhalika.

Sasa Mhe. Spika, mimi katika wizara hii pamoja na kuwa dakika ni chache, kwa hivyo kwa ufupi tu naomba kueleza yafuatayo.

Kwanza Mhe. Spika, wizara kwa makusudi kabisa imehimiza wananchi kujiunga katika vikundi na kufuga samaki na kuchimbwa mabwawa. Mabwawa mengi yamechimbwa baadhi wamefanikiwa lakini wengine wameshindwa kufanikiwa kutokana na kazi kuwa ni ngumu sana na baadae wakahitaji fedha kwa vifaa vyengine ikashindikana.

Kwa hivyo mimi ushauri wangu kwanza Mhe. Spika, kwa hawa watu wanaofuga samaki ambao watatusaidia sana, kabla ya kuchimba mabwawa yao ningeliiomba wizara kikamilifu kufanya utaratibu ambao wale watu ni lazima waombe ruhusa kutokana na wizara inayohusika na mazingira pale mahali pakaangaliwe pia wapewe taaluma ni samaki gani wanafaa katika kufungwa pale sio kila samaki anaweza kuishi na halafu pia tuwe tumejipanga watakapokwama

kwa mambo mazito majembe, mapauro, mashine ya kuvutia maji na kadhalika waweze kusaidiwa, nguvu tupu tu inaweza ikafanya mambo haya yakarudisha maendeleo.

Halafu kwa upande wa kuku Mhe. Spika, ninashukuru wizara kwa kuweza kuweka mbegu zetu za asili ziwepo na vile vile kutafuta machotara kwa kutumia mbegu za kigeni.

Halafu Mhe. Spika, mimi jambo ambalo nimeshuhudia ni kuwa wafugaji wetu wanapofanya kazi hii ya kufuga na wakapata mazao, kwa bahati mbaya huwa wengi wanakosa mazao kwa kuyauza. Kwa sababu mbili. Kwanza uzalishaji unakuwa ni mkubwa kuliko mahitaji na la pili kuingiliwa na bidhaa kama ile kutoka nchi za nje ambayo bei yake ni ndogo sana.

Sasa zaidi ya huu ushauri ambao wenzetu hawa walioufanya kwa kusema kuwa tutaondoa kodi kule ili bidhaa ziwe rahisi na wao waweze kuingia kwenye competition. Mhe. Spika, haoni Mhe. Waziri kwamba ipo haja ya hivi sasa kwa makusudi na kwa vile tuna ufugaji wa ng'ombe katika hali hiyo hiyo, wakashirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa makusudi hasa pakawa na viwanda vinavyohusika na usindikaji wa nyama hizi na vile vile wakaanza kutafuta mahala ambapo patakuwa na soko la kutosha ili wasiweze kuvunjika moyo.

Halafu jengine ambalo nimeliona na naomba nilieleze Mhe. Spika, ni kuwa sisi tumebahatika tunao mtambo wetu unaotoa *liquid nitrogen* na ni jambo ambalo tukilitafuta kwa muda mrefu, na ina uwezo wa kutoa nitrogen ya ziada na tena tunaweza kufanya hayo mambo yetu ya kuzalisha bila ya matatizo.

Jee, kulikuwa kuna ulazima gani hivi sasa kuagiza machotara kutoka Bara wakaletwa hapa wakati mbegu tunazo nzuri pale Maruhubi na badala yake fedha yote ile ikatumika kwa kufanya namna ambayo ule uzalishaji uliopo pale Maruhubi na Pemba tukaweza kufanya; yaani kuwepo na mtambo kama ule kama ikiwezekana au japo ikiwa hakuna mtambo wa liquid nitrogen lakini mambo mengine yale yote yanayohusiana na pale Maruhubi yanahusiana na upandishaji wa ng'ombe yaweze kufanywa kwa urahisi zaidi.

Mhe. Spika: Haya muda.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: la mwisho Mhe. Spika, ambalo ninapenda kuzungumza ni kutokana na muda ulivyo. Hapa kuna ufugaji wa mwani hapa na ufugaji wa mwani hauna season ya kuvunwa kila siku mwani unavunwa. Ufugaji wa mwani ni lazima mwani uanikwe na ili mwani uwe na thamani ni lazima upate jua ukauke. Mwani ukipata mvua unaharibika.

Nimetembea katika mvua hivi karibuni wenzetu wafugaji wa mwani walipata hasara kubwa sana. Tulipendekeza kwamba ifanye kila inavyowezekana ili kuwepo alau kiwanda kimoja cha kukaushia mwani; kimoja Unguja na kimoja Pemba. Lakini katika ripoti hii sikuwa lolote. Kwa kuwasaidia wakulima wetu wa mwani kwa sababu ya mvua, wizara ina mpango gani.

Mhe. Spika, nakushukuru.
Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nichangie hotuba hii ya ripoti ya Kamati ya Habari. Na kama nilivyokuomba sitochukua muda mrefu sana ili niweze kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wajumbe wenzangu.

Mhe. Spika, mimi nianze na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na nianze na mchango mzima wa nafasi kwa vyombo vya habari duniani. Mhe. Spika, duniani watu wanafikia vyombo vya habari kuwa ni muhimili wa nne wa dola. Tofauti sana na mtizamo na mwelekeo wa Serikali yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza naomba nitoe lawama kubwa kwa redio, *TV* na magazeti yetu ya Zanzibar Leo, kwamba pamoja na kuwa Baraza hili limeanza tarehe 3/04/2013, matarajio ya Wazanzibari kwamba magazeti yetu yaandike yale mambo ambayo yanatokeze humu ndani sana. Kwa mfano jana Mhe. Spika, licha ya kuwa kulikuwa na ripoti ya *PAC* lakini ukiangalia vyombo vya habari vilivyoripoti ni sehemu ndogo sana, wameona bora kuripoti kuna nyoka amekwama na chura ni habari muhimu kwao, kuliko kuripoti habari ya *PAC* Barazani kwa ajili ya maslahi ya watu.

Sasa ninavunjika moyo sana kwa kuona kwamba kweli sisi tupo makini kuwasaidia hawa kujenga hoja kwamba wapewe pesa zaidi. Ninadhani Mhe. Spika, vyombo vya habari bado vinafanya kazi katika mazingira ya woga. Lazima tuwajengee msimamo tuwatoe hofu kwamba wafanya kazi katika mazingira ya kujiamini na watambue kwamba wao ni sehemu ya jamii na sehemu ya muhimili wa dola katika dunia.

Mhe. Spika, udhaifu uliopo katika *ZBC* televisheni unasikitisha kwamba hivi tunavyozungumza matangazo ya televisheni baada ya kurushwa moja kwa moja kutoka *ZBC TV*, inaunganishwa na *Cable Television* ndio wanapewa wananchi wa Zanzibar. Kwa nini eti kwa sababu *transmission* tumempa *AGAPE*. Maana yake *AGAPE* sasa hivi imekuwa ndio sehemu hivi sasa ya *ZBC* jambo ambalo serikali imetenga mamilioni ya pesa kumpa mkandarasi huyu kwa ajili ya kutuwezesha katika mfumo huu wa *digital*.

Mhe. Spika, huu ni udhaifu. Leo Wapemba kule Pemba hawapati matangazo ya televisheni jambo ambalo ni ukiukwaji wa Katiba na ukiukwaji wa maazimio ya kimataifa. Sasa Mhe. Spika, naomba Mhe.Waziri atueleze kwa nini mumechukue Kampuni ya *AGAPE* lakini imeshindwa kurusha matangazo ya moja kwa moja na badala yake munachukua vifaa vya *ZBC TV* ndio wanavyotumia katika maslahi hayo, huku ikiwa mumempa zaidi ya dola milioni tatu kwa ajili ya shughuli hiyo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nikizungumzia suala jengine Mhe.Waziri atueleze hivi sasa dunia ipo katika mfumo wa *digital*. Zanzibar tupo wapi, tupo *digital*, *analogy* au tupo kati kati. Mimi naona hatupo popote, hatupo *digital*, *analogy*, tupo wapi atwambie sasa. Hatupo huko ni kwa sababu tumeshindwa kusimamia. Mhe. Spika, tufike pahala paambizane ukweli, tupo wapi.

Leo ukiangalia televisheni dakika tano macho unayapofua, mtikisiko kama vile bahari mawimbi, tupo wapi; tupo *digital* au analogue au tupo kati kati. Nadhani ikiwa tukiwa kati kati nani mtaalamu wetu anayefika hapo.

Mhe. Spika, nimalizie kwa hoja hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, nimuombe Mhe. Waziri kwamba tumekuwa tukizoea wafanyakazi wetu wa *TV* na redio hapa Barazani ambao ni waandishi wa habari maposho yao hawalipwi mpaka pengine kikao chengine kijacho. Posho la mwezi wa Januari Mhe. Spika, wamelipwa juzi. Si utaratibu mzuri.

Posho hili la leo Mhe. Spika, nina hakika watalipwa mwezi wa sita, si utaratibu mzuri. Mhe. Waziri nikuombe kwamba bajeti hii ndio inaandaliwa bajeti mpya, utupangie posho la waandishi wetu wa habari kwa maana ya redio, televisheni na gazeti, wakimaliza kazi jioni uwape pesa yao, ndio utaratibu ulivyo.

Tabia ya kuwawekea kwenye sanduku bubu mpaka miezi minne si utaratibu mzuri. Mhe. Spika, wale waliobahatika kuwa katika Kamati ya Habari wahakikishe kwamba bajeti ya wizara hii, posho la waandishi wa habari, televisheni, redio na gazeti wapewe hapo kwa hapo na wasiekewe mwisho wa mwaka si utaratibu mzuri.

Nimalizie mchango wangu kwa kumuomba sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, hivi karibuni alituomba tupeleke vikundi vya ushirika kila jimbo vikundi viwili. Bahati nzuri wawakilishi wote walipeleka barua zile mkono kwa mkono mbele ya ofisi ya Waziri. Katika ugawaji wa fedha ile hasa Pemba ambapo nina ushahidi nako, ofisi za Wilaya ziliingia kati na vikundi vile fedha hawakuzipata ipasavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ninataka utupe maelezo kwa nini ulipotaka kutupa vikundi sisi ndio uliotuomba vikundi, lakini ugawaji ukawaachia watu hatimaye fedha ile imepotea mikononi mwa watu. Mhe. Spika, nina ushahidi kuwa baadhi ya vikundi serikali imetenga kutoa shilingi milioni mbili, kuna vikundi vimepewa shilingi milioni moja. Tuambie pesa ile imekwenda wapi katika mikono ya watu.

Mhe.Spika, baada ya hayo Mhe. Waziri atatwambia tupo wapi, kama tupo *digital* au analogue ninaunga mkono hii hoja. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe.Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nguvu ya kusimama kwenye chombo hiki kwa kutetea wananchi wa Zanzibar, naomba nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache katika hoja hii ya ripoti ya Kamati ya Mifugo, Uwezeshaji, Utalii na Kazi.

Mhe. Spika, naomba niipongeze kamati kwa ripoti yao nzuri na vile vile niwapongeze mawaziri wote watatu kwa jinsi ambavyo wameleta ripoti zao za utekelezaji zikiwa na maelezo ya kina. Mhe. Spika, yapo maeneo machache ambayo ningependa kupata maelezo kidogo.

Naomba nianze na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Hapa Mhe. Spika, nina hoja moja tu. Mhe. Spika, katika ripoti hii ya utekelezaji kwenye kifungu nambari 4, “Katika jitihada za kupunguza unyanyasaji wa waajiria hasa wa sekta binafsi kamati imeshauri wizara kuwapa taarifa ya moja kwa moja wafanyakazi kupitia wilaya zao kila inapofanywa marekebisho ya mishahara”. Na katika maelezo imesemwa hapa kwamba hatua za kutoa taarifa kwa wafanyakazi juu ya marekebisho ya mishahara katika sekta binafsi imefanyika.

Mhe. Spika, mimi nimeamua kutumia nukta hii kuunganishia suala ambalo Mhe. Waziri atakumbuka nililileta hapa, nadhani kama sikosei kama mara tatu. Suala la wafanyakazi wa *ZANTEL*. *ZANTEL* Mhe. Spika, ni kampuni ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa,

kwa hivyo ni sehemu ya wamiliki. Lakini vile vile ina sehemu ambayo inamilikiwa na kampuni binafsi ya *Etisalat*, ambayo imeambiwa imeingia mkataba na serikali.

Hoja ambayo Mhe. Spika, ilikuwa inahusu maslahi ya wafanyakazi hasa vijana watoto wa Kizanzibari ambao wameajiriwa katika kampuni ile. Mhe.Spika, atakumbuka nilizungumzia hasa maeneo mawili. Kwanza walinzi walioajiriwa kulinda katika minara ya *ZANTEL* na sehemu mbali mbali ambao wapo Zanzibar, lakini vile vile vijana ambao wanafanya kazi katika ile *core centre*, kwa maana ya *customer care* na vitu vyengine kama vile ambavyo wananchi wanapopiga kutaka kusaidiwa wanapiga pale.

Hoja niliyoileta Mhe. Spika, ilikuwa kwamba malipo ambayo yanalipwa na kampuni hii moja ambayo makao makuu yake yalipaswa yawepo hapa Zanzibar ambayo Serikali ya Zanzibar ina hisa, lakini wanavyolipwa walioajiriwa Tanganyika, wanalipwa tofauti na wale ambao wameajiriwa Zanzibar.

Mhe. Waziri akaniahidi kuwa atalifanyia kazi na tulikuwa tunawasiliana muda mrefu lakini ninasikitika kumwambia kuwa karibuni kilichofanyika ni kwamba walinzi hasa walio wengi wamefukuzwa kazi na kwa vitisho, kwamba wamepewa fedha fulani wameambiwa kwamba hizi ni za kuondoka nazo kama ni shilingi laki saba au laki tano wala hakuna sababu inayoeleweka. Ukitaka chukua na kama huchukui hizi utazikosa na wala hakuna kuendelea na kazi hapa.

Sasa Mhe. Spika, nimepata matatizo kwamba badala ya kurundikiwa maslahi yao, ile kuja kuwatetea Waziri imeonekana ndio sababu ya wao kufukuzwa kazi. Lakini hata yale marekebisho ya mishahara kwa wale ambao wanaofanya kazi katika kile kitengo cha kupokea malalamiko mbali mbali ya wananchi ambayo ni kazi nzito Mhe. Spika, kwa sababu kwanza kiafaya itawaathiri kwa sababu inabidi kuvaa yale ma-*speaker* na madude mengine wakati wote kusikiliza wateja. Bado hakuna viwango vinavyolingana Mhe. Spika, palifanyika marekebisho madogo lakini bado hakuna uwiano.

Sasa Mhe. Spika, tunashangaa kazi ni ile ile moja. Katika nchi inayoitwa Jamhuri ya Muungano, vipi hawa walipwe tofauti na hawa na hasa ukizingatia kampuni hii Serikali ya Zanzibar ina hisa na ingepaswa kwanza kuwalinda Wazanzibari kabla ya watu wengine wowote. Mhe. Spika, naomba maelezo kwa Mhe. Waziri juu ya suala hili kwa sababu ninajua alikuwa akilifuatilia binafsi yeye mwenyewe na sio kwa kutuma watu wake.

La pili Mhe. Spika, naomba niende kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Katika wizara hii Mhe. Spika, naomba maelezo katika nukta mbili. Nukta ya kwanza huu waraka wao wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi umegawika katika sehemu mbili humu. Maana yake kuna sehemu ya kwanza inaanza nambari moja mpaka nambari ishirini, halafu yale mambo mengine yameandikwa mambo muhimu na ahadi za wizara pia imeanza nambari moja mpaka nambari gani.

Katika hii sehemu ya kwanza naomba maelezo katika kifungu nambari 6 na kinasomeka hivi Mhe. Spikia, “Wizara ya Mifugo na Uvuvi iangalie mikataba na makubaliano ya uvuvi wa bahari kuu yaliyofikiwa kwa mtazamo wa mbele ili kuepusha Zanzibar na maafa yanayoweza kuepukika”. Maelezo ya utekelezaji Mhe. Spika, yanasema, “Mikataba ya uvuvi wa bahari kuu

ipo katika mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu Serikali imeichunguza mikataba hiyo na kuona yapo mapungufu ya kisheria na hivi sasa yanafanyiwa marekebisho".

Mhe. Spika, haya maelezo kwa mtu ambaye si mtendaji wa wizara hii haelewi kitu hapa. Nilikuwa nilikuwa ninadhani tusaidiwe hapa labda atakapokuja Mhe.Waziri kutoa majumuisho atusaidie, haya mapungufu ya kisheria ni yepi na yanafanyiwa marekebisho ni yepi. Hebu tupewe maelezo kwa sababu hili suala Mhe. Spika, lina maslahi yetu kwa sababu pia linahusu upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano kwamba haidhuru uvuvi sio suala la muungano, yalipitishwa makubaliano kwamba yaendeshwe kwa pamoja na maslahi yetu yawe yanalindwa. Kwa hivyo ndio nilikuwa nataka maelezo juu ya eneo hili.

Jengine Mhe. Spika, katika eneo hili la pili lipo katika yale mambo muhimu na ahadi za Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Katika vifungu nambari 1 na nambari 2, kuna masuala yanayohusu mashamba ambayo yameelezwa kwamba yamechukuliwa.

Kifungu nambari moja kinasema, "Wizara ifuatilie shamba la Tunguu lenye ukubwa wa ekari 1000 ambalo limeelezwa kuwa limerejeshwa ardhi", na kifungu nambari mbili kinasema, "Wizara ifuatilie shamba la Kitumba ambalo wananchi wametakiwa wahame bila ya maelezo yanayotosheleza".

Sasa ukija kwenye utekelezaji Mhe. Spika, yanasema, "Shamba limechukuliwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na maeneo yake yamepewa taasisi tofauti za kiserikali na zisizo za kiserikali kwa ajili ya kuendeleza shughuli mbali mbali". Hili la Tunguu la ekari 1000 Mhe.Spika, nilikuwa naomba nisaidiwe hizi taasisi za serikali na zisizo za kiserikali ambazo zimepewa eneo hili ni zipi na zimepewa kufanya shughuli zipi. Naomba maelezo kwa sababu lile eneo ni kubwa sana Mhe. Spika, ekari 1000. Maelezo kama haya tu hayatoshelezi kwa wawakilishi wa wananchi ambao wameletwa hapa kwa kuja kuisimamia serikali.

Lakini la pili katika hili la Kitumba Mhe. Spika, vile vile imesema kwamba shamba hili ni mali ya serikali, ufugaji wa mbuzi wa serikali katika shamba la Kitumba unaendelea, sehemu ya shamba hili limechukuliwa na JWTZ na wavamizi wengine. Hii maana yake pia ni wavamizi; wao na wavamizi wengine.

Wizara imeanzisha mazungumzo na JWTZ na wavamizi wengine ili waondoke. Sasa mtu kavamia Mhe.Spika, halafu unakwenda kumpembejea aondoke au kwa sababu ndio jeshi labda imekuwa *above the law*, lipo juu ya sheria inapembejewa. Tunataka maelezo ya kina Mhe. Spika.

Haya kama ni mashamba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tuwaambiwe kwa nini yanachukuliwa na kugaiwa ovyo ovyo kama hivyo. Nilikuwa naomba maelezo Mhe. Spika, katika hili.

Naomba niondoke katika wizara hii Mhe. Spika, sasa niende katika Wizara ya mwisho Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Spika, kwenye wizara hii mimi nimepata mashaka bwana! pamoja na pongezi nilizotoa maelezo ya kina lakini vipo vifungu vimenitia mashaka.

Cha kwanza ni agizo la nambari 19 Mhe. Spika, agizo hili linasema ambalo linahusu kesi hizi ambazo zinaripotiwa kwa watalii wanapotembelea nchini wakafanya makosa. Inasema, "Wizara izitumie fursa za kisheria kwa watalii waliohusishwa na kesi mbali mbali nchini kwa kuzingatia kesi hizo kwenye *first track case* ili ziweze kusikilizwa haraka kabla ya watalii hao kuondoka.

Maelezo Mhe. Spika, yaliyotolewa, "Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii inafahamu kuwepo kwa fursa hizo za kisheria katika kushughulikia kesi za watalii katika mkondo wa *first track* na tayari imetumia fursa hizo, changamoto inayojichomoza ni pale watalii wanapolazimisha kuondoka mara baada ya tukio", Mhe. Spika, haya maelezo yamenishtua kweli kweli.

Ina maana tunakuwa na mgeni anavunja sheria katika nchi yetu, anakuwa na kesi halafu yeye anachagiza kuondoka na wizara inaturipotia hivi kwamba changamoto iliyokuwepo kuwa wageni hawa au watalii wanalazimisha kuondoka.

Mhe. Spika, kama mtu kafanya kosa katika nchi yetu lazima, kwanza ni lazima awekwe katika vyombo vya sheria na lazima a-*face the law*, ni lazima apambane na mkono wa sheria. Mhe. Spika, kuna kesi maarufu, nafikiri watakuwa wanaikumbuka hapa wenzangu. Katika Umoja wa Falme za Kiarabu Dubai, kulitokea watalii ambao walifanya mapenzi kwenye fukwe, ikaripotiwa dunia nzima na nchi yao ikajaribu kuingilia kati kwamba waachiwe. Lakini hata nchi ambayo milango yake iko wazi sana kwa wageni kama Umoja wa Falme za Kiarabu, haikukubali mpaka watu wale wakafikishwa katika vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua.

Sasa hapa wizara ilipokuja kuturipotia kwamba watalii wanalazimisha kuondoka. Mimi najiuliza Mhe. Spika, kwamba hivi tunafanya kazi kwa kuwapembejea watalii kiasi hiki kama mtu anavunja sheria halafu anataka kuondoka na sisi tunamuogopa. Nilikuwa naomba maelezo katika hilo Mhe. Spika.

Suala la pili Mhe. Spika, ni agizo nambari 28. Agizo hili linahusu michezo na suala zima la michezo sio suala la Muungano, lakini Zanzibar inashindwa kufaidika na fursa hizo kwa sababu inaambiwa haitambulikani kama ni nchi. Pametajwa hapa mpira wa miguu kupitia shirikisho la *FIFA*. Lakini vile vile na michezo mingine.

Mhe. Spika, katika hili mimi naomba niseme moja tu kwamba serikali katika hili ijifunze, kuwa katika muundo huu wa Muungano haya matatizo hayatatuki. Kwa sababu hili hata ukifanya vipi litabakia hivi hivi, ni lazima Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ije ituambie ina pendekezo gani juu ya mfumo wa Muungano ambao utaipa Zanzibar fursa ya kutumia haki zake katika mambo kama haya ambayo hivi sasa haiwezi kuyatumia.

Jengine Mhe. Spika, ni agizo nambari 29, hili sitaki kulisoma kwa sababu ni refu sana. Kwa ufupi tu agizo nambari 29 linahusu hili alilozungumza Mhe. Hija Hassan Hija, la utaratibu wa kutoka *analogy* kwenda *digital*. Mhe. Spika, mimi naomba maelezo ya kina katika hili kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kampuni ambayo imeteuliwa au imechaguliwa kupewa zabuni ya kutoa huduma hii kwa *ZBC*, Shirika la Utangazaji la Zanzibar, ni Kampuni ya *AGAPE*. Lakini tulivyofahamu sisi kutokana na maelezo ya awali, ni kwamba anayetoa huduma ni Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar kwa kupitia Shirika lake la Utangazaji, imeikodi Kampuni ya *AGAPE* ili kutoa huduma kwa *ZBC*. Lakini palikuja maswali mengi sana Mhe. Spika, hapa na wengine kwa sababu ya uungwana wetu tukawasiliana na uongozi wa wizara hata tungoje Barazani hapa, lakini tukaridhishwa kwamba wasi wasi unaoelezwa mitaani huko sio kweli. Lakini utendaji Mhe. Spika, umezungumzwa masuala mengi sana.

Kwanza wananchi wengi walipokwenda kununua hivyo vinavyoitwa ving'amuzi, walikuwa wanapatiwa risiti au stakabadhi za *AGAPE* na sio za *ZBC* wala sio za serikali. Watu wakajiuliza ina maana sisi tunaichangia kampuni binafsi. Lakini kama hiyo haitoshi, pamekuja suala zima la kwamba. Hili naomba Waziri akija anipe ufafanuzi na sio wangu mimi tu na wananchi huko nje, kwa sababu hili suala linaulizwa sana na limezua maswali mengi sana. Hata Mhe. Rais alipokwenda kutembelea wizara, nakumbuka alitaka wizara itoe elimu kwa wananchi, kwa sababu wananchi huko nje wamevigomea ving'amuzi vya *AGAPE*, kuna hisia nyingi sana huko mitaani Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tunachojiuliza ni kwamba kwanza ni nani anayedhibiti zile *channel* ambazo zitakuwepo pale zitakazotolewa na *AGAPE*. Nani anakuwa na udhibiti wa mawimbi ambayo yanatolewa na *AGAPE*.

Lakini Mhe. Spika, pia katika mitandao ya kijamii kuna mjadala mkubwa sana na mimi sio mtaalamu wa mambo hayo, naomba Mhe. Waziri akija kwa sababu ana wataalamu wazuri aje anisaidie, kwamba kwa kiwango ambacho kalipwa *AGAPE* ambacho ni dola milioni 3, inasemekana zingetosha kabisa kuwa *ZBC* yenyewe kuanzisha kituo chake kikaleta na mitambo yake na kikafanya kazi hii. Leo *AGAPE* ambayo inatajwa kuwa uwezo wake ulikuwa ni mdogo sana, imepata nguvu kwa fedha hizi ambazo zimelipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ndio leo inajiimarisha Tanzania nzima kwa sababu ya fedha hizi.

Vile vile tunataka kujua na Waziri aje atusaidie katika mkataba ikoje, kwa sababu tunaambiwa *TBC* upande wa pili wa Muungano huko. *TBC* imeingia mkataba na *Star times*, lakini mwenye udhibiti na kumiliki kila kitu ni *TBC* yenyewe, *Star times* ni watoaji wa huduma tu. Hapa kila kitu tunaambiwa ni cha *AGAPE*. Kuna nini Mhe. Spika, katika suala hili na kama watendaji walimpotosha waziri basi asitufiche waziri atuambie. Ndio hayo yaliyozungumzwa jana, kwamba mawaziri katika kuwatetea watendaji huwa wanajibebesha wao mizigo halafu inawagharimu wao.

Mhe. Spika, mfano hai ulikuwa ni uwanja wa ndege pale, tulipiga kelele sana hapa jinsi utendaji wa Meneja Mkuu wa pale, wakamtetea wakubwa. Lakini hivi karibuni Mhe. Hamad Masoud ambaye alikuwa waziri, gari yake mwenyewe imeyakumba yale madudu tuliokuwa tukiyasema hapa Baraza la Wawakilishi, siku saba limekaa pale. Kwa hivyo, mara nyengine tusiwatetee watendaji, kwa sababu baadae yatakuja kutukuta sisi wenyewe humu ndani kubeba majukumu ambayo sio yetu. Mhe. Spika, nilikuwa naomba suala hilo tupewe maelezo ya kina kabisa.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, nachukua dakika moja tu, naomba nisaidiwe maelezo. Mhe. Waziri hili halimo katika maagizo, lakini linahusu wizara hii. Mhe.Waziri mwaka jana atakumbuka nilitoa hoja humu kuhusu kupigwa muziki katika kumbi za wazi, ambazo

zinawabughudhi sana wananchi, kwa sababu maeneo hayo yako katika maeneo ya makaazi ya watu.

Ngome Kongwe pale Mhe. Spika, watu hawalali. Mhe. Waziri akaingilia kati akafanya ziara, siku moja akanipigia simu akataka diwani wetu aende akashirikiane na yeye, akatoa agizo. Lakini kama kawaida ndio yale yaliyosemwa jana, inaonekana mara nyengine serikali inapwaya, kwa sababu maagizo yake hayatekelezwi Mhe. Spika. Mpaka leo kunapigwa muziki Ngome Kongwe na namuomba Mhe. Waziri afanye ziara mara kwa mara apite.

Ukumbi wa Bwawani Mhe. Spika, juu kule wazi kunapigwa muziki mpaka alfajiri kubwa Mhe. Spika, haya mambo yanawaudhi watu wetu. Lilikuwepo tukio kama hilo pale katika eneo la Vuga karibu na jumba la *Culture*. Lakini wananchi wenyewe wakachukua hatua kupitia mahakama za vileo wakaifunga, *Dharma Lounge* wamepata utulivu wamepumua. Hawa ni wananchi wanaokaa maeneo ya Malindi na maeneo ya Forodhani pana tatizo. Naomba maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri, lile agizo lake limefikia wapi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, narudia tena naunga mkono hoja ya kamati kwa asilimia mia moja na ninaomba maelezo katika hoja ambazo nimezitolea maswali. Nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kuwepo hapa tukiwa tunaendelea na majukumu yetu ya kitaifa. Pia napenda kuchukua nafasi ya kukupongeza wewe kwa kunipa nafasi hii ya angalau na mimi kuchangia mawili au matatu katika Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari.

Pia nachukua nafasi ya kumpongeza Mwenyekiti kwa uwasilishaji wake mzuri na wa fasaha. Pia nawapongeza Mawaziri wa wizara hizi pamoja na watendaji wao wote.

Baada ya utangulizi huo Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni mdogo. Mhe. Spika, naanza na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Hapa nitazungumzia suala la uzalishaji wa mazao ya baharini kwa wafugaji wa samaki. Mhe.Spika, ufugaji wa samaki hii ni ajira muhimu sana na ni ajira kubwa kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, wananchi wa maeneo tofauti hapa Zanzibar yameshajihika katika ufugaji wa samaki, wakiwemo wananchi wa Jimbo langu la Chambani nafikiri pale nina vikundi karibu vitano vinashughulikia ufugaji wa samaki. Lakini Mhe. Spika, inasikitisha kwamba ufugaji huu wa samaki badala ya kuwanufaisha wananchi hawa kimapato, ya kukimu mahitaji yao ya kila siku hili ni tatizo. Kwa sababu samaki wanaofuga kutokana na umaskini wao basi wanakuwa ni wa kitoweleo tu na sio lengo, lengo la serikali ni kuwawezesha wananchi hawa kupata maendeleo endelevu katika maisha yao ya kila siku.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri awaangalie sana wafugaji wa samaki na awawezeshe ili waweze kukidhi haja iliyokusudiwa. Mhe. Spika, wafugaji wa samaki wana changamoto nyingi zinazowakabili, miongoni mwa changamoto hizo ni umaskini. Wanapiga matuta yale kwa kuzuia maji, lakini kutokana na umaskini wao sio muda mrefu linakuja pindua wimbi, linayakata matuta yale na mwisho samaki wale wanapotea, halafu wanaanza tena kazi upya.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, aliangalie vyema suala hili, awawezeshe wafugaji wa samaki ili na wao wapate mtaji wa kujiajiri katika uajiri ambao utawapa manufaa kwenye maisha yao ya kila siku.

Mhe. Spika, nikiondoka hapa katika ufugaji wa samaki, niende kwenye uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Spika, tuna bahari kubwa na yenye samaki wengi na wakubwa wako bahari kuu, lakini kila siku serikali inapanga kuwa tutalishughulikia. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ni lini wavuvi wa nchi hii ya Zanzibar watawezeshwa katika uvuvi wa bahari kuu, tumezuia uvuvi haramu lakini uvuvi halali ndio huu, vipi utawawezesha wavuvi hawa ili waitoe minofu ya samaki iliopo bahari kuu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu niende kwa watu wanaoshughulikia uzalishaji wa chumvi. Mhe. Spika, wananchi wetu wa baadhi ya maeneo likiwemo eneo langu la Chambani wanajishughulisha na uzalishaji wa chumvi. Lakini tatizo kubwa linalowakabili wakulima hawa wa chumvi, kwanza ni kukosa utaalamu wa kutosha, pili ni kukosa ubora labda wa chumvi ile. Je, Mhe. Waziri nikuulize hapa, watu hawa wanaozalisha chumvi unawapatia wataalamu ili kuiboresha chumvi yao.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo niende kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Spika, hapa nataka nizungumze maneno machache. Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ni miongoni mwa wizara muhimu sana, kwa sababu hii kazi yake ni kuburudisha na kuelimisha wananchi. Wizara hii ina mambo mengi ambayo Mhe. Waziri unapaswa kuwaboresha wafanyakazi wa wizara hii, ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Spika, niende kidogo katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Mhe. Spika, serikali baada ya kutangaza sera ya utalii hapa Zanzibar, imefungua Chuo cha Utalii Maruhubi. Kwa kweli wanaingia vijana wetu pale Chuoni kwa ajili ya kulikabili soko la ajira ya utalii. Jambo la kusikitisha Mhe. Spika, kitabu hiki cha ripoti za kamati katika ukurasa wa 140 kwenye changamoto za utalii, kwenye nukta nambari 2 kuna maelezo haya yafuatayo.

Baadhi ya mahoteli hayatoi ushirikiano unaohitajika kwa Chuo cha Maendeleo ya Utalii kwa kukataa kuwapokea wanafunzi kwa ajili ya mazoezi ya vitendo. Mhe. Spika, hili ni tatizo, wanafunzi wanaingia pale kwa gharama kubwa wanazolipa, leo wanakwenda kufanya mazoezi ya vitendo katika masomo waliyosoma pale, lakini baadhi ya mahoteli wanakataa.

Mhe. Spika, ripoti ya kamati inasema kati ya hoteli hizo ni *Serena, Zed Hotel* iliopo Nungwi na *Utalii Beach Resort* ya Michamvi. Namuuliza Mhe. Waziri je, hoteli hizi wanaozimiliki ni Wazanzibari au ni wawekezaji walioko nje. Lakini kwa tatizo hili Mhe.Waziri amechukua hatua gani juu ya hoteli hizi ambazo hawatoi ushirikiano kwa chuo chetu ambacho wanasoma watoto wetu kukidhi haya ya soko la ajira hapa Zanzibar. Mhe. Spika, hili ni tatizo usipoziba ufa utajenga ukuta. Hoteli hizi kama hazikufanyiwa marekebisho, kuna hoteli nyengine zitawakataa wanafunzi wale. Je, wanafunzi wale wakafanye mazoezi wapi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri juu ya suala hili aje na taarifa muhimu, ambayo itawafanya hawa wamiliki wa hoteli hizi kujua umuhimu wa kuwapokea wanafunzi wa chuo kile. Pia kwa

hoteli nyengine wajue kwamba wana haja kubwa ya lazima kuwapokea vijana wetu, ili kupata kufanya mazoezi hayo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo kwa haraka niende katika Shirika la Magazeti. Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba hadi leo shirika hili halina mtambo wa kuchapisha gazeti letu hapa Zanzibar. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa nguvu zake zote, ahakikishe kwamba shirika hili linawezeshwa na mtambo huu unapatikana ili gazeti hili liweze kuchapishwa hapa ili habari zetu za Zanzibar Leo zipatikane kwa wakati.

Mhe. Spika, niseme kwa haya machache, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani, naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuweza kuchangia mawili au matatu katika ripoti hii ya wizara zetu tatu ambayo imewasilishwa hapa asubuhi ya leo.

Mhe. Spika, mimi kwanza nianze kwa kuwashukuru Wajumbe wa kamati, ambao walikuwa wanaongozwa na mama yetu hapa, mama Asha Bakari Makame. Pia taarifa hiyo ambayo imesomwa na kaka yangu Mhe. Asaa Othman Hamad, kwa kweli ripoti yao niliisikiliza kwa makini sana. Kusema kweli ni ripoti ambayo Wajumbe walifanya kazi kubwa na ya msingi kabisa na maagizo ambayo waliyatoa na kuona kwamba kwa namna moja ama nyengine, Inshaallah mawaziri watakuwa wameyafanyia kazi na kuona kwamba tumefika pahala pazuri.

Mhe. Spika, mimi katika mchango wangu nilikuwa nataka nizungumzie suala zima la wizara ya kazi. Mhe. Spika, pamoja na mikakati na mambo ambayo yalikuwa yameelezewa mule, napenda kuchukua fursa hii vile vile kuwahimiza zaidi wenzetu wa idara ya kazi, ili kuona kwamba vijana wetu ambao tunawasomesha tujitahidi tuweze kuwafanyia utaratibu, ili waweze kufanikiwa na kupata ajira kwa mujibu wa taratibu ambazo tumejiwekea.

Mhe. Spika, katika ripoti ambayo imeelekezwa hapa, naomba kuhimiza suala la ulinzi na usalama kwa mahoteli yetu ya watalii. Mhe. Spika, naomba Waziri anayehusika katika sekta ya mambo ya uwekezaji, hususan katika sekta hii ya ulinzi na usalama, kuhakikisha kwamba tunatengeneza bajeti mahususi kwa ajili ya vyombo vya ulinzi, ili ulinzi na usalama uwepo katika mahoteli ambayo watalii watakuwa wanafikia na kuendelea na shughuli zao.

Jambo la pili Mhe. Spika, pia napenda kuchangia katika suala zima la malipo ya leseni. Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka jana ambayo tulichangia hapa, tulizungumzia suala zima la magari ambayo yanabeba watalii na kupeleka katika maeneo mbali mbali ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar. Lakini magari yale yanapowapakia watalii yanatakiwa yakakate vibali, tayari leseni alikwishapewa kwa ajili ya kufanya kazi ile. Sasa hivi vibali vya ziada vya kazi gani, tuweke utaratibu maalum utakaoweza kumlinda yule mtu ambaye anakata leseni, ili akishakata leseni isiwepo tena mambo ya kuzunguka kwenda kukata vibali na mambo mengine ambayo hayasaidii.

Jengine Mhe.Spika, ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia zaidi ni utaratibu wa kuwezesha vikundi vya ushirika. Mhe. Spika, pamoja na utaratibu mzuri ambao unafanywa katika

kuviwezesha vikundi vya ushirika, ningependa basi kuiomba wizara inayohusika kuboresha zaidi utaratibu wa kuweza kuvisaidia vikundi ambavyo vimo katika majimbo yetu, ili wananchi wote waweze kuneemeka na kufaidika na mambo ambayo yanapatikana katika taasisi hizi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulichangia ni suala zima la Utalii. Zanzibar tunajitahidi sana kufanya shughuli za utalii na kuingiza watalii katika visiwa vyetu. Lakini kuna utafiti ambao hauko rasmi ambao unaonesha kwamba kila watalii wanaokuja mara ya kwanza hawarudi tena kwa mara ya pili, na inatokea hivi kutokana na hali ya mazingira ya uchafu ambayo yametuzunguka katika maeneo yetu ya mji wa Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na maelekezo, mikakati na mambo yote yanayopangwa, tungeomba suala la usafi wa mji wa Zanzibar, tuweze kulifanya kwa umoja wetu sote ili tuhakikishe kwamba maeneo yetu ya mji wa Zanzibar yanakuwa safi. Lakini na wizara inayohusika vile vile ijitahidi kuona kwamba wanajitahidi zaidi ya hapa ambapo wanafanya, ili turejeshe hadhi ya Zanzibar na kuwa mji safi na salama na wageni waweze kuja zaidi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kupata ufafanuzi ni suala zima la ununuzi wa ving'amuzi. Mhe. Spika, kuna taarifa kwamba wizara ya habari ilinunua ving'amuzi vinavyokaribia shilingi bilioni 8. Kwa hivyo, nataka nipate taarifa kwamba je pesa hizi zimetoka katika utaratibu gani.

Vile vile katika bajeti zilizopita Mhe. Waziri alikuwa akituambia kwamba kulikuwa kuna mpango wa kuwasaidia watu wetu katika maeneo yetu kuwapatia boti za uvuvi. Sasa tunataka kupata taarifa je, boti zile zimefikia wapi na utaratibu ule uko vipi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima, nakubaliana na ripoti hii mim,I binafsi na kwa niaba ya watu wa Jimbo la Kikwajuni tunaunga mkono, ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nilifikiria utaniongezea kwa huruma yako, lakini naona umenipa zile zile dakika tano.

Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nasafi hii, nataka niende haraka katika michango yangu mifupi kabisa. Mhe. Spika, nataka nipate taarifa kutoka kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo nimesikia ukumbi wa *ZBC* redio unataka kukodishwa kwa watu binafsi. Sasa nataka nipate taarifa hili suala ni sahihi, kwa sababu kama ninavyosema siku zote kwamba katika nchi za Afrika, jengo lililojengwa na Wachina pale Rahaleo na ukumbi wake ule wa studio ni ukumbi ambao katika nchi za Afrika basi ni ukumbi wa pili baada ya Ghana. Sasa kama unataka kukodishwa kwa mtu binafsi, sijui sisi wenyewe tulishindwa nini. Lakini hii nimesikia tu, nataka nipate taarifa.

Jengine Mhe. Spika, nataka nizungumzie suala la maafisa wa habari. Juzi nilipokuwa nikichangia katika hotuba yangu ya Kamati ya Viongozi Wakuu wa kitaifa, nilizungumzia kuhusu suala zima la maafisa wa habari waliopelekwa katika wizara mbali mbali, bado inaonesha kwamba hawajapata mashirikiano ya kutosha, hasa katika kupata taarifa zilizokuwa sahihi ndani ya wizara, kujua malengo na matarajio ili kuweza kuwaelezea wananchi wetu.

Suala hili Mhe. Spika, nataka nilizungumzie hivi kwa kutilia nguvu hoja ya Mjumbe wangu wa Kamati, Mwenyekiti wa Baraza Mhe. Mgeni Hassan Juma, alizungumzia sana suala la maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Alisema kwamba tungefanya *program* maalum ndani ya miezi sita kabla ya kuadhimisha zile sherehe basi kuwe kuna vipindi mbali mbali, na vile vile wananchi wawe wanahojiwa ili kuweza kutoa yale maoni yao. Tangu Mapinduzi yetu, sasa hivi tuna miaka 50 je, yale matarajio tunayapata kama vile tulivyotarajia, kama malengo ya waasisi wetu au tumeanza kupoteza muelekeo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo alifanye hivyo. Vile vile nilikuwa naomba zaidi kwamba hawa maafisa wa habari, sijui baada ya kupelekwa katika mawizara kuna mkono wa wizara ya habari wenyewe kuweza kuwashughulikia kule walikokwenda au moja kwa moja wanakabidhiwa zile wizara. Lakini kama wanaachiwa moja kwa moja wizara, wizara walizopelekwa wao wenyewe hawana taaluma ya mambo ya habari na wengine wala hawajui umuhimu wa habari zao kupata kutolewa kwa wananchi.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri, kama baada ya kuwapeleka katika wizara mbali mbali, hakuna kiungo moja kwa moja baina yako na wao, basi nilikuwa naomba kuandaliwe utaratibu maalum ili kupatiwa mafunzo ya kina. Kama kamati ya *PAC* inavyokuwa na uchunguzi wa kina sasa hivi, na wao wapatiwe taaluma ya uchunguzi wa habari na kuweza kutoa taarifa kwa wananchi. Lakini ile hoja ya Mhe. Mgeni Hassan Juma naomba sana Mhe. Waziri wa Habari aweze kuishughulikia, ili wananchi waweze kutathmini Mapinduzi yao, malengo yao na matarajio yao yako vipi na hatima yake miaka 50 inayokuja twende vipi.

Jengine Mhe. Spika, nataka nizungumzie suala zima la Utalii. Mhe. Spika, nimepata taarifa moja kwamba sasa hivi kuna ukaguzi wa mahoteli na sisi Mhe. Spika, hapa Zanzibar uchumi wetu mkubwa unategemea zaidi utalii, na utalii wetu unalenga zaidi katika suala zima la mahoteli. Tuna hoteli ya nyota moja, nyota mbili, nyota tatu na mpaka nyota tano. Sasa kuna taarifa kwamba sasa hivi kuna ukaguzi wa mahoteli, kuangalia zile *status* zao je, hii hoteli kama tunaiita ni nyota tatu, je bado inastahili katika suala zima la nyota tatu. Sasa hapa Mhe. Spika, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kidogo anisikilize.

Mhe. Spika, hivi karibu Mhe. Waziri wa Fedha ameteua ile bodi ya *ZIPA*, lakini katika ile bodi ya *ZIPA* hakuna mjumbe kutoka Wizara ya Afya. Sasa najua kwamba kuna *limit* ya wale wajumbe kuwemo, lakini mmoja katika ambao anatakiwa atoe *approval* ya ile wanaita *Environmental Health Inspection*, ambayo hiyo ndio inatoa cheti cha kusema kwamba hii hoteli inaendelea ku-*retain* ile sifa yake ya kuwa na nyota tatu. Sasa hilo kama lilikuwa halipo, basi namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ajaribu kuangalia, kama kuna uwezekano wa kuweza kumuingiza huyu afisa basi aweze kumuingiza.

Mhe. Spika, nina maswali mawili au matatu. Vipi kuhusu zile ajira za Qatar, Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika vipi zile ajira, kwa sababu vijana wetu wanatuuliza sana.

Vile vile Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi naulizia suala zima la hospitali ya wanyama. Hapa Mbweni Matrekta, kuna hospitali ya wanyama. Ile hospitali naomba ishughulikiwe kwa karibu

sana, kwa kweli hali yake sio nzuri sana kusema ile ni hospitali ya wanyama. Pia nataka nijue, kuna suala la hivi vibali vilivyotolewa, risiti ambazo ni *fake*. Tumepoteza karibu shilingi bilioni 1.5, suala hili mpaka sasa hivi katika ada za meli za uvuvi, suala hili tutapata jawabu gani.

Mhe. Spika, baada ya hayo, la kumalizia kabisa dakika moja kusema kwamba hivi karibuni nilisikiliza katika kipindi fulani cha *Star TV*. Kuna mwalimu mmoja wa Chuo anasema kwamba kuna mahoteli wanampelekea barua ya kumuomba wafanyakazi ambao wanatoka katika chuo, kuna chuo fulani kiko Mwanza kule. Naulizia hiki Chuo chetu cha Hoteli na Utalii sasa hivi hakisomeshi na kama hakisomeshi vipi vijana wetu ambao wanasoma pale Chuo cha Hoteli, mbona tunasikia wanalalamika wanakosa ajira, lakini tayari kuna barua kwa wawekezaji hasa wenye mahoteli wanaomba wafanyakazi kutoka vyuo vya kule Mwanza.

Mhe.Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii, lakini naunga mkono hoja ya ripoti ya Kamati, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana kwa kutumia dakika 7.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe tunarudi kwa Waheshimiwa Mawaziri, nimeombwa kabla ya kumuita Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, karibu kwa kifupi sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nataka nijibu baadhi ya hoja na nyengine Mhe. Waziri atazitoa kwa ukamilifu. Kwanza niipongeze sana Kamati yetu kwa ushauri ambao mara zote inatupa, pia tumechukua ushauri mwingi kutoka kwao, niwashukuru Wajumbe wote walioonesha hoja zao mbali mbali na mimi nitajaribu kuzijibu kwa kifupi sana na Mhe. Waziri atazikamilisha.

Kwanza nimpongeze sana kaka yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa hoja yake ya uwekezaji wa Pangeni. Mhe. Spika, naomba nimjibu kama ifuatavyo. Kwa kweli hoja ya Pangeni bado tunaifanyia kazi na tulikuwa tumechagua mashamba matatu, ili kuweza kumpa mwekezaji yule na shamba ambalo tumekwenda ni Kizimbani pamoja na Bambi.

Kwa upande wa shamba la Pangeni bado hatujaenda kutokana na yule mwakilishi wa mwekezaji alikuwa bado hajawa tayari na yuko nje ya nchi, basi akija wakati wowote tutakwenda pale kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, kwa ajili ya kumpatia sehemu ambayo ataona ni bora zaidi. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mwakilishi kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba aridhie na tunalifanyia kazi kwa pamoja.

Vile vile Mhe. Saleh Nassor Juma alizungumzia kuhusu chanjo ya mahepe. Kwa kweli chanjo hii ni nzuri sana kwa kuku iwapo watapewa kabla ya msimu wa maradhi yenyewe, sio unaitoa baada ya maradhi, lakini kabla ya maradhi ukiwapa chanjo hii inakuwa ni vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu maradhi ya kiwele, ambapo maradhi haya husababishwa sana na uchafu wa mabanda ya ng'ombe. Wataalamu wetu wapo karibu na wanalifanyia kazi suala hili, ili kuondosha kabisa na kuwapa muda mwingi wafugaji wetu katika kuwapa ushauri, kwa ajili ya kuepusha uchafu kwenye mabanda yao.

Suala jengine ni kuhusu uhaba wa wataalamu. Mhe. Spika, ni kweli tunakiri ni mkubwa sana, lakini serikali inajitahidi sana kusomesha kila zinapopatikana fedha inajitahidi kusomesha na hata sasa tumeamua kumsomesha *Pathologist* mmoja, ili aweze kufanya vipimo katika maabara yetu ambayo ipo pale Maruhubi na kuondokana na adha ya kupeleka *speciman* Temeke au nje ya nchi. Kwa hivyo, tunataraji hivi karibuni baada ya kupata fedha tutamsomesha mtaalamu mmoja, ili aweze kufanya mambo hayo.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kuhusu vipando kwa madaktari, Mhe. Mwakilishi ameonesha kero ya vipando vya madaktari. Lakini nataka niseme kwamba vipando vipo, isipokuwa havitoshelezi na kila pale tunapovipata vipya basi huwa tunawapa kwa ajili ya kukidhi haja ya madaktari wale.

Huduma ya *Mobile Clinic* kwa sasa hatuna Pemba. Lakini tunao madaktari ambao wanavyo vifaa vingi na wanawafuata wafugaji kule walipo na matumaini yetu ni kwamba wananchi wanapata huduma hii kwa uhakika zaidi.

Vile vile ameonesha nia moja ya kusema *risk allowance* vipi madaktari wanapata. Mhe. Spika, kwa sasa madaktari hawapati *risk allowance* na kutokana na mfumo mzima wa serikali Wizara ya Fedha inafanya utaratibu sasa wa kupata *risk allowance* kwa serikali nzima, ili pamoja na madaktari nadhani wa binadamu.

Mhe. Hamza Hassan Juma, naye alizungumzia kuhusu Hospitali ya Vinyama. Mhe. Spika, nataka niseme kwamba tutafanya ukarabati wa kutosha. Pia alizungumzia kuhusu suala la vibali *fake,* hili tunaomba suala hili atuachie kidogo Mhe. Mjumbe, kwa sababu hatua tumeshazichukua na tukilielezea hapa Mhe. Spika linaweza kuharibu ushahidi mzima wa kesi inavyokwenda.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, naye alionesha hizi boti za zamani labda tulikisia ni boti zile za Safiko. Mhe. Spika, boti hizi hivi sasa hakuna hata moja na zimeuzwa na mwenyewe mwenye mali maana yake ni Wizara ya Fedha hapo zamani na serikali haina sera ya kufanya biashara hivi, isipokuwa serikali sera yake ni kuwashajihisha wananchi, ili waweze kuvua au kufanya kitu ambacho kitawezekana kitaleta tija au mafanikio mazuri zaidi.

Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa haya machache Mhe. Waziri anaweza akaeleza vile vyengine ambavyo nimeviacha. Nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kufanya majumuisho ya ile michango yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wajumbe na nitajitahidi kadri ninavyoweza kutoa maelezo hayo.

Mhe. Spika, samahani kidogo nimesahau. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, alikuwa anakusanya zana zake. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwanza niwashukuru wale Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wameweza kuchangia wizara hii, ambapo kwa ujumla walikuwa kama 11 naomba niwataje kwa haraka kwa ajili ya kuokoa muda.

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Nassor Salim Ali
3. Mhe. Mohammed Haji Khalid
4. Mhe. Saleh Nassor Juma
5. Mhe. Abdi Mossi Kombo
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad
7. Mhe. Hija Hassan Hija
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
10. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
11. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Spika, naomba nianze kutoa majibu au maelezo kwa maswali ambayo yameulizwa na Waheshimiwa Wajumbe na naomba nianze na Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye aliuliza maswali kadhaa na nitajaribu kutoa ufafanuzi na mengine tutafahamishana baadaye.

Kwanza ilikuwa ni shamba ambalo wamepewa JWTZ. Mhe. Spika, nataka afahamu Mhe. Mjumbe kwamba shamba lile ilikuwa ni sehemu ndogo tu ya shamba letu la Kitumba na shamba hilo walipewa tokea miaka ya 1970. Lakini hivi karibuni JWTZ imezidisha maeneo yake kwa kumega shamba letu. Kwa hivyo, tumewaita kwa ajili ya kuzungumza nao, lakini kwa bahati mbaya walipokuja wametuonesha hati kwamba walipewa yale maeneo na Wizara ya Ardhi.

Kutokana na hali hiyo, naomba niseme tu katika kufanya mchakato huo wizara haikushirikishwa, kwa hiyo tunasikitika kwa hilo na tumesema tutapeleka suala hili Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa ajili ya kupata ufumbuzi zaidi.

Vile vile Mhe. Mjumbe aliuliza kuhusiana na shamba la Tunguu. Mhe. Spika, shamba la Tunguu nalo lilitumika hapo awali lilitumika kuwa ni shamba la kufugia ng'ombe wa nyama na lilikuwa chini ya Shirika la Mifugo na ambalo hivi sasa halipo. Kwa kweli serikali ilitenga eneo hilo na ndani ya eneo hilo kwa kutengeneza kiwanja cha Maonesho ya Biashara kile kiwanja tunachokiona hivi sasa.

Pia serikali ilitoa eneo jengine ndani ya shamba hilo hilo kwa kuendeleza ujenzi wake wa Chuo Kikuu cha *SUZA*, Chuo cha *ZAYADESA*, Chuo cha Utumishi wa Umma, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ilitoa viwanja hivyo kwa ujenzi wa nyumba za wananchi.

Mhe. Spika, kuhusuiana na maeneo yanayohitaji marekebisho katika Kanuni na Sheria, ambapo waziri taasisi husika Zanzibar na Tanzania Bara walibidi kushirikiana. Kwa hivyo, hivi sasa vyombo vinavyovua vinalipishwa kutokana na urefu wa muda wa kuvua, hivyo ni vyema bei itokane na uzito wa samaki wanaovuliwa na wala hakuna mrahaba unaolipishwa kwa samaki wanaovuliwa, hivyo pawekwe mrahaba.

Tukiendelea na Mhe. Salim Abdalla Hamad naye aliuliza maswali kadhaa kuhusiana na ujenzi wa mabwawa kama kuna utaalamu wowote ambao unafanywa. Mhe. Spika, naomba

nimfahamishe tu kwamba kuhusu suala la wafugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini wanaotaka kuanzisha mabwawa ya serikali.

Kwa kweli kwa kawaida wizara yangu kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira, Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka huwa inafanya ukaguzi wa eneo husika pamoja na kuangalia tathmini ya kimazingira, ili kuweza kutoa ushauri unaostahiki kabla ya kuanza shughuli yoyote ya ufugaji.

Mhe. Spika, suala jengine ni kweli kwamba wakulima wengi hupata hasara ya kuharibika kwa mwani wao wakati wa mvua. Suala hili wizara yangu imeliona na inaendelea kulifanyia kazi. Kwa hivyo, katika jitihada zake wizara tayari imeshafanya mazungumzo na Shirika la *KOICA*, ili kuanzisha Kituo cha Ukaushaji na Usarifu wa Mwani katika kijiji cha Tumbe kisiwani Pemba.

Suala la bei ndogo ya mwani. Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Abdi Mossi Kombo kwamba bei ya mwani ni ndogo ukilinganisha na kazi kubwa wanayofanya wakulima katika uzalishaji.

Mhe. Spika, kama ilivyo katika utaratibu wa biashara nyengine kwamba bei ya bidhaa pamoja na mambo mengine hutegemea na umuhimu wa bidhaa husika, na nyingi ya bidhaa hizo ilivyo kwenye soko, kwa bahati mbaya sana kwamba mwani wa *Sponosiam* tunazalisha hapa kwetu hauna thamani kubwa sana na pia kuna ushindani mkubwa katika soko, kwani zipo nchi nyingi zinazozalisha mwani kama huo.

Hivyo, suala la kuongeza bei bado litakuwa zito kidogo kutokana na mambo kama hayo. Kwa hivyo, njia pekee ambayo inaweza kusaidia kupitia usarifu ambao unaweza kusaidia kukuza thamani ya zao hili.

Pia kwa kuongezea ni kwamba tutajaribu kukaa na wizara husika, yaani Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, ili tuone kama kuna uwezekano wa kununua mwani vile vile kama wanavyonunua zao la karafuu. Kwa hiyo, suala tutakaa na kuliangalia na tuangalie *impact* zake na taratibu za kibiashara na bei za kimataifa.

Mhe. Spika, kuhusu boti za uvuvi zilikuwa zikigaiwa kupitia Mradi wa *MACEMP*. Mradi huu sasa umeshamalizika na tokea tarehe 15 Februari, 2013. Kwa hivyo, wizara imeshasita na utaratibu wa kutoa boti, isipokuwa itafanya manunuzi ya boti mbili kubwa za kusomeshea vijana 60 kuhusiana na Uvuvi wa Bahari Kuu.

Mhe. Saleh Nassor Juma naye aliulizia ingawaje Mhe. Naibu Waziri alilieleza, lakini kwa ufupi ni kwamba chanjo ya mahepe kwa kuku ni nzuri, iwapo kuku watapewa kabla ya msimu wa maradhi hayo.

Vile vile kuhusu maradhi ya kiwele kusababishwa na uchafu wa mabanda ya ng'ombe, kama banda la ng'ombe ni chafu basi maradhi haya huwa yanajitokeza.

Mhe. Spika, uhaba wa wataalamu ni mkubwa na serikali imeliona na itajitahidi kusomesha kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu.

Pia kuhusu vipando kwa madaktari ni vichache, lakini kila zinapopatikana fedha basi tutanunua vyombo vipya na tutawapa madaktari wetu.

Kweli hakuna *Mobile Clinic* Pemba isipokuwa madaktari huwa wanafuatia wafugaji wenyewe katika sehemu au pale wanahitaji huduma. Kwa hiyo, tunao madaktari katika kila wilaya ambao ndio kazi yao kufuatilia wafugaji walipo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuzorota kwa mradi wa vikundi baada ya kukamilika mradi. Kwa kweli masuala haya yanasababishwa na mambo mengi ikiwemo taaluma ya ushirika wizara imegundua hilo na imeanza kuchukua hatua kwa kukaa pamoja na Idara ya Ushirika, kwani ni njia ya kuwasaidia wafugaji wetu. Wizara itatoa taaluma kwa wafugaji kupitia maafisa wetu ambao wako mawilayani.

Kuhusiana na suala la leseni *fake* ambazo zimetolewa na hoja hii aliizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Spika, suala hili kama alivyoeleza Mhe. Naibu Waziri. Kwa ufupi ni kwamba tayari tumeshachukua hatua na kesi hii iko mikononi mwa polisi na hatuwezi kwenda zaidi ya hapo, isipokuwa tusubiri. Lakini hata hivyo huyo mfanyakazi ambaye amefanya hayo tumeshamsimamisha kazi, ili kuacha nafasi ya uchunguzi kuchukua mkondo wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ukulima wa mwani ni kazi ngumu na bei ya kwa mkulima bado ni ndogo sana. Kutoa elimu ya ukaushaji na uhifadhi baada ya mwani kukauka, kuwasaidia kuwapatia vifaa wakulima inapobidi, kutoa elimu ya usarifu, matumizi ya mwani na bidhaa zinapotengenezwa kwa kutumia mwani wakulima na wananchi wote kwa ujumla kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo.

Wizara yangu imo katika jitihada ya kuweza kuanzisha Viwanda vya Usarifu wa Mwani katika hatua za awali (*reprocessing*) au hatua ya mwisho ya usarifu (*finally*), ili kuweza kuongeza soko la mwani wa *Sponosiam* ambao unazalishwa kwa wingi na bei yake bado ni ndogo katika soko la nchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa muhtasari hayo ni maelezo au taarifa kuhusiana na malalamiko au madai ama maswali na mengine yalikuwa ni nasaha au ushauri. Kwa hivyo, kwa ufupi tunachukua ushauri huo na tutajitahidi kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wajumbe katika majimbo pamoja na wananchi wenyewe, ili kuona kwamba shughuli hii ya ufugaji inaendelea ipasavyo na kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na naomba nichukue fursa hii kama ulivyonipa ni kutoa maelezo kuhusiana na hoja mbali mbali ambazo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wametoa na mengine wameyataka baada ya Mhe. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hii ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ambayo inaongozwa na mama yangu Mhe. Asha Bakari Makame, lakini leo Mhe. Asaa Othman Hamad ndiye alikuwa muwasilishaji wa ripoti. *(Makofi)*

Mhe. Spika, takriban Wajumbe 11 walitoa maelezo na kutaka ufafanuzi au ushauri kuhusiana na mambo hayo naomba niwataje Waheshimiwa Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Nassor Salim Ali
3. Mhe. Mohammed Haji Khalid
4. Mhe. Saleh Nassor Juma
5. Mhe. Abdi Mossi Kombo
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad
7. Mhe. Hija Hassan Hija
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
10. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa; na
11. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Spika, naomba nianze na hoja za Mhe. Kaimu Mwenyekiti mwenyewe. Vile vile niipongeze tena Kamati hii kwa kweli imekuwa ikitusaidia sana wizara yetu katika kutuongoza na kutuelekeza kwenye mambo mbali mbali na mara nyingi maelekezo yao huwa yenye maana na yanatusaidia sana kupata ufanisi.

Mhe. Spika, nipokee pongezi ambazo amezitoa Kaimu Mwenyekiti kuhusiana na ufanisi wa Mkurugenzi wa Chuo tutampelekea mwenyewe na ninakubali kwamba yule mama anajitahidi sana. Kuhusu suala la mmong'onyoko wa fukwe katika chuo, kweli kuna tatizo hilo kubwa na sisi tumeanza kulichukulia hatua.

Kwa kweli hivi sasa tumeiomba Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na wataalamu wake wa mazingira wamekuja na waliangalia na wametupa ripoti ambayo tumeanza kuifanyia kazi, ambayo inahitaji fedha nyingi kidogo. Lakini tutashirikiana na wafadhili, wadau wa maendeleo pamoja na serikali yenyewe kuona namna gani mmong'onyoko ule wa ardhi sehemu ya bahari katika chuo kile utashughulikiwa.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo Kaimu Mwenyekiti amezungumza kuhusu uvamizi wa Hoteli ya Bwawani. Mhe. Spika, ni kweli eneo la Hoteli ya Bwawani lilivamiwa na hata pale baada ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kutoa maagizo basi tuliona watu wameanza pirika za ujenzi tena. Lakini uongozi wa hoteli kwa kushirikiana na wizara tukasimama kidete na tunafurahi kusema kwamba sasa uvamizi ule umedhibitiwa.

Eneo jengine ambalo Kaimu Mwenyekiti alitaka maelezo ni kuhusu suala la maslahi ya wafanyakazi wa Kituo cha *ZBC* Dar-es-Salaam. Mhe. Spika, suala hilo tumelifanyia kazi na katika masuala ya utumishi (*nominal role*) iliyofanywa katika bajeti ya mwaka huu, basi eneo hilo linafanyiwa kazi pamoja na Idara ya Utumishi Serikalini na tunaamini kwamba katika bajeti ijayo hali itakuwa ni tofauti sana.

Mhe. Spika, suala la uhaba au ubovu wa vifaa vya studio katika Shirika la *ZBC*. Kwa kweli hilo tunalikubali, lakini kama nilivyosema jana asubuhi ni kwamba hivi sasa tunafanyia kazi

uwezekano wa kununua vifaa vipya vya *studio* kwa ajili ya *Studio* ya *ZBC Karume House* na pia *Studio* ya Pemba.

Kwa hivyo, serikali inatarajia kutumia dola milioni moja kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo na tukijaaliwa katika kipindi si kirefu kinachokuja basi hali hii itafanikiwa, baada ya kujenga mitambo ya *digital* tunakoendelea sasa ni kuimarisha mitambo ya studio na tumeanza vizuri na Mhe. Waziri wa Fedha ameniahidi kwamba atakwangua kila alichonacho lakini serikali iweze kununua mitambo hiyo, kwa kweli ninamuamini sana akiniahidi huwa anatekeleza. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Kaimu Mwenyekiti alitaka tuimarishe eneo la kiwanja cha Dole (*Olympic Station* ya Dole) na suala hili pia alilizungumza Mhe. Nassor Salim Ali. Mhe. Spika, kiwanja hichi kiko chini ya Kamati ya *Olympic* Tanzania ndio wenyewe na sio Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Kwa hivyo, ni kweli kwamba kina matatizo ya vyoo, umeme na maji, lakini mmiliki ndiye mwenye jukumu kubwa la kupeleka haya na kama amepata matatizo basi aje wizarani tuje tukae tuangalie tutamsaidia vipi. Lakini hata hivyo, kwa sababu limezungumzwa hapa tutawaita na kuwauliza mipango yao ni ipi na tukiona kwamba wanahitaji msaada wa wizara, basi tutaangalia uwezo wetu tuwasaidie lipi katika mambo mengi waliyonayo.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na suala la maeneo ya kihistoria hasa kuhusu Mkamandume limezungumzwa sana. Kweli Mhe. Spika, maeneo ya kihistoria ya Mkamandume hali yake si nzuri yamemaliza kiasi ya kwamba ni kifusi na wala si gofu tena. Kwa hiyo, kuna kazi kubwa kwa sababu kuna historia kubwa na sisi chini ya Idara ya Mambo ya Kale imelifanyia kazi na imeliweka kama ni eneo la kipaumbele eneo hili la Mkamandume, kwa sababu lina historia kubwa na linahitaji fedha nyingi.

Kwa maana hiyo, kazi ya kwanza tuliyofanya ni kulifanyia *study*, kwa hiyo tunalifanyia *study* na tunashirikiana na wengine wenye *interest*, na hili na baada ya hapo tukishafanya *study* tuangalie tutapata fedha, kwa kweli linahitaji *total renovation* na sio kufanya mas-hara, kwa sababu liko chini lote linahitaji kuchimbuliwa, hivyo linahitaji fedha nyingi lakini kwa kuwa ni eneo ambalo lina utajiri mkubwa wa historia katika nchi yetu basi kazi hiyo tumeikusudia kuifanya.

Mhe. Spika, pia Mhe. Kaimu Mwenyekiti alizungumza jambo ambalo kwa kweli halikunifurahisha kwa sababu Mhe. Kaimu Mwenyekiti mimi ni mwenzangu sana, baadhi ya mambo nadhani angeweza kuniuliza basi ningeweza kumpa majibu kuliko kuliripua hapa kama alivyoliripua ni kuhusu suala la Mhariri Mkuu wa *ZBC*.

Mhe. Spika, alieleza asubuhi hapa kwamba Mhariri Mkuu wa *ZBC* kwa taarifa aliyoipata ni kwamba alifanya utovu wa nidhamu mbele ya Katibu Mkuu pamoja na kufanya uharibifu wa fedha shilingi milioni 6 na baadaye akachukuliwa hatua na Katibu Mkuu, lakini mimi kama Waziri nikamrejesha. Kwa kweli kauli hii haina usahihi, isipokuwa ina usahihi kidogo lakini haina usahihi kama ilivyo. *(Makofi)*

Kwanza nakubaliana naye kwamba kwa vipimo vyangu alifanya utovu wa nidhamu mbele ya Katibu Mkuu na ni kweli kuwa kuna mazingira alifanya uharibifu wa fedha, pia ni kweli

kwamba Katibu Mkuu wa Wizara alimchukulia hatua za kinidhamu lakini si kweli kama Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo alimrejesha baada ya kutiwa adabu na hilo ndilo ambalo ninalolikanusha. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, usahihi wake baada ya Katibu Mkuu kumchukulia hatua za kinidhamu alikimbilia Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ndiyo iliyomrejesha. Kwa hiyo, sisi kama wizara tunayafanyia kazi maamuzi ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma na wala hatuwezi kukubali kwamba mtumishi afanye utovu wa nidhamu mkubwa mbele ya Katibu Mkuu wa Wizara na halafu atiwe adabu na baadaye Kamisheni ya Utumishi wa Umma imwambie rudi na uchukue nafasi yako.

Kwa kweli ni jambo ambalo tumeliona pale wizarani na sio tunalifanyia kazi kidogo na tutashirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tuone na ikiwezekana Katibu Mkuu Kiongozi tuone hali ile tutairekebisha vipi, lakini nasema Waziri hajamrejesha. *(Makofi)*

Nikiendelea sasa nataka nitoe ufafanuzi kuhusu hoja za Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Jasiri). Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Mjumbe alizungumzia mambo tofauti, lakini mengi yalikuwa ya kunishauri, yaani amenishauri mambo mengi na ninamshukuru sana.

Vile vile alitaka kujua *scheme of service* ya waandishi. Kweli Mhe. Spika, waandishi wetu wanafanya kazi kubwa sana na wanahitaji kutunzwa sana, sasa baada ile sheria iliyopitishwa na Baraza lako tukufu la mwezi wa Januari la Shirika la *ZBC*, basi eneo moja ambalo tunalipa kipaumbele ni suala la maslahi ya wafanyakazi hawa.

Kwa hivyo, tunasikitika na hali ambayo wanaipata hivi sasa, lakini hili ni kipaumbele na mara baada ya sheria ile kuwekwa saini na Rais basi ni jambo ambalo tunaliahidi Baraza hili kwamba maslahi ya waandishi wa habari yatashughulikiwa kwa mazingatio mapana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo alizungumza Mhe. Mwakilishi ni kuhusu suala la Hoteli ya Bwawani kuhusu hati miliki. Kwa kweli suala hili tumeanza kulifanyia kazi kwa mashirikiano na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na tunaamini baada ya muda mfupi, kwa sababu ni suala ambalo la siku nyingi basi suala hili litapatiwa ufumbuzi.

Pia alizungumzia kuhusu wafanyakazi 15 waliofukuzwa. Mhe. Spika, hapa naomba nitoe ufafanuzi kwamba hakuna wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani 15 waliofukuzwa, isipokuwa usahihi wake ni kwamba wakati wanaajiriwa wafanyakazi wa Hoteli ya Bwawani, wafanyakazi 8 waliwasilisha vyeti vya kughushi, hivyo kwa sababu ya kosa hilo hawakuweza kuajiriwa.

Mhe. Spika, wamefanya kazi kubwa ya kwenda huku na kule mpaka wameshakwenda Tume ya Utumishi Serikalini, Mhe. Makamu wa Kwanza Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kulizungumza hili, lakini kwa kuwa wameonesha kutokuwa waaminifu tokea mwanzo kwa kuwasilisha vyeti vya kughushi kwa kweli hatuwezi kuwaajiri katika sekta ya umma na hivyo, itakuwa kweli tunapalilia mambo haya.

Mhe. Nassor Salim Ali namshukuru sana kwa mchango wake na ameweza kunisaidia sana na huyu ni mwanamichezo maarufu sana, hivyo namshukuru sana kwa ufafanuzi na ushauri alionipa, lakini akataka baadhi ya mambo niyatolee ufafanuzi. *(Makofi)*

Jambo la kwanza ni kuhusu *Studio* ya Rahaleo, kwa kweli pale tumejenga ukumbi wa vijana wa kurekodia muziki, jengo zuri naye bahati nzuri liko jimboni kwake. Katika jengo lile kuna vyumba kadhaa. Kuna ambavyo vinatumika kurekodia sanaa lakini pia kulikuwa na ukumbi ambao zamani asili yake ulikuwa ukumbi wa sinema mkubwa tu.

Sasa vikundi hivi mbali mbali tunavishajiisha vije vitumie jengo lile ni jengo lao. Lakini pia katika kuendeleza sanaa ukumbi huu mkubwa tumeuweka unaweza ukatumika kwa shughuli mbali mbali za ngoma. Kwa sababu ngoma nayo ni moja katika shughuli za kuendeleza sanaa. Kwa hivyo katika hili mipango imefanywa na Kamisheni ya Utamaduni na Michezo ambaye ndio mmiliki wa jengo hili kuona kwamba ule ukumbi mkubwa wa shughuli mbali mbali pia unaweza kutumika kukodiwa kwa shughuli za ngoma mbali mbali. Kwa hivyo mtu yoyote ambaye ana ngoma yake anataka kupiga ukumbi ule tumeweka ruhusa kuja kwa utaratibu maalum kupitia Kamisheni ya Utamaduni basi anaweza kuupata kwa njia hiyo. Kwa hivyo sio kwamba iwe harusi iwe jambo gani ikiwa ni shughuli ya ngoma basi ruhusa kufanyia kazi.

Masuala ya uhusiano baina ya *ZFA* na *TFF*. Mhe. Spika, naomba sote tukubaliane kwamba shughuli za michezo si jambo la muungano hilo jambo la msingi la kuliweka moyoni. Kwa hivyo *TFF* wana shughuli zao za michezo na *ZFA* wana shughuli zao za michezo.

Kwa hivyo, kwamba *TFF* haikuja hapa wana uhuru wao wakija sawasawa na *KFF* katika suala hili. Sawa sawa na *Kenya Federation of Football* kwa hivyo wakija sawa kwa sababu *ZFA na TFF* kwa kweli tunavichukulia ni kama vyama sawa. Kwa hivyo hakuna mmoja anayemdharau mwengine, hakuna mmoja anayempandisha mwengine. Kwa hivyo katika hili nadhani tukaliweka katika nafasi hiyo.

Migogoro iliyoko katika ngazi mbali mbali za vyama vya michezo ni kweli ipo lakini jukumu letu sisi wanamichezo kuhakikisha kwamba tunafanya kazi ya ziada kuviasa vyama na vilabu mbali mbali kufanya kazi zao kwa murua kabisa bila kusababisha migogoro. Sote wengine humu wanamichezo mbali mbali kwa hivyo tujitahidi kulifanya hilo.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa ni kuipitia katiba ya *ZFA*, nimeliagiza Baraza la Michezo imeifanyia kazik hiyo na baada ya muda nadhani kwamba suala hili litapata ufumbuzi. Kuna suala la kwamba tuvitgafutie Ofisi vyama mbali mbali vya michezo 33 vile vilivyosajiliwa. Mhe. Spika, mimi nadhani kwamba labda vyama vimekuja kujishtaki. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria ya kusajili vyama hivi moja vinatakiwa viwe na ofisi.

Sasa kama chama kimepata usajili halafu vinakuja tena kwetu wapewe usajili nadhani wanatwambia kwamba tumfutia usajili wake kwa sababu hawajakamilisha masharti. Basi tutavifanyia uhakiki Mhe. Spika, vile vyama ambavyo ni vya mfukoni tutachukua hatua ya kumwambia Mrajis wa Vyama avifute lakini Wizara haiwe kuchukua kazi hiyo ya kukitafutia kila chama ofisi kwa kweli bajeti hiyo hatuna. Nadhani kwamba fedha ya mlipa kodi ya Zanzibar

haiwezi kutumika katika suala hilo. Mheshimiwa alikuwa na suala la sport academy nimeshalizungumza pia.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo amelizungumza ni suala la digital ya Zanzibar na hasa king'amuzi chetu kionesha mipira ya ligi ya Uingereza. Jambo zuri Mhe. Spika, hili na kweli lingezidisha hadhi katika ving'amuzi vyetu. Lakini nataka nimwambie kwamba ligi ya Uingereza ina copy right ili uweze kuitumia lazima ulipe fedha nyingi na kwa nchi zetu hizi huku wakala wake *DSTV* na nchi za kaskazini wakala wake ni Abudhabi.

Sasa sisi kama muksi wa serikali hatuwezi kufanya *piracy* itakuwa ni kosa kubwa. Wengine wanaofanya waachie na sisi kupitia *Zanzibar Protracting Commission* tunatakiwa tuhakikishe kwamba kituo chochote kile cha utangazaji kiliopo Zanzibar hakifanyi kosa la piracy. Kwa hivyo kama kuna mtu anafanya kosa la piracy ajue kwamba anavunja sheria na sisi Wizara kupitia Kamisheni ya Utangazaji tuna jukumu la kumchukulia hatua. Lakini la kwanza tunaelimisha kwamba vituo vya televisheni viliopo tuhakikishe kwamba mipira wanayoitangaza ni jambo zuri lakini wafuate sheria ambazo zinaeleweka.

Baada ya hapo niende kwa Mhe. Mohammed Ali Khalid ninamshukuru sana kwa ushauri wake na hasa katika suala la waandishi wa habari tutalifanyia kazi na utalii kupitishwa mahali muchafu hilo tutalizungumza.

Suala la Mhe. Saleh Nassor Juma tunamshukuru, suala lake la *TFF* nalo nimelizungumza kwamba suala hili si suala la muungano kwa hivyo hatuwezi kuilazimisha *TFF otherwise*.

Mhe. Abdi Mossi Kombo tunakushukuru sana kwa ushauri wako, Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Mtambwe tunakushukuru sana isipokuwa uliuliza suala la kwanza kuhusiana na Hoteli ya Bwawani ama kuuzwa ama kubinafsishwa au kuvunjwa au vyenginevyo.

Ni kweli Mhe. Spika, serikali inaangalia kwa makini matumizi sio ya Hoteli ya Bwawani, lakini ya ile *pyramid* ya Bwawani, kuna hoteli na lile eneo zima yaani ile njia tatu. Kuna ile njia kubwa halafu kuna zile njia moja inatoka pale inapita watersale mpaka Bwawani na nyengine inatoka huku msikiti mabuluu. Kwa hivyo eneo lile tumeliona kwamba serikali inalizingatia kwamba linaweza likatumika vizuri zaidi kubadilisha haiba ya nchi yetu. Kwa muda mrefu tumekuwa na Bwawa lile ambalo umelisema, bajeti ya serikali kuweza kulifukia au kulitumia vizuri lile linahitaji fedha nyingi.

Kwa hivyo Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya habari inalizingatia suala hilo kwa makini sana na kuna wawekezaji wamekuja Wizara ya Fedha kupitia *ZIPA* inaangalia kama atapatikana muekezaji mzuri ambaye kwa kweli anaweza akabadilisha mandhani ya pale serikali itayazingatia na baadae taarifa italetwa Barazani nini ambacho kilifanyika. Lakini kwa hivi sasa naweaza kuzungumza hivyo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la fedha zitapatikanaje katika kuendesha *ZBC* hapo baadae kama nilivyozungumza asubuhi kwamba shirika hili linategemea kujiendesha kibiashara na wale wote ambao watafaidika kwa njia moja au nyengine na huduma ambazo *ZBC* wanazotoa itabidi walipe. Kwa hivyo tunaamini kwamba kwa mtindo huo basi *ZBC* itaweza kujiendesha vizuri,

itakuwa na biashara ambayo inafanya vizuri na itaweza kulipa vizuri wafanyakazi wake na waandishi mbali mbali kwa wale wanaotafuta habari na wale ambao wanakuja hapa Barazani pia.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la *ZBC* na zaidi kwanza gazeti. Kwanza nataka waheshimiwa wajumbe wakulibaliane name kwamba Shirika la Magazeti kwa kweli katika kutangaza shughuli za Barazani linajitahidi sana lazima tukubaliane mtu lake apewe wakati mwingine si vizuri kulaumu kila jambo. Shirika hili kila siku utaona kuna ukurasa ambao waheshimiwa wajumbe wametoa taarifa mbali mbali. Sasa kama mwaka jana imepitikiwa au haikotoa taarifa zinazohusu na *PAC* pengine kuna jambo lifuatwe lakini si sahihi ku-*excuse* Shirika la Magazeti katika suala la kuripoti shughuli za Baraza lako tukufu Mhe. Spika.

Jambo jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala na katika hili nitakuwa ninamjibu Mhe. Jussa katika suala la Zanzibar Multiplex. Kwanza naomba niseme kwamba serikali ya Zanzibar iliahidi tokea mwaka 2012 Januari kwamba ikifika Disemba au Januari mapema Zanzibar itakuwa imeingia katika anga za digital kwa sababu ilikuwa ndio makubaliano ya nchi hizi za Afrika ya Mashariki.

Kwa hivyo, wenzetu walianza mapema na sisi kwa sababu hiyo mwaka 2012 tukautumia kuhakikisha kwamba Zanzibar nayo haiachwi nyuma katika hili. Kwa hivyo makampuni mbali mbali yakaja kuomba tenda ya kuanzisha *digital* ya Zanzibar. Nimetaja juzi hapa kwamba alianza Huawei alitaka dola ishirini na nane milioni, zikaja kampuni nyengine nazo zikataka pesa nyingi. Star times alikuja yeye alikuwa na masharti ambayo kwa kweli sisi kama Zanzibar tuliyakataa kwa sababu tulikuwa na vigezo vyetu.

Kigezo cha kwanza ni kwamba mitambo itakayowekwa iwe ni mali ya Serikali hiyo lazima kwa sababu *information* is *power* hatuywezi kumwachia Kampuni yoyote kumiliki mitambo ile muhimu ya habari. Kwa hivyo hilo ndilo lililokuwa shurti la kwanza kwamba yeyote atakaekuja basi mitambo ile iwe ni mali ya serikali.

Lakini la pili ni kwamba vifaa vitakavyotumika hasa *transmitter* ziwe za *road insure* za Kijerumani na zisihamishwe kutoka eneo moja kwenda jengine. Tumefanya hivi kwa sababu mafundi wetu wameshatumia hizi *transmitter* kwa siku nyingi. Sasa wakaja Kampuni hii ya kwanza wakataka dola ishirini na nane pesa nyingi. *Star times* yeye akaja akataka sisi atujengee mitambo iwe yake tukamwambia nenda, yeye akatwambia mtapitisha *channel* yenu moja pale tukamwambia hapana.

Akaja *AGAPE* akataka dola milioni 4 lakini akakubali yeye mitambo iwe ni yetu na *transmitter* ziwe za kwetu za *road insure* za Kijerumani na atafanya kazi hii ndani ya miezi 3. Akaja mwengine *DIXIN* ya China, yeye akakubali kujenga lakini kwa *transmitter* sio za Kijerumani za Kichina tukamwambia hapana, sasa tukampa *AGAPE* kwa sababu masharti yetu yote ameyakubali.

Kwa hivyo, kazi yake sisi tulitoa kama serikali imetafuta dola milioni nne kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anajenga halafu anakwenda mitambo ya kwetu, hatukutaka ajenge halafu a-

own kama utaratibu wa *star times* amesema Mhe. Jussa *Star times* na *TBC* ndoa yao nzuri, mbaya sana.

TBC amepitisha *channel* moja wameunda kampuni moja ya star media mtihani. Sasa sisi hapana, sisi ile *infrustructure* ya SMZ si ya mtu mwengine. Sasa amejenga tunashukuru ametujengea na kwa kweli ametuwekea *transmitter* 12 sisi tumetaka 10 ameleta *transmitter* 12 mpya sasa zipo na baada ya kujenga sasa nani ataendesha hii ndio ilikuwa mtihani mkubwa.

Mhe. Spika, suala kubwa kwa kutilia maanani kwamba hii ni teknolojia mpya inahitaji wahandisi wazuri katika mambo ya *network* na mambo ya *digitalization* jambo ambalo katika wahandisi wangu nilionao Wizarani sina, sasa ama ibakie *white elephant* au i-*operate* na ikibakia *white elephant* maana dhana na muongozo na haja ya serikali ku ingia *digital* ingelikuwa haiwezekani. Ingelikuwa wenzetu wameshakwenda sisi bado tumebakia. Kwa hivyo sasa tufanye nini tukasema aa tutafute mtu mwengine sasa tumpe *contract* ya *operation ZBC* mafundi wangu hawawezi huo ndio ukweli wenyewe.

Sasa kwa masharti kwamba wakati wa kipindi cha *operation* atawafundisha watu wetu ili akiondoka watu wetu waweze kuendesha. Sasa katika hali hiyo basi sisi tumejaribu kuangalia na tukakubaliana kwamba *AGAPE* kwa sababu ndie aliyejenga apewe kwa muda wa miaka 2 na tungempata mtu mwengine lakini *any technical fault* ingelitokea baadaye angetwambia aa mitambo mibovu. Lakini kwa sababu Agape ndie mtoto aliyemzaa lazima amlee kwa muda wa miaka 2 halafu wakati huo huo wahandisi wameshafahamu nini kinafanyika akiondoka itakuwa sasa tuna *infrastructure* ya kwetu ambayo vijana wetu sasa wanaweza kufanya kazi.

Lakini la pili jengine ni kwamba *ZBC* ni *content provider* yaani ni mtengenezaji vipindi na sheria ya Tume ya Utangazaji inataka tutenganishe *content provider* na *multiplex operator*. Sasa ZBC tayari yeye ni mtayarishaji vipindi hawezi tena kuwa *multiplex operator*, kwa hivyo ndio maana yake sasa serikali hivi sasa kwa kusaidiana na Mwanasheria Mkuu tunatayarisha kampuni inaitwa *Zanzibar Multiplex Company*, huyu ndie atakuwa hii mitambo yote ya *digital* ndie yeye atakuwa anai-own akiondoka *AGAPE* yeye ndie mwenyewe.

Sasa hivi tunachofanya tumewaweka pale wahandisi wetu na vijana wetu wanaangalia nini *AGAPE* anafanya tunafanya pamoja tuna-*joint operation* kuhakikisha kwamba baada ya muda vijana wake tuliowapeleka pale ni mahiri wanajifunza kwa vitendo na baada ya miaka 2 Mhe. Spika, na waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakuwa wana uwezo *Zanzibar Multiplex Company* tuna mitambo yetu inafanya kazi vizuri bila ya matatizo.

Kwa hivyo *ZBC* kazi yake sasa hivi ni kutayarisha vipindi pale *Karume House* na Kuvipeleka Rahaleo kazi yake imekwisha, *Zanzibar Multiplex Company* anachukua hapa anasafirisha nchi nzima kupitia minara sita inayotumika katika nchi yetu, mitatu Unguja, mitatu Pemba. Kwa hivyo hatujachukua kwa hivi sasa bado hatujachukua mitambo ya *ZBC* tumejenga wameleta vifaa wanafanya kazi, labda minara, minara tumetumia miwili na tunatumia miwili ya *ZANTEL* na tunatumia miwili ya *E-government* kwa sababu hatukutaka kujenga minara mengine. Kwa hivyo suala hilo ni muhimu mulifahamu na lifahamike vizuri.

Nimeulizwa hapa na Mhe. Hija tuko *digital* au tuko *analogy*. Tuko *both digital* na *both analogy* hivi sasa kwa sababu gani Mhe. Spika, wenzetu hapa Dar es Salaam kama mnafatilia vyombo vya habari hivi sasa kuna mgogoro mkubwa baina ya serikali na watu hawa makampuni wanaotua huduma za *digital* kwamba walitaka wende kwa pamoja *digital* na *analogy*.

Sisi mwanzoni kabisa tukawalazimisha *AGAPE* kwamba lazima twende *both analogy* na *digital*, utaratibu huu kwa kitaalam unaitwa *simulcast* yaani *simultaneous broadcasting*. Kwa hivyo hivi sasa wale wenye ving'amuzi wanapata *digital* na wale ambao hawana ving'amuzi wanapata analog kwa hivyo sisi tuko mbele sana katika kutoa huduma hizi. Kwa hivyo hatukutaka kuzihamisha kabisa lakini tunakwenda hivi mpaka tuhakikishe kwamba ving'amuzi vishaenea nchi nzima tuta-*switch off analogy* na kwa hivyo tutakwenda moja kwa moja katika *digital*.

Mhe. Spika, nimechukua wakati wako mrefu kwa sababu hili lilikuwa ni jambo ambalo linazungumzwa sana. Lakini pia

Utaratibu

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, naomba muongozo wako kidogo Mhe. Waziri wakati anaeleza kuhusu ushirikiano *TFF* na *ZFA* wakati nachangia mimi pamoja na Mhe. Saleh nilisema kwamba *TFF* haitoi ushirikiano katika timu ya Taifa. Timu ya Taifa ya Tanzania yaani *Taifa Stars*.

Sasa timu ya Taifa ni ya muungano na mimi nikiwa ni mstaafu wa *ZFA* nayafaham haya, timu ya taifa inaundwa kwa nchi mbili yaani Tanzania Bara na Zanzibar yaani *TFF* na *ZFA*. Hapa kuna utaratibu ambao katika kuteua makocha, kocha akitoka Bara kocha msaidizi anatoka Zanzibar hata madaktari pia. Sasa anaposema kwamba ushirikiano haupo na kila mmoja anafanya mambo yake *TFF* yake na *ZFA* yake hapa sio sahihi. Katika timu ya taifa hii ni timu ambayo ya Taifa ni timu ya Watanzania ya Muungano sasa nataka anipe maelezo sahihi kuhusiana na timu ya Taifa ya Tanzania *Taifa Stars*.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nitarudia hapo lakini nimalize na hili la *digital* nimeulizwa kwamba nani anamiliki *content*. *Content* ni ya kwetu sisi ndio wenye wajibu wa kuangalia nini kinatangazwa katika king'amuzi kile. Kwa hivyo tumeunda kamati ndogo ya *content* pale wanaangalia na wakimwambia hiyo toa hana ujanja itabidi atoe.

Mhe. Spika, naomba nirudie kusema kwamba bado suala la michezo si suala la muungano na bado nasema *TFF* ni Chama cha Mpira wa Miguu cha Tanzania Bara huo ndio ukweli wenyewe. Sasa kama kuna makubaliano yetu, makubaliano ya vyama viwili ni juu yao vyama viwili kuhakikisha kwamba wana-*observe* makubaliano wenyewe lakini hayakuwa *binded* na sheria wala na Katiba ya nchi yetu. Kwa hivyo ninachokusudia kusema kwamba hebu tuimarishe *ZFA* na tuna timu yetu ya Taifa iweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Spika, kuna masuala mengi ya Mhe. Hija nadhani yamepata majibu, masuala ya maposho nimeyazungumza sana kwamba tunayafanyia kazi inshaallah kuhakikisha kwamba tunalisimamia vizuri, Shirika la *ZBC* kuhakikisha hawa vijana wanalipwa. Na wao wanajua concern yangu

katika hili. Kwa hivyo jitihada nitaiongeza kuona kwamba hawafanyi kazi ambavyo haina malipo.

Mhe. Spika, Mhe. Mohammed Abdalla ninamshukuru na suala la kwa nini vijana wetu hawapati nafasi ya kufanya mazoezi katika mahoteli. Hili tulililetewa Mheshimiwa na uongozi wa Chuo, jitihada tuliyofanya tulikaa na *Zanzibar Association for Tourism Industries* kwa sababu hawa ndio wenye mahoteli na tumelizungumza vizuri hili na tumekubaliana kwamba yatarekebishwa. Kwa hivyo nawaamini watu wa *ZAT* wakizungumza huwa kama hawajakubali kitu huwa hawazungumzi. Lakini kwa hili wameliona na tumekubaliana kwamba tutalifanyia kazi kwa pamoja lakini kama kulikuwa na matatizo hayo siku za nyuma basi sasa tumekubaliana kuyarekebisha.

Mhe. Mahmoud Mussa Mwenyekiti na Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni tunashukuru sana kwa ushauri wako ambao unanipa mara kwa mara hata tukiwa nje ya Baraza ninakushukuru sana utaratibu huu unao sana wewe na Mhe. Mtando ninakushukuruni sana kwa kunipa taarifa zinazohusu Baraza nje ya kikao. Na suala la ving'amuzi vya dola milioni nane uvumi huu Mhe. Spika, si kweli hata kidogo.

Mhe. Hamza suala la ukumbi wa *ZBC* Radio haujauzwa wala kukodishwa kwa mtu binafsi. Maafisa wa Habari waliopelekwa katika maofisi mbali mbali hawa ni wafanyakazi wa maofisi hayo kwa kweli wanafanya kazi kubwa za kuandika habari, za viongozi mbali mbali wa Wizara hizo na taasisi mbali mbali. Kwa hivyo nadhani tuendelee kuwatumia lakini kama kuna jambo lolote ambalo linakwaza basi Wizara ya Habari ni kwao wakati wowote wanakaribishwa kupata miongozo.

Mhe. Hamza na suala lako la *decomentary* ya miaka 50 ambayo imetoka kwa Mhe. Mwenyekiti tunalichukua na tunalifanyia kazi. Na kuhusu Chuo cha Hoteli umezungumza kama wanasomesha au hawasomeshi, wanasomesha wanatoa Diploma na tuko mbioni tukijaaliwa kuanza mafunzo ya digirii ya kwanza.

Mhe. Spika, ninakushukuru nimechukua muda mwingi wa kutoa majumuisho lakini kwa sababu ya hoja ambazo zimeletwa niliona ni muhimu sana nichukue nafasi hiyo kufanya majumuisho hayo. Ninakushukuru.

Utaratibu

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Nilipokuwa nikichangia kwenye ripoti hii nilitaka kupata maelekezo juu ya malipo ya leseni ya watu ambao wanashughulika na biashara ya utalii, wale ambao wanakata leseni ya mwaka na baadae kukata vibali nilikuwa nataka maelekezo yako katika hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ninakushukuru mimi naomba dogo tu kwamba inawezekana kwa sababu nilikuwa nimechangia mambo mengi ameghafilika Mhe. Waziri niliuliza na ningeomba kauli yake kwa sababu ninakerwa sana jimboni kwangu suala la amri aliotoa au agizo kuhusu muziki kupigwa katika kumbi za wazi. Nilikuwa naomba muongozo wake hapa ili wananchi wa Mji mkongwe wasikie, viongozi na watendaji wanao ongoza kumbi

hizi wasikie, wafanya biashara wanaoendesha kumbi hizi wasikie ili nipate ufumbuzi kwa lugha ya Mhe. Rashid Seif *once and for all*.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ninakushukuru na naomba radhi waheshimiwa wajumbe kwa ku-*script* yote mambo mawili.

La kwanza ni suala la Mhe. Mwenyekiti suala la vibali vya utalii. Mhe. Mwenyekiti ni kweli kwamba Kamisheni ya Utalii inakusanya mapato na nataka niseme kwamba katika taasisi za Wizara yangu ambayo inakusanya mapato kwa kiwango kikubwa sana ni Kamisheni ya Utalii inafanya kazi nzuri. Sasa katika kufanya hivyo kuna ada mbali mbali wameziweka katika kuona kwamba ile azma ya serikali ya kuona kwamba tunakusanya mapato mengi kwa ajili ya uendeshaji mbali mbali unafanikiwa. Kwa hivyo ni kweli kama kuna leseni ya mwaka lakini na pia kuna leseni ya kila ambapo unakwenda.

Kwa hivyo ni utaratibu tuliouweka na unatusaidia sana Mhe. Spika, kwa hivyo kama una tatizo basi wacha nikae na watu wangu tuangalie kuu-*review* vizuri zaidi na baadae nitatoa taarifa kwake Mheshimiwa.

Kuhusiana na suala la vurugu zilizoko katika kumbi mbali mbali na hama ame-*sight* maeneo mawili. La kwanza la Ngome Kongwe na la pili la Bwawani. Lile la Bwawani kwa kiasi Fulani Mhe. Spika, limeweza kudhibitiwa kidogo. Mimi mwenyewe nimeshafanya ziara zaidi ya mara tatu usiku kwenda kuangalia namna gani ukumbi ule wa Bwawani unavyopiga muziki. Lakini ukiwa huku nje husikii na ukenda ndani utaona watu wanatipuka.

Kwa hivyo nimeridhika kwamba ile volume ya ghasia kidogo kwa ukumbi wa Bwawani kwa kweli ni nzuri isipokuwa suala hili la muda sijakaa mpaka saa nane mimi huenda mpaka saa tano pengine nikaangalia. Lakini sheria yetu inazungumza kwamba vibali ambavyo tunavitoa mwisho iwe saa sita za usiku. Sasa kama Bwawani wanakwenda above that kwa hivyo hili tutalifanyia kazi na naamini kwamba kwa uongozi uliopo pale Bwawani basi hili na kuzungumza. Ila nina tatizo ya baadhi ya maeneo Mhe. Spika, pamoja jitihada kubwa iliyofanywa jitihada zaidi inahitajika na naomba tushirikiane.

Na si Wizara yangu tu lakini kwa sababu jukumu la kukazia sheria yaani law inforcement si la taasisi moja ni la vyombo mbali mbali katika serikali. Kwa hivyo tunaelewa kwamba muziki, shughuli mbali mbali za burudani zinatakiwa zipigwe baada isha hadi saa sita usiku. Na sauti iwe ile ambayo inakubalika.

Kwa hivyo Ngome kongwe ni eneo ambalo nimejaribu kwenda zaidi ya mara tano kwa sababu wananchi kama Mwakilishi wanampa taarifa na mimi Waziri huwa wananipa wananiandikia katika massage bwana hatulali, ghasia nyingi. Mimi siku nyengine humpigia simu mtu wa utamaduni nikamwambia twende na kweli tukifika kuna ghasia sana. Mara moja, mbili, tatu nishawaambia zimeni na wakazima, wanakaa baada ya wiki moja hivi utasikia vitu vinaanza tena.

Kwa hivyo nimepewa agizo na serikali kuiangalia upya sheria inayohusiana na mambo ya burudani na vibali vyake iko katika ngazi ya Makatibu Wakuu nimeshakwena mara ya kwanza

tukapewa ushauri tuirekebishe kidogo iko sasa katika ngazi Kamati ya Uongozi ya Wizara baada ya hapo tutatoka na sheria ambayo ni kali sana kwa wanaovunja sheria hizi. Kwa hivyo naomba mnipe nafasi kidogo katika suala hili.

Lakini zaidi kuhusu Ngome kongwe miaka 7, 8 iliyopita jengo lilikodishwa kwa mtu binafsi na anamaliza mwezi wa 7 nimewaambia watu wa Mji Mkongwe tutaendelea kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba ghasia pale zinadhibitiwa, hilo tutaendelea kulifanya na mimi nikienda humchukua Sheha, Diwani kwa hivyo huwa tunafanya kazi ya pamoja na huwaambia kwamba, nikiondoka mimi rudini, lakini wanakaa mpaka waziri aje mtuhani kidogo. Ndio tukasema haya mambo lazima ni yetu pamoja tusaidiane. Lakini ikifika mwezi wa saba lile jingo litarudi chini ya Mamlaka ya Wizara na yule yeyote atakaekwenda kufanya hivyo atakuwa ni yule ambaye tunaweza kumdhibiti.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Utaratibu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu Mhe. Waziri nilipokuwa nimezungumzia suala la Rahaleo kuhusu kukodisha ule ukumbi, hoja yangu zaidi niliokuwa nimekusudia Mhe. Spika, pale serikali imewekeza fedha nyingi sana, na pale pana askari wanalina studio zetu na *investment* iliyokuwepo pale.

Sasa ukumbi ule pamoja na kwamba alinijibu kuwa haukodishwi kwa mtu binafsi lakini utakodishwa kwa ajili ya harusi. Mhe. Spika, harusi anaingia aliyekuwa ndiye na siye na pale serikali ime-*invest* pesa nyingi sana, tunaweza tukaja tukapata hasara kubwa kodi tunajua wizara itapata fedha kama shilingi laki moja na nusu, laki mbili, laki tatu, lakini hasara itayokuja kutokezea pia na usumbufu kwa wale askari wanaolinda pale.

Mhe. Spika, nilikuwa naomba hilo tu Mhe. Waziri aliangalie kwa kina. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika nakushukuru, na sisi tumeliona hilo na kabla ya kufanya tulionana na Kamishna wa Polisi Zanzibar, tukamuangalia tukamuuliza *sensitivity* ya eneo na dhamira yetu, akasema inawezekana, lakini kwa sababu tushapewa indari na chombo hiki kitukufu Mhe. Spika, nadhani indhari yake ina maana nitakaa na wenzangu kuangalia twende vipi au ikiwezekana tuvunje kabisa. Kwa sababu chombo hiki kikishatoa husema mimi siku zote Baraza la Wawakilishi lina kauli mbaya, likizungumzwa jambo kama hukulifanyia kazi ukilidharau likitokea huwa si tulisema! Kwa hivyo, mara nyingi huwa likisemwa jambo nalichukulia kwa tahadhari sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Muda wetu ni mchache na sipendelei kuja kumkatisha Mhe. Waziri wakati anaendelea na majumuisho.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliombele yetu hautoselezi kumaliza shughuli zilizo mbele yetu, hivyo naliomba Baraza lako tuweke muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyengine na *In shaa Allah* nitajitahidi niwe *very brief* ili tumalize mapema kidogo.

Mhe. Spika, nianze kwa kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia na niwataje haraka haraka kama ifuatavyo:

1. Mhe. Asaa Othamn Hamad
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohammed Haji Khalid
4. Mhe. Saleh Nassor Juma
5. Mhe. Abdi Mosi Kombo
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad
7. Mhe. Hija Hassan Hija
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa na
10. Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Spika, naomba nianze na Mhe. Asaa Othman Mwenyekiti wa Kamati, lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ile inayoongozwa na Mhe. Asha Bakari Makame na Mhe. Asaa amewasilisha kwa ufasaha kama ilivyo kawaida yake. Yeye Mhe. Asaa alikuwa anatusaidia sisi na bahati mzuri Mhe. Makamu wa Pili wa Rais upo sasa hivi na najua hili unalijua na lilizungumzwa hata kwenye uwasilishaji wa taarifa yetu ya Mpango Kazi pale Ikulu, suala zima la kuwa Kamati imekuja na pendekezo la kwamba kunahitajika nguvu za pamoja na serikali kuliongeza lile jengo letu la Makao Makuu ya wizara yetu.

Sasa hili tuliambiwa kuwa katika bajeti hii basi *Inshaa Allah* tuliingize kwenye bajeti na bahati mbaya Waziri wa Fedha hayupo lakini mkuu wa shughuli za serikali Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anasikia akija atamnong'oneza kwamba, safari hii tutaingiza kwenye bajeti yetu pesa kabisa za ujenzi wa jengo kwa awamu ili kunusuru maisha ya Idara ya Mikopo katika jengo ambalo wako katika hali mbaya sana Mhe. Spika. Lakini pia Vyama vya Ushirika wako katika hali mbaya sana inabidi zikinyesha mvua wahamishe meza hapa na pale.

Kwa hivyo, tukianza kupata pesa hizo mimi naahidi ikifika mwaka 2014 basi Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika tutaweza kuweka ghorofa mbili pale na kuhamia bila ya matatizo yoyote, na *Inshaa Allah* tutaliweza kwa sababu nia tunayo.

Lakini pia walizungumzia suala zima la jitihada iliyochukuliwa na mimi nashukuru ni kweli. Juzi wenzetu Bara wamepata US$ milioni 10 katika suala la kuwarejesha watoto waliokuwa katika mazingira magumu. Lakini sisi kwa kushirikiana na wenzetu na suala hili si la Muungano tumelisimamia sisi wenyewe na tayari vijana 377 walioko katika hali ngumu ya kufanya kazi au kutumikishwa vibaya katika kazi basi tumewarejesha skuli kwa kusaidiana na *Save the Children*. Naomba mbele yako Mhe. Spika, niwashukuru sana *Save the Children*. Lakini pia *Sober houses* tumekuwa karibu nao sana vijana wale.

Mhe. Spika, vijana hawa ukiwasikiliza wakija kuzungumza na wewe hata kama chozi lako liko mbali kiasi gani basi litakudondoka tu, lakini waliniomba na mimi nimekubali kwamba tuwawezeshe na tumeanza kuvisaidia vikundi hivi sasa kuvipatia fedha na mipango mbali mbali. Hivi juzi tu wenzetu kutoka *Ras-el-Khaima* wale wa taasisi hii ya *Al-Rahma* wamekuja na wao wenyewe wamechangia pale walivyokuja lakini pia watapata msaada mkubwa ili kupata njia za kuwezesha kiuchumi waweze kujitegemea na wasahau kule wanakotoka.

Lakini pia walinieleza tatizo lao kubwa moja kwamba hata wazee wao wamewakataa, femilia zao zimewakataa. Tunafanya juhudi sasa hivi na mimi nimewaahidi kwamba nitawachukua, nitakwenda kuzungumza na wazee wao kwamba wawakubali hawatorejea tena makosa kama hayo.

Mchangiaji mwengine Mhe. Makame Mshimba, sijui kama yupo lakini kama hayupo nataka nimpe ushauri wa bure Mheshimiwa. Mara nyingi masuala kama haya ni vizuri angekuwa anayaleta kwenye taasisi zetu kabla ya kuyaleta kwenye Baraza.

Pia kuna suala ambalo alisimamia yeye Mhe. Mjumbe na naomba niliseme hapa. Mnakumbuka Waheshimiwa Wajumbe na Mhe. Spika, Mhe. Mshimba alitoa sauti kali sana hapa kulaumu na kutulaumu Wizara ya Kazi kwamba tumeshindwa kutoa vibali kwa mawakala binafsi kupeleka watu nje kwenda kufanya kazi. Kwa nguvu zake zote Mhe. Mshimba akachukua juhudi akachukua dhamana akatuletea kampuni moja ya *ZAM*. Mhe. Spika, mimi nilitoa agizo na nikazuwia utaratibu wa kupeleka vijana wetu nje ya Zanzibar baada ya kupata barua kutoka ofisi zetu za Balozi.

Kama vile hayatoshi yale yote niliyoeleza lakini bado Mhe. Mshimba akasisitiza kwamba lazima tumpe kibali. Busara zikachukua mkondo wake tukaitana tukasawazisha. Nilipozuwia nilipata vitisho vingi, mama huyo alinisema vibaya sana hatimaye vijana mitaani wakenda mpaka kwenye familia wakasema sasa wakati umefika wa kumdhuru Waziri wa Kazi kwa sababu anatuzuilia rizki zetu. Nini matokeo yake sasa hivi? Mhe. Spika, vijana 150 kila mmoja katoa shilingi laki tatu, mama kakimbia haonekani aliko, yale ambayo niliyazuwia sasa yanaonekana. Kwa hivyo, Mhe. Mshimba atusaidie kututafutia huyo mama yuko wapi, kwa sababu yeye ndiye aliyemleta.

Mhe. Spika, haya angekuwa hakuyaleta hapa tena alikuja ofisini tukazungumza vizuri na nikamjibu vizuri kwamba tustahamili kidogo, sasa bahati mbaya Mhe. Mshimba hayupo basi apelekewe salamu na mimi nadhani wakati umefika na sisi tutoe yale madukuduku yetu ndani ya moyo wetu, karibu shilingi 45 milioni za vijana wetu zimechukuliwa.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tumsikilize Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, sasa limejitokeza tatizo hili la mahoteli, karibu hoteli zote Mhe. Mshimba anakwenda sawa hakuna matatizo, lakini matatizo ya ajira mimi nililitolea ufafanuzi na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo shahidi, aliponialika kwenda kutoa vyeti katika Chuo cha Utalii nimetoa mwaka mmoja, nimesema Wazanzibari wote ambao wana sifa kama hizo au zaidi ya hizo tayari nimewataka mameneja wa hoteli na barua tutaziandika kuanzia wiki ijayo kuwaambia mameneja wa hoteli wote, wale wote wenye mikataba ambao si Wazanzibari basi nafasi zai wapatiwe Wazanzibari wafanye kazi pale, hilo tushalitolea ufafanuzi.

Lakini pia panapotokea fursa za kazi kwa mfano sasa hivi amelalamikia suala la *overtime* kaingia tena kwenye *ZAN Tour* Mhe. Mshimba. Sasa na huko kafika lakini na sisi tunasema taratibu ziko katika Kitengo kile cha Usuluhishi wa Migogoro ni kama Mahkama hatuwezi kuyaingilia. Sasa madhali yameshafika huko basi angojee matokeo yatayotokea huko. Lakini kama anataka tukatembele kule hotelini tutakwenda mimi huwa nakwenda ati, lakini sendi bure nakwenda nikikaa na familia yangu nikishalala nalipa naondoka. Sasa kama anataka tukafanye ziara tu sijui, lakini makamishna wangu pamoja na wakurugenzi.

Unajua Mhe. Spika, jambo moja lazima Waheshimiwa walifahamu, watendaji wetu hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, kila wakati kuwasema sema wengine sio wote wakorofi, wengine wazuri tu na hasa hao wangu mimi wazuri sana, na wapo leo wamekuja wote. Sasa tunapowasema sema na wao wanavunjika moyo wakati mwengine. Watendaji hawa ni wazuri wanafanya kazi nzuri, namuomba sana Mhe. Makame Mshimba akiwa na tatizo aje.

Mhe. Ismail Jussa alipokuwa na tatizo lake la watu wa *Zantel* alinifuata tukazungumza vizuri akanipa vielelezo vyote na hilo nitamjibu vile vile kwa sababu jawabu lake lishapatikana. Wahehsimiwa wengi sana Mhe. Spika, wanakuja ofisini kwetu tunazungumza tunatatua matatizo, kuyakusanya matatizo huko ukayatafuta kuyaleta hapa Barazani si suluhisho la kupata jawabu. Mimi nadhani tujenge ile spirit ya maelewano na mashirikiano hayo yatatusaidia sana. Nadhani inatosha kwa Mhe. Makame Mshimba.

Mhe. Mohammed Haji Khalid anasema wajasiria mali tunawaleta hapa zinauzwa dawa, dawa zile tunasema zinatibu kisukari, *pressure* lakini pia zinatibu mabadiliko ya tabia ya mwili. Sasa nataka nirejee sitaki kutumia ile *statement* aliyoitumia yeye, mimi nasema zinasaidia kubadilika mabadiliko ya tabiamwili. Taarifa nilizokuwanazo Mhe. Spika, ni kwamba hazina madhara dawa zile na zimethibitishwa na Wizara ya Afya kupitia kitengo kile, sasa kama katumia zimemdhuru basi mimi namshauri asiendelee kutumia.

Mhe. Spika, naomba tuwatie moyo sana wajasiriamali wetu wanafanya kazi nzuri, tumepata sifa Zanzibar wajasiriamali wetu wanafanya bidhaa nzuri na sasa hivi soko letu zuri, naomba tupeane muda kidogo tunataka kufanya mpango wa kuwawezesha vizuri sana baadae nitatoa taarifa hizo tukijaaliwa.

Mhe. Spika, Mifugo ya AK na JK haitolewi kwa ubaguzi, lakini karibu mwaka mmoja na kidogo pesa hizi sasa hazitolewi kabisa, benki wameshindwa kuzifuatilia. Nashukuru sana kwa mashirikiano mazuri na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo siku si nyingi fedha hizi zitaletwa katika Wizara ya Kazi tutazisimamia sisi wenyewe na tutazifuatilia sisi wenyewe. Kwa hivyo, Waheshimiwa kaeni mkao wa kuondokana na umasikini tukijaaliwa, sio nyinyi kwa wananchi wenu.

Lakini pia nataka tuelewane kwamba suala hili la Mfuko wa AK na JK ni Mfuko mmoja tu, kuna Mfuko wa Kujitegemea. Hivi sasa Mhe. Rais ameanzisha Mfuko wa Uwezeshaji unaendelea kuchangiwa na Mwenyezi Mungu akipenda katika kipindi chetu cha bajeti tunatarajia *Inshaa Allah* Mhe. Rais atazindua Mfuko huu wa Uwezeshaji hapa hapa au mahala popote ambapo Mhe. Rais ataamua, lakini kwa kweli tumeshakusanya fedha nyingi ni mapema kuzitaja ambazo zitatumika fedha hizo kuwawezesha wananchi katika majimbo yetu yote 50 Unguja na Pemba tukijaaliwa.

Kwa hivyo, mikopo hii haitolewi kwa ubaguzi kwanza haitolewi kabisa hivi sasa imezuilika kwa sababu ya taratibu ambazo zipo. Watu wameuliza Benki Kuu lakini Benki Kuu ni *guarantor* tu hapa anasaidia yeye ni dhamana, kwa sababu PBZ ni taasisi ya kibiashara kwa hivyo *BoT* ndio imekuwa dhamana hapa. Mhe. Salim Abdalla Hamad nadhani umeuliza kwa nini *BoT* imeingia hapa, lakini msiwe na wasi wasi siku si nyingi pesa hizi zitaingia katika dhamana ya wizara yetu na unajua ina watu waaminifu msiwe na wasi wasi wowote kazi itakwenda vizuri tu.

Mhe. Spika, suala zima la ajira, nimeshalitolea ufafanuzi kwama sasa hivi kampeni iliyokuwepo ni kuhakikisha Wazanzibari tunawapatia ajira popote pale walipo katika taasisi mbali mbali. Lakini nikasema kuna kazi wakati mwengine vijana wetu huwa wanachagua. Mzanzibari ukimpa kazi ukimwambia hoteli ziko kazi ya kutandika kitanda, aah! Nikatandike kitanda changu mimi mwenyewe nyumbani kinanishinda.

Mhe. Spika, pia suala zima la ukakamavu katika kufanya kazi. Mhe. Spika mimi juzi nilikuwa katika hoteli fulani wahudumu wanaoleta chakula wanaosafishwa vyombo pale ukishamaliza kula sahani ishachukuliwa, lakini nikawaulia wote hakuna Mzanzibari hata mmoja. Nikamwita meneje nikamwambia kule nimetangaza mwaka mmoja wewe nakupa miezi mitatu tu ujitahidi angalau uwalete Wazanzibari hapa. Sasa akanambia Wazanzibari walikuwepo hapa lakini mtu akishakula sahani inakaa kama robo saa au nusu saa haijachukuwa, nikasema tatizo mafunzo, lakini sasa hivi vhu vhetu vya utalliita yari kinaandaa mafunzo hayo na vijana wake wengi wamegraduate nikamtoa mashaka nikamwambia sasa tutashirikiana.

Mhe. Spika, sasa hivi pale tumeanzisha kitengo cha kuripoti wale wanaokuja kutafuta ajira au kuandjiksha na natarajia inshaallah kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutafanikiwa. Tumeanza kufanikisha kaibu karibu vijana 78 wameingia kwenye mkumbo wa kutaka ajira hivi karibuni na tutaendelea kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka naaomba nizunbumzie kidogo suala zima la Mhe. Abdi Mosi Kombo eneo lako la Jimbo la Matemwe kule kuna kijiji cha Mbuyutende sasa kijiji hiki tumekichagua kama ni *satellite village* pamoja na Ungi kule Msuka. Miongoni mwa mambo mengi tunajaribu kuhakikisha kwamba vijana katika eneo hili tunawawezesha, tayari vijana wetu

wa kazi nje nje wale wako na mtaalamu kutoka Rwanda yupo anafanya kazi vizuri basi tutaleta maeneo ya kule ili wasaidie kutoa taaluma kwa vijana wetu ili waweze kujiajiri na hatimaye waweze kujitegemea. Tuwatumie sana wale vijana wako huko Mheshimiwa tusiwe mbali nao.

Vikundi vya ushirika tutaviwezesha katika kila hali, hatukutoa kwa upendeleo Mhe. Hija Hassan Hija. Wakuu wa Wilaya hawajateka nyara, Wakuu wa Wilaya wengine wamelalamika hawakushirikishwa. Kulikuwa na matatizo lazima nikiri baadhi ya maafisa wetu wa vyama vya ushirika katika wilaya walichanganya madawa kidogo hapa. Mheshimiwa ilibidi wengi wenu hapa na taarifa nimetoa kuwa nileteeni vikundi vyenu vya ushirika nivisaidie na waheshimiwa wengi walileta, bahati mbaya wengine walichelewa na ule utaratibu ulikuwa tayari. Lakini nilichofanya kibinadamu hata wale ambao walichelewa basi wale waliokuwa wameandikiwa shilingi milioni tatu au mbili tukagawana shilingi milioni moja yende huku na nyengine yende huku, si kwa sababu ya nia mbaya.

Lakini pia nataka nikuhakikishie Mhe. Hija na wengine kwamba hivi karibuni tutatoa tena fedha kama hizi na Inshaallah tutakupeni *priority* wale ambao walikosa furs ile na wale ambao walikatwa tutawasaidia vile vile.

Mhe. Ismail Jussa kilio chake cha kila siku *Zantel*. Juzi niliwaita Makatibu Wakuu au Vyama vile vya Wafanyakazi pamoja na waajiri *ZANEMA*. Miongoni mwa wafanyakazi na waajiri wale waliokuja alikuwemo kiongozi wa wafanyakazi wa *Zanztel*, akaja akanishukuru akanambia tunashukuru Mhe. Waziri kwamba matatizo yetu sasa yamemalizika. Sasa leo Mhe. Ismail anakuja anasema hayajesha, kama hayajesha bado mimi sijachoka kufanya kazi hiyo nitaendelea kuifanya. Lakini nikiona kama hayatoshi nikamwita *CEO* wa *Zantel* amekuja na bahati nadhani siku hiyo alionana na Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo vile vile wote wawili, yule aliyeondoka na huyu mpya.

Mhe. Spika, aliyeondoka amekiri kwamba bado kuna tatizo la walinzi pale, alikiri ina maana kama limemshinda. Sasa yule jamaa akaniomba nimpe japo wiki mbili tatu kwa sababu ndio kwanza kaingia, atalisimamia suala hilo la walinzi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Ismail tuliache hili mikononi mwao huyu CEO mpya aliyekuja na mimi bado nitaendelea. Lakini wale waliopewa mikataba wafanyakazi wengine ambao wameambiwa wanapumzishwa…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda si mkubwa tutapitisha ripoti hii, naona *quorum* yangu mnaiteteresha. Kwa hivyo, nikuombeni dharura zenu zichukue muda mfupi sana na ikiwezekana basi tubaki tumalize kazi hii. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Wale wote ambao mikataba yao walipewa wengine sasa wameshapewa haki zao, huyu mkubwa wao ndiye aliyesema tumeshamalizana kila kitu. Sasa kama bado kuna tatizo baadhi ya kesi hizi sasa hivi tunazi-*forward*, tunawashauri wazipeleke katika Kitengo chetu cha Utatuzi wa Migogoro. Na mimi nina hakika basi suala hili litashughulikiwa ipasavyo, lakini pia bado nitatafuta wakati tutakaa zaidi na wale vijana ulioniletea kama ni wengine zaidi ya yule, mimi nakumbuka yule mmoja aliyekuja kunambia juzi ni miongoni mwao, basi uniletee nikaenao tena ili kuweza kulimaliza suala hili lisiendelee tena. Nataka ikifika *budget time* suala hili tuwe tumeshalimaliza tukijaaliwa.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa nadhani suala lake la msingi lilikuwa suala la ajira, tutajitahidi kuendelea kutoa taaluma na tunaanzisha *course* tena hizi za kazi nje nje, zimeleta tija kubwa sana. Kwa taarifa yenu Waheshimiwa hivi karibuni tu kutakuwa na *program* maalum itatolewa na vijana hawa wa kazi nje nje ili kuhakikisha kwamba tunawapatia ajira vijana wetu katika sehemu mbali mbali. Tunaviwezesha vikundi vya ushirika na mambo mengine.

Mhe. Hamza Hassan Juma alisema kwamba mwaka jana ulizungumza habari ya ajira ya Qattar. Nataka kidogo nitoe ufafanuzi wa suala hili la ajira ya Qattar na bora umelisema. Mheshimiwa sisi tumezungumza na Oman na tulizungumza na Qattar, wakati mazungumzo haya yakiendelea bahati nzuri Oman tulikuwa tumeshafika mbali na marekebisho au mazungumzo yetu na maelewano yetu tayari ya *MOU* yalikuwa yashafika hatua mpaka kupita kwenye serikali zetu zote mbili. Bahati n zuri juzi tu kama wiki mbili tatu zilizopita waziri wa Oman amenileta ile *MOU* yenyewe ambayo anasema niipitie kwa mara ya mwisho ili tupange siku tuje tusaini, mambo yote yamekamilika.

Sasa wenzetu upande wa pili wa Tanzania Bara waliitaka hii *MOU* yetu ya Oman ili sasa walitushauri tuichanganye iwe moja. Lakini kwa hili mimi Mheshimiwa nimelikataa kwa sababu sikuona sababu kwamba tumeshafika hatua hiyo kubwa halafu sasa turejeshe tena tuichanganyishe. Mimi nadhani masuala haya ya kazi ni vizuri watu wakaelewa kwamba si masuala ya Muungano, masuala ya uwezeshaji si ya Muungano, masuala ya vyama vya ushirika si ya Muungano. Kwa hivyo, masuala haya yote tutayasimamia sisi wenyewe.

Lakini kwenye Qattar kumetokea mtihani kidogo, wenzetu walitutangulia wakazungumza nao ukaja ujumbe na hatimaye wakataka kwamba Wizara ya Kazi isimamie suala hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi nikasema kwamba na bahati nzuri watendaji wangu walikuwa wanahudhuria vikao vile nikawaambia Wizara ya Kazi haiwezi kusimamia mkataba wa Qattar kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kama hapana budi basi iwe ni Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na ndivyo ilivyokwenda.

Kwa hivyo, sisi tulichofanya kwamba masuala yetu yameingizwa kwenye mkataba huu wa pamoja, lakini juhudi maalum zinafanyika sasa hivi. Kwa sababu kuna wakati unaweza kuwa na mkataba wa Jamhuri ya Muungano lakini na sisi Zanzibar tukawa na mkataba wetu, tunafanya juhudi maalum na mawasiliano na wenzetu wa Qattar na kulikuwa na ujumbe uende Qattar ukafanye mazungumzo hayo pamoja na Kuwait ili kufanya utaratibu mzima wa kuwa na makubaliano yetu *separate,* mbali ya yale ambayo yamefanywa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, Mheshimiwa juhudi zinachukuliwa na tutajitahidi Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Asaa Othman Hamad (Kny: Mhe. Asha Bakari Makame, Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu lwa neema alizotujaalia tumekutana tena jioni hii kuhitimisha shughuli zetu tulizotumwa na wananchi na kwa idhini yako Mhe. Spika, na kwa idhini ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu naahidi nitatumia muda mchache sana na kama si utaratibu basi kwa kazi nzuri

waliyokwishaifanya Waheshimiwa Mawaziri ningesema itoshe, lakini kuna shughuli ya kamati hii inayoongozwa na mama yetu Mhe. Asha Bakari Makame kazi yake kubwa na nzuri inahitaji nayo yenyewe itoe angalau neno.

Mhe. Spika, katika hilo nadhani na ni imani yangu unakubaliana name kwamba Wajumbe wako wa Baraza lako tukufu namna gani wanavyofanya shughuli zao kati ya unayotutuma huko kwenye taasisi na sekta zote na wizara za serikali. Michango iliyotolewa ni ushahidi tosha kwamba wanakwenda huko kwa kazi maalum na ni vipi wanayatoa hata yale ambayo hufikirii ama hutegemei kama yangeweza kutajwa hapa. Ni ushahidi tosha kwamba wanakwenda kufanya kazi ya wananchi kwa kuthamini jasho la wananchi wa nchi hii, fedha inayotumika itumike mahali stahiki na thamani inayotumiwa ionekane mrejesho.

Mhe. Spika, suala la *AGAPE* lilitawala kwenye ukumbi ni namna gani fedha hizi na mitambo ile ya serikali ya Wizara ya Habari, Waheshimiwa walitaka kujua ni kwa vipi kuna mikataba, makubaliano yakoje hata kampuni iweze kuitumia. Nashukuru Mhe. Waziri ametoa ufafanuzi tosha juu ya suala hili.

Mhe. Spika, jengine ni suala la ardhi. Waheshimiwa Wawakilishi ardhi inayochukuliwa kiholela holela na wawekezaji na bahati mbaya wenzetu watendaji ikawa wanashiriki katika hili, umeona namna gani linavyotukwaza. Mhe. Spika, kwa kutumia chombo hiki kitukufu tunawaasa wenzetu watendaji kamwe wasijaribu palipotumika, palipofanyiwa, palipotendwa patoshe kwa suala la ardhi. Ardhi ni mali ya serikali, ardhi ya Wazanzibari hivyo kwenda mikononi mwa watu wengine taratibu zilizowekwa za kisheria ni lazima zifuatwe na ziheshimiwe.

Mhe. Spika, suala la *Academia* ya Michezo ilioko Dole, tuna vipaji vya vijana wetu, *academia* hii ni tunzo tumeipata na nchi nyengine za wenzetu wamepata kama sisi, lakini bado wizara tunaiomba ipeleke nguvu zake kusudi lengo lililokusudiwa liweze kupatikana.

Mhe. Spika, zao la mwani na pia samaki, kuna malalamiko kwamba bado soko ni dogo. Bei ya mwani ni ndogo sana kazi ni ngumu, mama zetu, dada zetu, watoto wetu wanateseka sana na zao hili, hivyo tunaiomba serikali kupitia wizara husika bado ifanye kazi ya ziada kuona ni vipi kazi hii itaweza kuleta tija kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, *Captain*, Mhe. Abdi Mosi Kombo Mwakilishi wa Matemwe, amekumbukia enzi yetu na ile dhana ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tutauza kwa vibati, kwa nini samaki Zanzibar hatujauza kwa vibati? Nadhani suala hili ameshalijibu mwenyewe Mhe. Waziri mwenye dhamana ya wizara hii. Shughuli ziko mbioni jitihada kubwa na Wwaziri haya wa Fedha kwa kadiri na kwa namna tunavyomfahamu sisi tunaomfahamu jibu litapatikana kabla ya Baraza hili kufika tamati yake ya kipindi chake cha miaka mitano *Inshaa Allah*.

Mhe. Spika, mahoteli ambayo hayatoi ushirikiano na Chuo chetu cha Utalii. Nadhani Mhe. Waziri amelibeba hilo na *Inshaa Allah* wataelewa. Lazima tupate ushirikiano, dhana ya utalii kwa wote ibaki kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, Ukumbi wa Rahaleo umeona Waheshimiwa Wawakilishi ulivyowagusa baada ya kusikia sasa utakodishwa kwa mtu binafsi kuendesha shughuli ambazo ni nje ya ile dhana

iliyokusudiwa. Mhe. Spika, ukumbi ule upo kwenye sehemu nyeti, yale ni majengo ya Wizara ya Habari ni mdomo wa taifa hili, si vyema na hatutoeleweka kuonekana shughuli kama hizo tena zinakwenda kufanywa mahali pale, tutawasumbua sana walinzi wetu na hatimaye kuja kuwatwisha mzigo ambao itabidi tuje tulaumiane wenyewe. Mhe. Spika, ninadhani ninaamuamini Waziri mwenye dhamana amelipokea na atakwenda kulifanyia kazi iliyostahiki.

Mhe. Spika, la mwisho ni maeneo ya wazi na muziki inayoleta kero. Mhe. Spika, jambo hili ninamuomba tena Mhe. Waziri ana mamlaka, ana madaraka aliyopewa kikatiba na yeye Mhe. Rais kampa dhamana hii kwa kumuamini. Kwa hivyo ninakuomba sana Mhe. Waziri zana ya Mhe. Rais ibaki kama mwenyewe alivyoitoa ndani ya kalbi yake. Wazanzibari ni waungwana, wastaarabu wanafanya kazi zao kutafuta riski zao, umefika wakati wa kupumzika wasipate vurugu zisizokuwa si za lazima. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Bi. Asha Bakari Makame naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari na sasa Waheshimiwa Wajumbe ni kwenu nione wale wanaopokea ripoti hizi za utekelezaji wa wizara mbali mbali pamoja na ripoti ya kamati wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KUAKHIRISHA BARAZA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa sababu kazi hii haikuwa nyepesi ilikuwa ngumu kidogo, lakini kwa mashirikiano makubwa ambayo mumeyatoa leo Katibu anatwambia kwamba shughuli zote ambazo zimepangwa kwa mkutano huu zimemalizika. Ninakushukuruni sana kwa ushirikiano mkubwa ambao mumetupa katika utekelezaji wa shughuli zetu.

Kazi iliyobaki sasa ni kufunga shughuli zetu. Kwa heshima kubwa na taadhima naomba sana nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Karibu. (*Makofi*).

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehma na neema kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kuhudhuria mkutano huu wa kumi na moja wa Baraza lako tukufu.

Ninakushuru wewe Mhe. Spika na wasaidizi wako wote, kama kawaida yako umeliendesha vyema Baraza hili na kwa umahiri mkubwa, hekma na busara ambazo zimefanikisha mkutano huu.

Mafanikio ya mkutano huu pia yanatokana na umakini wa heshima na umakini wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango mbali mbali waliyoitoa wakati wa mijadiliano. Mhe. Spika, mchango wa waandishi wa habari pia ni mkubwa katika kufanikisha mkutano huu kwa kipindi chote cha mkutano wetu, vyombo vya habari vya serikali na watu binafsi vimekuwa vikifuatilia kwa karibu majadiliano yetu na hatimaye kuwafikishia wananchi wetu. Hongereni sana kwa kazi yenu nzuri.

Mhe. Spika, ninamshukuru kwa dhati Rais wetu mpendwa wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein kwa busara, hekma na ujasiri mkubwa alionao katika kuliongoza taifa letu na kutetea maendeleo. Ni dhahiri kwamba wananchi wa Zanzibar wamekuwa na imani na matumaini makubwa kwa Rais wao kutokana na mabadiliko yanayoonekana katika nyanja za uchumi, kisiasa, kijamii.

Aidha ninamshukuru na kumpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa jitihada kubwa anayochukua kumshauri vizuri Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Sina budi pia kuwashukuru viongozi wote wa serikali, vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla kwa namna wanavyoendelea kudumisha amani na utulivu na kutekeleza majukumu yao katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Ni matumaini yangu kwamba wataendeleza mwenendo huu ili amani na utulivu uendelee kutawala katika nchi yetu, kwani bila ya amani na utulivu maendeleo tunayoyatafuta yatakuwa taabu kupatikana.

Mhe. Spika, tarehe 24 Machi, 2013 nchi yetu ya Tanzania ilipokea ugeni wa Rais wa Jamhuri ya Watu wa China XI Jinping ambapo lengo kubwa la ziara hiyo ni kukuza uwekezaji wa biashara baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Aidha, Rais wa China alipata nafasi ya kuzungumza na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na viongozi waandamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilinufaika kwa kiwango kikubwa na ziara ya Rais XI Jinping, ambapo jumla ya miradi saba imo kwenye mpango wa kunufaika na ufadhili wa Serikali ya China. (*Makofi*)

Kati ya miradi hiyo saba, miradi mitatu imekubaliwa kupewa fedha ikiwemo mradi wa kazi za miundombinu, ukarabati wa matengenezo ya Hospitali ya Abdalla Mzee na kupatiwa vifaa vya kukagua mizigo iliomo ndani ya makontena bandarini. (*Makofi*)

Ninapenda kumshukuru sana Mhe. Omar Yussuf Mzee, Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kuliarifu Baraza lako tukufu kwa ukamilifu kuhusu ugeni huu.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa hivi sasa tumo katika msimu wa mvua za masika. Mwishoni mwa mwezi wa Februari, 2013 Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania kanda ya Zanzibar ilitoa taarifa ya mwelekeo wa mvua za masika kwa mwaka huu ambayo ilielezea mvua hizo

zilitarajiwa kuanza mapema kuliko kawaida na zingekuwa za wastani na juu ya wastani kwa mwezi wa Machi na kutarajiwa kuwa juu ya wastani kwa miezi ya Aprili na May.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Kamati ya Taifa ya Kukabiliana na Maafa ilijadili na kuweka mikakati na hatua madhubuti za kuchukuliwa ili mvua hizo pindipo zikinyesha zisiweze kuleta madhara makubwa.

Kamati iliziagiza sekta zote zinazohusika na kukabiliana na maafa ziendelee kuchukua hatua za tahadhari na kujiandaa kukabiliana na majanga pindipo yakitokezea. Mpaka sasa tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hali ya wananchi bado ipo salama na hakuna madhara makubwa yaliyokwisha kutokezea.

Aidha, mvua za mwaka huu zimekuwa zikinyesha vizuri, kwani zimekuwa zikitupa muda wa kujitafutia riski.

Mhe. Spika, nchi yetu imo katika mchakato wa kupata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume iliyoundwa na kukusanya na kuratibu maoni ya mabadiliko ya Katiba kutoka kwa wananchi tayari imekamilisha kukusanya maoni hayo kupitia Shehia zao, taasisi za serikali na zisizokuwa za kiserikali pamoja na makundi maamlum. Hii ilikuwa ni hatua ya kwanza.

Hivi sasa kazi ya uundwaji wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ikiwa ni hatua ya pili inaendelea ambapo Mabaraza hayo yataanza kazi zake za kupitia rasimu ya awali ya Katiba mpya hivi karibuni. Ni imani yangu kwamba Mabaraza hayo yatatekeleza majukumu yao kwa umakini na ufanisi kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizoekwa.

Niitumie nafasi hii kuwasihi wajumbe wa Mabaraza haya, kuitumia fursa hiyo muhimu na ya kipekee kutoa michango yenye maslahi ya nchi yetu na wananchi wake bila ya kuweka mbele itikadi zao za vyama vya siasa, dini na maeneo wanayotoka. Ninaamini kuwa kama ilivyomalizika hatua ya kwanza na hatua hii ya pili itamalizika salama.

Mhe. Spika, siku ya tarehe 10 Aprili, 2013 Wazanzibari wote tulijumuika katika sherehe za uzinduzi wa kukamilika mradi wa njia mpya ya kusafirishia umeme yenye uwezo wa kuchukua megawatt 100 za umeme kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar, ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein.

Kwa hakika nchi yetu imefungua ukurasa mwengine wa maendeleo katika nyanja hii muhimu kwa mustakabali wa maendeleo yetu ya kiuchumi na kijamii. Hatua hii ni mwendelezo wa azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuimarisha upatikanaji wa huduma ya nishati ya umeme hapa Zanzibar kama ilivyoelezwa katika dira yetu ya maendeleo ya 2020, mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUZA 11) na ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010/2015.

Tunatoa pongezi na shukurani za dhati kwa Serikali ya Watu wa Marekani kupitia mfuko wa changamoto za *millennium MCC* kwa kutuunga mkono katika jitihada zetu za kujiletea maendeleo hasa katika mradi huu na ule mradi wa ujenzi wa barabara za Kaskazini Pemba.

Ninapenda kutoa wito kwa wananchi kuthamini jitihada hizi za serikali kwa kuilinda na kuitunza miundo yote ya umeme huu na ile ya awali kwa kuhifadhi maeneo ya mazingira ya miundombinu hiyo imepita.

Kwa kuupata umeme huu tunatumai kauli ya Mhe.Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuwa mgao wa umeme sasa basi itakuwa ni ya kweli. Pamoja na kuupata mradi huo muhimu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea na juhudi zake za kuwakaribisha wawekezaji wenye nia ya kuekeza katika miradi ya nishati mbadala ili kuongeza uwezo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa na umeme wa kutosha.

Mhe. Spika, taarifa za kitaalamu juu ya ugonjwa wa malaria hapa nchini inaonesha kwamba kwa kiasi kikubwa ugonjwa huu umedhibitiwa kupitia programu ya kupambana na malaria inayofadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Marekani.
Hata hivyo bado kuna matokeo machache ya kupatikana wagonjwa katika wilaya 9 za Unguja na Pemba. Ni Wilaya ya Mjini pekee ambayo hadi sasa haijaripotiwa kupatikana magonjwa ya malaria.

Serikali inaendelea na kazi ya upigaji wa dawa katika maeneo yaliyobainika kuwepo wagonjwa wa malaria. Jumla ya nyumba 26,900 zimepigwa dawa kati ya nyumba ya 28,423 sawa na asilimia 94.5 za nyumba zote zilizotakiwa kupigwa dawa.

Aidha jumla ya wagonjwa wanne wa malaria Unguja na Pemba wameripotiwa kufariki katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013.

Ninatoa wito kwa wananchi kuendelea kutumia vyandarua vilivyoekwa dawa pamoja na kutoa mashirikiano kwa watendaji wanaosimamia zoezi la upigaji dawa majumbani, ili kushinda vita dhidi ya malaria, kwani Zanzibar bila ya malaria inawezekana.(*Makofi*)

Pamoja na juhudi hizo za serikali bado kuna baadhi ya wananchi wakiwemo na baadhi ya viongozi kukataa nyumba zao kupigwa dawa. Niwasihi sana wananchi na hasa viongozi kuacha tabia hiyo, ili wawe mfano kwa wananchi wengine.

Mhe. Spika, katika siku za hivi karibuni nchi yetu imeshuhudia matokeo mbali mbali ya majanga hasa kwa kuungua kwa majengo ya makaazi na biashara. Matokeo ambayo yanarudisha nyuma ustawi na maendeleo ya wananchi na taifa kwa jumla. Uzoefu unaonesha kwamba wananchi wanaofikwa na matatizo hayo, mara nyingi hushindwa kurudi katika hali za kawaida kwa haraka na hivyo kupelekea kukataa tamaa na shughuli zao za kiuchumina kupata makaazi bora. Ni vyema basi wananchi na wafanyabiashara wetu kuwa na utamaduni wa kukata bima ili kulinda mali zao majumbani na sehemu za biashara.

Aidha ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kutumia nafasi zao kushajihisha jamii katika maeneo yao juu ya umuhimu wa kukata bima. Ni jambo la kustaajabisha kuona mwananchi anaikatia bima gari yake yenye thamani ya shilingi milioni tano au kumi, lakini anaacha kukata bima nyumba yake au sehemu yake ya biashara yenye thamani kubwa zaidi ya hiyo. Nawaomba wananchi wazitumie fursa zinazotolewa na mashirika ya bima ili kulinda mali zao.

Mhe. Spika, ardhi ni raslimali muhimu katika maendeleo ya nchi na wananchi wake kiuchumi na kijamii. Kwa mujibu wa sheria raslimali hii bado itaendelea kuwa ni mali ya serikali. Hivyo wananchi na taasisi zitapewa ardhi kwa matumizi yao tu na haitoruhusiwa kuuzwa. Hata hivyo, kumejitokeza tabia ya wananchi na baadhi ya viongozi kuuza ardhi kiholela bila ya kufuata sheria na taratibu ziliopo, hali ambayo husababisha migogoro.

Serikali haitomvulia mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na taratibu hizo. Kama kila mara Mhe. Rais anavyotukumbusha kuwa ardhi ni mali ya serikali na haipaswi kuuzwa. Mtu anayeuza ardhi anauza mali ambayo sio yake. Hivyo muuzaji na mnununi wote kwa pamoja ni wakosaji na wanapaswa kuadhibiwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Ninaelekeza Wizara ya Ardhi, Makaazi, Makaazi Nishati kusimamia vyema sheria za ardhi bila ya kumuonea haya mtu yeyote. Ninaipongeza Kamati ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kutukumbusha kuwa ardhi ambayo imetengwa kwa ajili ya jamii iachwe itumike kwa shughuli hiyo. Lakini pia na wale wananchi waliopewa maeneo makubwa yapunguzwe ili wananchi wengine nao wafaidike na raslimali hii. Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati amesikia ushauri huu na atauzingatia na kuchukua hatua zipasavyo kwa kufuata taratibu ziliopo.

Mhe. Spika, katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu suala la migogoro ya ardhi, serikali imeona njia ya pekee na ni nzuri ni kusajili ardhi kwa utaratibu uliowekwa na sheria Nam. 10 ya 1990. Katika utaratibu huo kutakuwa na mfumo maalum wa kuwatambua watumiaji wa ardhi kama vile waliopewa eka tatu tatu, mashamba binafsi, mashamba ya serikali na maeneo ya wazi. Hivyo ninachukua fursa hii kuwataka wananchi wote kusajili ardhi wanazozitumia katika muda uliopangwa kupitia Ofisi ya Mrajis wa Ardhi ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

Mhe. Spika, serikali imeanzisha sheria ya mfuko wa maendeleo ya jimbo ya mwaka 2012 kwa lengo la kuhakikisha kuwa inapeleka maendeleo na huduma mbali mbali za jamii karibu na wananchi wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Fedha hizo tayari zimeshakabidhiwa Waheshimiwa Wajumbe wote wanaostahiki kwa mwaka 2012 ambazo zilikuwa ni shilingi milioni 10 kwa kila mmoja.

Ni mategemeo yangu na mategemeo ya serikali kwamba fedha hizo zimetumika kwa mujibu wa matakwa ya sheria. Kwa mwaka huu 2012/2013 serikali imeamua kuongeza kima hicho cha shilingi milioni 10 hadi shilingi milioni 15, ili kuwawezesha Waheshimiwa Wawakilishi kuwaunga mkono wananchi wao katika miradi midogo midogo wanayoianzisha kwa mujibu wa vipa umbele wanavyoviweka. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena ninapenda niwakumbushe Waheshimiwa Wawakilishi kuwasilisha marejesho ya fedha walizopokea kwa mwaka 2012 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwani hayo ni matakwa ya kisheria ambayo tumeijadili na kuipitisha kwa pamoja ndani ya Baraza letu hili. Haitokuwa jambo la busara kuja kuoneshana vidole humu ndani, kwani sisi ni viongozi na tunatakiwa tuwe mfano mzuri kwa jamii, kwa mujibu wa sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2013 Mhe. Mwakilishi hatopatiwa fedha nyengine hadi atakapowasilisha marejesho kamili na sahihi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, katika mkutano wa kumi na moja wa Baraza lako tukufu serikali imewasilisha jumla ya miswada mitano ya sheria ambayo inalenga kulinda ustawi na maslahi ya nchi yetu. Aidha Baraza lako tukufu lilipokea ripoti za utekelezaji wa maagizo wa kamati za kudumu za Baraza kwa wizara kwa mwaka 2011/2012, zilizowasilishwa na Waheshimiwa Mawaziri wa wizara husika.

Pia Baraza lilipokea ripoti za kamati za kudumu za Baraza kwa mwaka 2012/2013 zilizowasilishwa na wenyeviti wa kamati hizo. Ripoti hizo zilijadiliwa na kuchangiwa kikamilifu na Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Spika, vile vile katika mkutano huu jumla ya maswali 82 ya msingi na maswali yapatayo 107 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wawakilishi na kujibiwa kwa ukamilifu na Waheshimiwa Mawaziri wa wizara husika.

Mhe. Spika, mswada wa kwanza kuwasilishwa ulikuwa kwanza ni Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Madhumuni ya mswada huu ni kuanzisha sheria ya mamlaka ya udhibiti wa huduma ya maji na nishati ambayo itasimamia ubora wa huduma inayotolewa kulingana na viwango pamoja na kudhibiti bei kwenye huduma za maji pamoja na nishati.

Katika kujadili mswada huu Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa ujumla walisisitiza zaidi juu ya usimamizi na utoaji wa huduma bora za maji na nishati pamoja na kusimamia utoaji wa leseni kwa wauzaji wa mafuta kwa kuzingatia viwango vilivyoekwa katika sheria hii.

Ninapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa jumla kuwa serikali inajidhatiti kuhakikisha kwamba huduma ya maji safi na salama na nishati itatolewa kwa kufuata misingi ya sheria hii ambayo itazingatia upatikanaji wa huduma bora yenye viwango vinavyokubalika na itakayokidhi mahitaji ya watumiaji. Aidha, mamlaka itasimamia viwango vya bei za maji na nishati ili kudhibiti upandaji wa bei hizo kiholela.

Mhe. Spika, mswada mwengine uliowasilishwa na kujadiliwa ni Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Bandari na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mswada huu una madhumuni ya kufanya marekebisho ya sheria kuanzishwa kwa Shirika la Bandari Nam. 1 ya mwaka 1997 yenye lengo la kuweka mazingira bora ya uendeshaji na udhibiti wa bandari pamoja na kukuza uwiano na mashirikiano mazuri kati shirika na Mamlaka ya Usafiri wa Baharini.

Wakati wa kuujadili mswada huu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu walishauri kuwepo na udhibiti na usimamizi mzuri wa uuzwaji wa tiketi za kusafiria ili kudhibiti upakiaji wa idadi kubwa ya abiria kuliko uwezo wa vyombo hivyo. Aidha suala la ujenzi wa gati lilichukua nafasi kubwa katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe na walishauri kuwa serikali ijenge bandari itakayokidhi mahitaji ya hivi sasa na baadae.

Niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba serikali inaendelea na jitihada za kuzungumza na washirika wa maendeleo, ili kupata fedha kwa ajili ya kuliendeleza eneo la Mpigaduri kwa kujenga bandari ya kisasa. (*Makofi*)

Aidha ninachukua fursa hii kuzitaka taasisi zote zinazohusika na usimamizi wa uuzwaji wa tiketi kuhakikisha kwamba suala la uuzwaji wa tiketi kiholela linadhibitiwa na kwamba yeyote atakayekwenda kinyume na sheria zilizopo atachukuliwa hatua zinazofaa.

Pia niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tushirikiane kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kununua tiketi katika maeneo yaliyoruhusiwa ikiwa ni pamoja na kukataa kununua tiketi zinazouzwa kiholela mikononi mwa walanguzi kwa ajili ya kulinda usalama wao.

Mhe. Spika, mswada wa tatu uliowasilishwa na kujadiliwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ni mswada wa Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na kuweka utekelezaji wa majukumu na uwezo wa mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Wadhifa ya Mwanasheria Mkuu umeanzishwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 55. Katika kifungu cha 56 cha Katiba hiyo kinaeleza kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa ndiye atakayekuwa mshauri mkuu wa kisheria wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, na atatekeleza shughuli nyengine zozote za kisheria zitakazopelekwa kwake au atakazoagizwa na Rais au kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyengine zozote.

Kutokana na mapungufu ya kimsingi ambayo yanaathiri ufanisi wa utendaji kazi, serikali imeona haja ya kuanzishwa kwa sheria hii itakayoiwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Wakijadili mswada huu Waheshimiwa Wajumbe waliishauri serikali kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ishirikishwe kikamilifu katika kuandaa na kufunga mikataba mbali mbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuepuka watendaji kufunga mikataba mibovu. Serikali itaendelea kuitumia ipasavyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa masuala yote yanayohusu sheria ya ufungaji wa mikataba ambapo kitengo maalum cha kusimamia mikataba kitaundwa ili kudhibiti mikataba na nyaraka za serikali.

Mswada wa nne Mhe. Spika, uliowasilishwa ni mswada wa sheria ya Mahakama ya Biashara Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Madhumuni ya mswada huu ni kuanzisha mfumo madhubuti wa kufanya mageuzi na kuimarisha mfumo wa kisheria kitaasisi na utendaji wa shughuli zake hapa Zanzibar.

Pia mswada huu umezingatia changamoto zinazokabili utatuzi wa migogoro ya kibiashara hapa Zanzibar chini ya sheria uliopo sasa ambao unazingatia migogoro ya kibiashara kama migogoro mengine yoyote.

Wakati wakichangia mswada huu Waheshimiwa Wajumbe walieleza kuwa kuna tatizo la kesi kukaa muda mrefu bila ya kusikilizwa na hivyo kuongeza malalamiko ya wadai na wadaiwa wa kesi hizo. Pia imeonekana kuwa kuna tatizo la uwekaji wa kumbukumbu za kesi zote zinazowasilishwa na zilizokamilika.

Mhe. Spika, kupitia sheria Mahakama itaweka utaratibu mzuri kuhakikisha kuwa kesi zote zinazowasilishwa zinasikilizwa kwa muda mfupi zaidi. Aidha suala la uwekaji wa kumbukumbu

za kesi zote na utekelezaji wake utapatiwa ufumbuzi kwa kuanzishwa daftari maalum la kumbukumbu ambalo litahifadhi kesi zote na maamuzi yanayotolewa.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali kwamba Baraza hili pia lilipokea na kujadili ripoti za utekelezaji wa maagizi ya kamati za kudumu za Baraza kwa wizara kwa mwaka 2011/2012 pamoja na ripoti za kudumu za Baraza kwa mwaka 2012/2013.

Waheshimiwa Mawaziri walitoa ufafanuzi wa kina na kwa ufasaha hoja zote zilizojitokeza. Ninachukua nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana wenyeviti wa kamati na wajumbe wao kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuishauri serikali katika kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

Aidha ninapenda pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi wa hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wawakilishi, ninaamini hoja na ufafanuzi uliotolewa ni kwa lengo la kuimarisha utendaji wetu katika sekta mbali mbali za serikali, ili serikali yetu iendelee kuaminika mbele ya macho ya wananchi inayowatumikia.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa namna walivyoichangia ripoti ya *PAC* kwa hisia kali zilizoonesha utendaji dhaifu wa watendaji wetu kwa matumizi yasiyoridhisha ya pesa za serikali katika mawizara na taasisi mbali mbali za serikali. Nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Omar Ali Shehe, pamoja na wanakamati wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kufanya uchunguzi wa kina kwenye mawizara na taasisi mbali mbali za serikali mpaka wakaiwasilisha ripoti nzuri kama hii.

Mhe. Spika, mawaziri wakiwa ni wasimamizi wakuu wa watendaji wao, wamezisikia hisia hizo na watafanya kila linalowezekana kuzirekebisha kasoro zilizoonekana. Nina amini kwa kasoro hizo zitarekebishwa na hazitarejewa tena hapo baadaye.

Mhe. Spika, katika michango iliyohusiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, liligusiwa suala la mafuta na gesi asilia kutolewa kutoka katika orodha ya mambo ya Muungano na suala hili lilipofikia wapi.

Mhe. Spika, kamati yetu inaongonzwa na Wanasheria Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, bado inalifanyia kazi suala hili. Tunategemea tutapata taarifa ya awali namna suala hili linavyoendelea tutakapofanya kikao chetu cha pamoja, kati ya SMT na SMZ chini ya uwenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuzungumzia kero za Muungano, kitakachofanyika tarehe 28 April, 2013.

Lakini niseme tu Mhe. Spika, kwa suala hili sio rahisi kama tulivyofikiria lina mambo mengi ya kiufundi ambayo ndiyo yanayofanyiwa kazi na wanasheria wakuu wa serikali wa pande hizi mbili. Hata hivyo, nina matumaini makubwa kwamba wanasheria wetu hawa wa SMT na SMZ watalifikisha jambo hili mahala pazuri kwa muda mfupi utakaowezekana.

Mhe. Spika, wakati wa kujadili ripoti ya Wizara ya Katiba na Sheria, baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe waliitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, itowe kauli yake kama serikali ya kutoa muongozo kuhusu suala la hatima ya Zanzibar katika suala zima la mjadala wa Katiba.

Mhe. Spika, kama nilivyokwishaeleza hapo mwanzoni, mchakato wa Katiba sasa unaingia katika hatua yake ya pili, baada ya hapo zitabaki hatua za kufanyika kwa Bunge la Katiba, kujadili rasimu ya Katiba hiyo na hatimaye hatua ya Kura ya Maoni.

Mhe. Spika, suala la mchakato wa Katiba linaendeshwa kwa kufuata sheria iliyotungwa kwa pamoja, baina ya pande mbili za Muungano na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia Baraza lako tukufu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika kutokana na mchakato wa Katiba kuendeshwa kwa kufuata sheria, ambao umeweka utaratibu mzima wa kuliendesha zoezi hilo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama serikali haina kauli ya kutoa muongozo wala msimamo juu ya jambo hili, tunaiwachia Tume ya Katiba ifanye kazi yake.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu ya ufungaji wa Kikao cha Baraza cha mwezi January 2013, nililielezea Baraza lako tukufu, kwamba maandalizi ya ununuzi wa meli ya abiria yameshakamilika, kilichosalia ni utiaji wa saini. Tumechelewa kukamilisha uwekaji wa saini mkataba wa kutengeneza meli hiyo kutokanana kwamba tulitaka tupate meli itakayokidhi haja yetu, meli hiyo itabeba abiria 1200 pamoja na mizigo isiyopungua tani 200. Aidha, meli hiyo itaweza kuhimili bahari yetu hasa mkono wa Nungwi.

Sasa napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa maandalizi yote juu ya ujenzi wa meli hiyo mpya ya abiria, pamoja na mchoro wa meli yenyewe yamekamilika na fedha tulizokusanya zitatumika kulipia sehemu ya gharama ya ujenzi wa meli hiyo. Ni matarajio yangu kuwa utiwaji wa saini utakamilika ndani ya mwezi wa May, 2013. Kadhalika, ujenzi wa meli hiyo unatarajiwa kuchukua miezi 18 baada ya utiwaji wa saini.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru tena wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako, Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliendesha Baraza hili vizuri na kwa ufanisi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Pia nawashukuru Waheshimiwa Wawakilishi kwa kutekeleza majukumu yao ya kuishauri serikali na mwisho nawashukuru wananchi wote kwa kufuatilia mwenendo wa Baraza letu hili. *(Makofi)*

Vile vile nawashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi wetu wa wananchi kwa michango yao ya uwazi, ambayo ilikuwa na nia ya kuimarisha utendaji wa serikali. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na tumeupokea ushauri wao kwa mikono miwili, pamoja na kupokea mawazo na mapendekezo yao na kuahidi kuyatekeleza.

Nimefarijika sana pale ambapo mawaziri waliofanya vizuri wamesifiwa na kupongezwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili waweze kufanya vizuri zaidi katika siku zinazokuja. Naomba sana mwenendo huu uendelee.

Pia napenda kuwapongeza waandishi wa habari pamoja na wale wenzetu wanaotafsiri kwa njia ya alama kwa kuwawezesha wananchi wetu kuelewa nini kilichokuwa kinaendelea ndani ya Baraza. *(Makofi)*

Mwisho Mhe. Spika, niwatakie Waheshimiwa Wawakilishi kila la heri na mafanikio mema katika kuwatumikia wananchi kwenye majimbo yao na ninawatakia safari njema na ya salama ya kurejea majimboni mwao kuendelea kuwatumikia wapiga kura wao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako tukufu, hadi siku ya Jumatano ya tarehe 12 Juni, 2013 saa 3:00 barabara za asubuhi. *(Makofi)*
Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tunakushukuru kwa hotuba hiyo safi, ambayo imetoa mambo mengi yanayohusu shughuli zetu, lakini pia mambo mbali mbali yanayohusu nchi yetu. *(Makofi)*

Nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano makubwa mlionipa, pamoja na kuwashukuru wasaidizi wangu wote akiwemo Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza. Katibu nampa shukrani za pekee yeye pamoja na watendaji wake, kwa kutoa mashirikiano makubwa sana ya kufanya shughuli zetu hizi zikafikia hapa zilipofikia. *(Makofi)*

Waandishi wa habari pamoja na watu wa kamera wametusaidia sana katika shughuli zetu. Naomba nichukuwe nafasi hii kuungana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuwashukuru sana kwa kupitia kwa Waziri wao wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, hakuna kazi nyengine isipokuwa sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ya kuakhirisha mkutano huu mpaka tarehe 12 Juni, 2013 siku ya Jumatano saa 3:00 za asubuhi wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumaliza kabisa shughuli yetu kuna matangazo mawili. Tangazo la kwanza Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo anawakumbusha Waheshimiwa Wajumbe wanawake, kwamba yale mazoezi yatakuwa yanaendelea kwa siku za Alhamis, Ijumaa na Jumamosi saa za asubuhi, nadhani katika viwanja vya hapa. Mazoezi hayo ni kwa ajili ya mchezo wa *netball*.

Tangazo la pili Waheshimiwa Wajumbe, tunaombwa radhi na Mhe. Mnadhimu wa Wawakilishi wa CCM, kwamba ule mkutano ambao ulikuwa umepangwa ufanyike siku ya Jumapili pale Ofisi

Kuu Kisiwandui, sasa umeahirika mpaka pale mtakapopewa taarifa nyengine, mkutano huo mtapewa taarifa lini utafanyika tena.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo nakushukuruni tena kwa mashirikiano makubwa mlionipa na sasa naakhirisha kikao hiki mpaka tarehe 12 Juni, 2013 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 2:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 12 Juni, 2013 saa 3:00 za asubuhi)

WIMBO WA TAIFA